# Misingi ya Jamii Huru

# Misingi ya Jamii Huru

EAMONN BUTLER

Uhuru Initiative for Policy & Education

Dhima ya Taasisi ya Masuala ya Kiuchumi (IEA) ni kuboresha uelewa wa watu kuhusu taasisi za msingi za jamii huria, hasa kwa kuonyesha kazi ya masoko katika kutatua matatizo ya kiuchumi na kijamii.

Hakimiliki © Institute of Economic Affairs, 2013

Haki ya kimaadili ya mwandishi imetambuliwa.

Haki zote zimehifadhiwa. Pasipo kuzuia haki chini ya haki zilizohifadhiwa hapo juu, hairuhusiwi kuchapisha sehemu ya kazi hii, kuihifadhi au kuiweka kwenye mfumo wowote au kusambazwa kwa namna yoyote (kielektroniki, urudufishaji, kunakili, au namna yoyote), pasipo ruhusa ya maandishi ya mmiliki na mchapishaji wa kitabu hiki.

## YALIYOMO

**KUHUSU MWANDISHI** .......... 4
**DIBAJI** .......... 5
**SHUKRANI** .......... 7
**MUHTASARI** .......... 8

**1 UTANGULIZI** .......... 10
Madhumuni ya kitabu hiki .......... 10
Namna kitabu kilivyopangiliwa .......... 11

**2 MANUFAA YA KIMAADILI NA KIUCHUMI YA UHURU** .......... 13
Jamii huria .......... 13
Suala la maadili kwa uhuru .......... 17
Suala la uchumi kwa uhuru .......... 25

**3 TAASISI ZA JAMII HURIA** .......... 39
Jamii bila serikali .......... 39
Kwa nini seriali ziwe na ukomo .......... 42
Njia za kudhibiti serikali .......... 54
Kuweka kanuni .......... 61

**4 USAWA NA KUKOSEKANA USAWA** .......... 64
Usawa katika Jamii huru .......... 64
Aina za Usawa .......... 65

Usawa wa matokeo.......... 73
Usawa na haki .......... 78
Uharibifu zaidi wa usawazishaji.......... 82
**5 BIASHARA HURIA** .......... 86
Uchumi wa soko huria.......... 86
Jinsi ya kuwa tajiri .......... 90
Hakuna kushikilia nguvu ya kiuchumi.......... 91
Ujasiriamali .......... 92
Faida na ukisiaji.......... 94
Jinsi masoko yanavyofanya kazi .......... 96
Masoko hayawezi kuwa timilifu.......... 97
Mipango mikuu isiyowezekana.......... 98
Makampuni yanayofadhiliwa na serikali.......... 100
Biashara ya kimataifa.......... 101
**6 MALI NA HAKI** .......... 105
Mali binafsi.......... 105
Kanuni za haki .......... 110
Utawala sheria.......... 117
Haki za binadamu.......... 122
**7 JAMII HURIA** .......... 126
Utaratibu bila shuruti .......... 126
Uvumilivu.......... 130
Tatizo la uungwana.......... 141
**8 UBINAFSISHAJI NA UTANDAWAZI**.......... 147
Uhamiaji na teknolojia .......... 147
Kukuza jamii huria .......... 148
Haki za umiliki mali zikiwa kazini .......... 150
Huduma za kibinadamu pasipo serikali.......... 159

Utandawazi na biashara ....................................................167
Umuhimu wa amani ..........................................................171

**9 MJADALA KWA UFUPI** .................................................174

Kuhusiana na uhuru .........................................................174
Serikali yenye mpaka ........................................................175
Usawa mkubwa zaidi .........................................................175
Uchumi huria ...................................................................176
Haki na utawala wa sheria .................................................177
Jamii huria ......................................................................178
Ulimwengu wa uhuru ........................................................179

## KUHUSU MWANDISHI

Eamonn Butler ni Mkurugenzi wa Taasisi ya Adam Smith, kituo cha kinachoongoza cha utungaji sera. Ana shahada katika uchumi, falsafa na saikolojia, akipata shahada ya uzamivu kutoka Chuo Kikuu cha St. Andrews mwaka 1978. Mnamo miaka ya 1970, alifanya kazi kwenye Bunge la Wawakilishi la Marekani, kabla ya kurudi Uingereza kusaidia kuasisi Taasisi ya Adam Smith. Mwaka 2012 alitunukiwa shahada ya heshima ya udaktari wa fasihi na Shule ya Biashara ya Edinburgh. Kwa sasa ni Katibu wa Jumuiya ya Mont Pelerin.

Eamonn ni mwandishi wa vitabu vingi kuhusu wachumi waasisi Milton Friedman, F. A. Hayek na Ludwig von Mises na kinara wa SHule ya Uchumi ya Austria. Kwa IEA, ameandika miongozo juu ya Adam Smith, Ludwig von Mises na nadharia ya chaguo la umma. Pia ni mwandishi mwenza wa historia ya malipo ya posho, udhibiti bei na mfululizo wa vitabu kuhusu IQ. Kazi zake maarufu za hivi karibuni *The Best Book on the Market*, *The Rotten State of Britain* na *The Alternative Manifesto*, vimevutia wengi na huchangia katika vyombo mbalimbali vya habari na utangazaji.

## DIBAJI

Misukosuko ya kisiasa na kiuchumi mara nyingi imepelekea uhuru kushambuliwa. Wakati wa Anguko Kuu la kiuchumi, nchi zote kubwa kiuchumi zilidhibiti biashara kwa kuongeza kodi za forodha. Mwitikio huu wa ghafla uliishia tu kukuza wasiwasi wa kisiasa ya maeneo na kuongeza zaidi hali ngumu ya kiuchumi. Kuibuka kwa tawala za kisoshalisti kulipelekea kugandamizwa kabisa kwa uhuru kwa kiraia, kisiasa na kiuchumi kwa karibu nusu ya dunia.

Hivi karibuni, matukio ya kigaidi ya 9/11 na mwitikio uliofuata wa Marekani umepelekea sera zilizotoa kafara uhuru ili kuongeza usalama. Vivyo hivyo, msukosuko wa kiuchumi ulioanza mwaka 2008 na ambao pia ulianzia Marekani, umefuatiwa na udhibiti zaidi, kanuni na ulindaji. Badala ya kutegemea mfumo bunifu wa kanuni ya kubomoa wa soko huria, serikali za pande zote za Atlantic zimetumia pesa nyingi ya walipa kodi kuziokoa biashara zilizokuwa zinaanguka.

Bado kuna vitisho kwa uhuru. Robo karne iliyopita, ulimwengu ulikaribisha uwazi katika Jumuiya ya Kisovieti, kasha ukashangilia kuanguka kwa ukuta wa Berlin. Lakini changamoto mpya sasa zimeibuka kwa mfumo wa utaifa mpya barani Ulaya na msimamo mkali Mashariki ya Kati. Mwelekeo wote utapunguza uhuru ikiwa utaendelea bila kushughulikiwa. Barani Ulaya, kurejea huku kwenye utaifa na hata ubaguzi rangi

kunaendelea japo kuna kiwango cha juu cha uhuru wa kisiasa – na demokrasia ifanyayo kazi. Mashariki ya Kati kuibuka kwa msimamo mkali wa kidini hakushtui zaidi – si masoko wala demokrasia iliyo katika hali nzuri.

Pamoja na matatizo haya, watu katika karne ya 21 wako huru zaidi kuliko watangulizi wao wa karne iliyopita. Mapinduzi ya teknolojia ya habari na mawasiliano yameondosha vikwazo vya kila aina. Nchini China kwa mfano, Li Chengpeng ni mwandishi na mkosoaji maarufu: blogu yake ya Sina Weibo ina wafuatiliaji zaidi ya milioni sita. Na wakati wa Mabadiliko katika nchi za Kiarabu, mitandao ya Kijamii imesaidia kusambaza maendeleo kisiasa na kijamii. Ikiwa habari ni nguvu, basi teknolojia ya habari imempa nguvu mtu. Mipaka ya kijiografia bado ipo lakini inazidi kupoteza maana yake.

Kwa muktadha huu, chapisho la Eamonn Butler limekuja kwa wakati. Misingi ya Jamii Huru ni nyongeza inayokaribishwa kwenye familia ya kisasa ya miongozo juu ya uhuru. Ujuzi wa kipekee wa Butler na uwezo wake kuelezea mawazo tata na yenye ushawishi mkubwa kwa lugha rahisi. Pia kwa mafanikio amekosoa maelezo ya wakosoaji na wapinzani kwa mifano kuntu ambayo inaonyesha mawazo yake na kuunga mkono maelezo ya nadharia zake.

Hivyo, makala hizi ni utangulizi mzuri kwa wale wanaopenda kuelewa kanuni za msingi za jamii huria. Zitakuwa muhimu hata zaidi kwa wale wanaochochea uhuru kwenye nchi ambako kanuni hizi hazifahamiki zaidi, na pia kwa wale wanaolinda uhuru kwenye maeneo ambako desturi ya uhuru inavamiwa.

ALI SALMAN
Muasisi na Mkurugenzi Mtendaji,
Policy Research Institute of Market Economy (PRIME),
Islamabad, Pakistan
Septemba 2013

Maoni yaliyoelezewa kwenye kitabu hiki, kama ilivyo kwa vyote vya IEA, ni ya waandishi husika na siyo ya Taasisi (ambayo haina maoni ya kitaasisi) wala bodi ya wadhamini, wajumbe wa Baraza la Ushauri wa Kitaaluma au watendaji wake wakuu. Isipokuwa kwa baadhi ya mambo kama vile machapisho ya muhadhara, vitabu vyote vya IEA hupitiwa na angalau wanataaluma au watafiti wawili waliobobea kwenye tasnia husika.

# SHUKRANI

Shukrani maalumu ziende kwa Nigel Ashford, ambaye amemruhusu mandihi kukopa mawazo mengi kutoka kwenye kitabu chake '*Principles for a Free Society*'. Rasilimali nyingine muhimu zinajumuisha vitabu vya H. B. Acton, *The Morals of Markets*, pia *On Liberty* cha J. S. Mill, *Freedom 101* cha Madsen Pirie, *A Beginner's Guide to Liberty* cha Richard Wellings, *Why Freedom Works* cha Ernest Benn na *The Morality of Capitalism* cha Tom Palmer.

## MUHTASARI

- Uhuru huleta ustawi. Hufungulia vipawa vya watu na ubunifu, vikiunda utajiri ambapo haukuwepo kabla. Jamii ambazo zimekumbatia uhuru zimejitengenezea utajiri. Ambazo hazijakumbatia uhuru zimesalia masikini.
- Watu kwenye jamii huria hawawi matajiri kwa kuwanyonya wengine, kama ambavyo watu wa tabaka la wasomi lifanyavyo kwenye nchi zisizo huru. Hawawezi kuwa matajiri kwa kuwafanya wengine masikini. Wanakuwa matajiri kwa kuwapa wengine wanachohitaji na kuboresha maisha ya wengine.
- Wanufaika wakuu wa mabadiliko ya kiuchumi kwenye jamii huria ni masikini. Jamii huru zina usawa zaidi kuliko jamii zisizo huru. Masikini kwenye jamii huru zaidi wanafurahia fahari ambazo hazikuwazika miaka michache tu iliyopita, starehe ambazo zinapatikana kwa tabaka tawala la jamii zisizo huria.
- Biashara ya kimataifa huwapa wajasiriamali fursa mpya za masoko na kusaidia kuinua zaidi ya watu bilioni kutoka kwenye umasikini wa kupindukia katika miaka ishirini iliyopita. Kweli uhuru ni moja ya nguvu zenye msukumo sana kwenye historia ya binadamu.
- Majaribio ya serikali kusawazisha utajiri au kipato yamekuwa kinyume na uzalishaji. Yameharibu motisha ya kufanya kazi kwa bidii na biashara na kuvunja moyo watu kujenga mitaji inayoweza kuchochea uzalishaji

kwenye jamii nzima.

- Jamii huria ni jamii inayokua yenyewe. Hujengeka kutokana na matendo ya watu binafsi, kufuatia kanuni zinazochochea ushirikiano kwa amani. Si kwa kuwekwa kwa lazima na mamlaka za kisiasa.
- Serikali ina jukumu dogo lenye ukomo kwenye jamii huria. Ipo kuzuia madhara kutokea kwa raia wake kwa kulinda na kusimamia haki. Haijaribu kuweka usawa wa mali na haijaribu kuzuia shughuli kwa kuwa tu watu wengine wanaziona hazikubaliki au zisizopendeza. Viongozi hawawezi kuwapora wananchi kwa manufaa yao wenyewe, na kuwapendelea rafiki zao au kutumia mamlaka yao dhidi ya maadui zao.
- Serikali ya jamii huria imedhibitiwa na utawala wa sheria. Sheria zinafanya kazi kwa kila mtu sawasawa. Kunapaswa kuweko mchakato wa haki wa sheria katika kesi zote, kukiwa na uendeshaji wa kesi kwa haki na kutoshikiliwa muda mrefu pasipo mashtaka. Watu waliotuhumiwa kwa makosa wanapaswa kuchukuliwa kutokuwa na hatia mpaka ithibitike vinginevyo, na watu hawapaswi kunyanyaswa kwa kushtakiwa kwa jambo lile lile kila mara.
- Kuvumilia mawazo na mtindo wa maisha wa watu wengine huifaidia jamii. Hatuwezi kuwaamini wadhibiti kuyabana mawazo yasiyofaa pekee. Wanaweza kukosea na kubana mawazo na namna ya kuenenda ambayo ingeweza kuisaidia sana jamii huko mbeleni.
- Teknolojia ya mawasiliano imefanya iwe vigumu hata zaidi kwa serikali za kiimla kuficha matendo yao kwa wengine. Matokeo yake, nchi nyingi zaidi zinafunguka kwa ajili ya biashara na utalii, mawazo mapya pia yanasambaa. Watu wengi zaidi wanaona manufaa ya uhru wa kiuchumi na kijamii, na wanaudai.

# 1 UTANGULIZI

## Madhumuni ya kitabu hiki

Kitabu hiki kinaainisha kanuni za msingi zinazoelezea jamii huru. Sababu gani kinahitajika ni kwa sababu uhuru wa kweli wa mtu binafsi, jamii, kisiasa na kichumi ni adimu sana – hata katika nchi zinazojidhania kuwa huru. Ni kweli kuna tofauti kubwa baina ya nchi huru sana na zile zisizo huru sana, lakini katika kila nchi, kwa kiasi kikubwa au kidogo maisha ya kijamii na ya kiuchumi ya watu yanadhibitiwa au kuongozwa na maafisa wa serikali au wanasiasa. Udhibiti huo umekuwepo kwa muda mrefu sana, na huzuia kiwango kikubwa cha maisha yetu ya kila siku kiasi kwamba imekuwa sehemu ya utamaduni wetu. Watu wanachukulia kuwa sehemu ya maisha, asili kabisa na isiyokwepeka.

Matokeo ni kwamba, wengi ulimwenguni, hata ikiwa wanaamini wanaishi katika jamii huru, hawawezi kudhania kabisa uhuru wa kweli una maanisha nini – achilia mbali kuelewa jamii huru ingeonekanaje na ingefanyaje kazi.

Mbali na hayo, watu wanataka uhuru. Wanataka kuwa na uwezo wa kufanya biashara pasipo kukumbana na ulazima wa kuwa na vibali visivyo na idadi. Wanataka kuwa na uhakika wa kudumu kwa nyumba zao, mashamba na

karakana zao badala ya kuwa katika hatari ya wanasiasa kuwaondosha na kuwaharibia. Wanataka kuamua njia gani ni bora kwa familia zao kuliko kile maafisa wa serikali wanakiamua. Wanataka kuendelea na maisha yao bila kulazimika kuwahonga askari au warasimu ili wasiwasumbue.

Ndiyo maana ni muhimu sana kuweka kanuni za msingi za uhuru wa kijamii na kiuchumi. Uelewa mzuri wa nini maani ya uhuru, namna gani hufanya kazi, ni msingi ambao watu wanaweza kujengea jamii huru haswa.

## Namna kitabu kilivyopangiliwa

Sura ya 2 inaleezea siyo tu manufaa ya *kiuchumi* ya kuwa na jamii huru, bali pia ya *kimaadili* kuhusu uhuru. Uchumi huru na jamii huru vimejengwa katika maadili ya kina sana – siyo maadili yanayotoa changamoto kwa mifumo mingine ya maadili, bali inayojali, kuthamini, kuimarisha na kuwezesha. Uhuru ni kwa ajili ya kila mmoja.

Sura ya 3 inaelezea jinsi jamii huru inavyoweza kumpa mtu mahitaji yake kwa namna ya ufanisi mno pasipo kuhitaji watawala wenye nguvu kumweleza kila mmoja nini cha kufanya. Inaelezea hasa kwa nini serikali ziwe na *ukomo* wa ukubwa na madaraka, na inelezea namna jamii huru inaweza kuonekana na namna gani inapaswa kufanya kazi.

Sura ya 4 inajadili mvutano baina ya *uhuru* na *usawa*. Inaeleza kuwa uhuru zaidi kiuhalisia huleta usawa zaidi katika kila kinachohusika. Lakini majaribio ya kuweka usawa wa matokeo kwenye jamii unapuuza kanuni za uhuru na kuleta madhara ya muda mrefu.

Sura ya 5 inaonyesha mfumo wa kiuchumi wa jamii huru, ikielezea namna masoko, yakiwekwa huru na usimamizi wa serikali, huweza kutengeneza na kusambaza ustawi. Inaelezea kanuni tunazofuata kufanya mchakato huo kufanya kazi kwa urahisi na umuhimu mkubwa wa biashara huria katika kuchochea ushirikiano wa watu.

Sura ya 6 inachunguza kanuni za *mali* na *haki*. Inaelezea namna gani sheria za jamii huru zinapaswa kuwa za ujumla, zikifanya kazi kwa walioko mamlakani kama ilivyo kwa watu wa kawaida, ikiwa tunahitaji kupunguza matumizi ya nguvu na unyonyaji. Na inaelezea namna gani jamii huru inaheshimu haki za msingi za binadamu.

Sura ya 7 inaelezea kwa undani zaidi namna jamii huru inafanya kazi pasipo kuhitaji kushurutishwa na walioko madarakani. Inaonyesha kanuni za msingi za *kimaadili* na *kitabia* ambazo huleta utaratibu mzuri wa kijamii ulio huru. Inasisitiza juu ya uhitaji wa kuwepo *uvumilivu* na inaelezea matatizo kwa kuiegemeza jamii kwenye uungwana.

Sura ya nane inaangazia namna ya kujenga jamii huria pale isipokuwepo. Inaonyesha umuhimu wa kuboresha motisha katika maisha ya kila siku, na upuuzi wa kujaribu kulazimisha maamuzi kutokea juu. Inaonyesha kuwa hata huduma muhimu zinaweza kutolewa pasipo serikali. Na inasisitiza umuhimu wa *biashara huria* na *amani*.

# 2 MANUFAA YA KIMAADILI NA KIUCHUMI YA UHURU

## Jamii huria

*Uhuru una maana gani*

Uhuru una maana zaidi ya kutokuwa kifungoni au utumwani tu. Una maana ya kukupa haki ya kutenda, kuongea na kuwaza ulivyochagua, pasipo vikwazo vya kiunyanyasaji vinavyowekwa na wengine, ikiwa ni pamoja na walio madarakani. Unahusika kwenye maisha yako binafsi, ya familia yako, na ya jamii yako, pamoja na mtazamo wako kisiasa na shughuli zako za kiuchumi na watu wengine.

Jamii huru ni ile ambayo inataka kufuata mambo haya. Zamani na sasa, uhuru umechochea kwa mafanikio kutengeneza utajiri na kuusambaza kwa raia. Umethibitika kuwa moja ya nguvu kazi ya kibunifu na fanisi zaidi. Umeboresha maisha ya watu – hasa walio masikini zaidi – kotekote ulimwenguni.

Uhuru maana yake hakuna vikwazo kuwekwa mbele yako, hakuna vizuizi shidi ya kutenda unavyoamua. Unamaanisha kutolazimishwa, kutoelekezwa, kutotishwa, kutosongwa, kutopandikiziwa, kutoingiliwa au kutochezewa na wengine. Unamaanisha kuwa na uwezo wa kuendelea na maisha yako pasipo kushambuliwa, kuhongwa, kuporwa au kuumizwa. Hiyo iko hivyo kwa sababu kanuni za uhuru

zinafanya kazi sawa kwa kila mmoja kwenye jamii huru. Hakuna miongoni mwetu mwenye haki ya kuingilia, kuzuia au kuumiza wengine, kitu ambacho kingeharibu uhuru ambao wao pia wanao.

Hivyo, uhuru upo tu ikiwa watu wengine hawajaumizwa. Haki yako ya kuzungusha ngumi inaishia pale pua yangu inapoanzia. Hautumii uhuru wako pale unapotishia, kulazimisha, kupora, kushambulia au kuua wengine. Kinyume chake, unazuia uhuru wao kwenda sawa. Kanuni hii huitwa kutodhuriana: *uko huru kufanya chochote utakacho, ila tu kisiwaumize wengine.*

Vivyo hivyo, hauzuii uhuru wa mtu yeyote ikiwa unapinga ubabe wao. Uhuru na kanuni ya kutodhuriana huruhusu wewe kuzuia watu wengine kukudhuru wewe na wengine unaowajali. Pia una uhalali wa kuingilia jambo ili kuzuia mabaya kutokea kwa mwingine, ikiwemo usiowafahamu – japo jukumu hili la kuwalinda raia mara nyingi limeachiwa polisi na mamlaka za kisheria.

Hata hivyo, kanuni ya kutodhuriana hufanya kazi pale wengine wanapoumizwa. Inaruhusu wewe kufanya unachotaka na mwili wako, na mali yako, iwe tu haukiuki uhuru wa wengine katika kufanya hivyo. Kwa mfano, unaweza kutoa mali zako zote, kujihatarisha kuumia kwa kufanya kitu cha hatari au kuumiza mwili wako, ikiwa tu hilo halimuumizi mtu mwingine yeyote. Na japokuwa watu wengine wanaweza kutia moyo usijiumize, hawawezi kukuzuia, ni chaguo la kujitakia mwenyewe.

*Uhuru na jukumu la serikali*

Inaweza kuonekana haifai kusemakuwa hatuna uhuru wa kuingilia matendo ya watu wengine, hata ikiwa ni

kwa ajili ya manufaa yao wenyewe. Lakini hakuna yeyote kati yetu anayeweza kujua hasa kipi ni cha maslahi kwa wengine. Watu wanajua wenyewe kipi ni cha ustawi kwao. Wana uelewa mzuri zaidi wa maadili yao, hali, mahitaji, matakwa, matumaini na matarajio kuliko mwingine yeyote. Wao ni waamuzi wazuri zaidi wa malengo na matendo yao.

Mtu wa nje anaweza kuchukizwa na namna tunavyowachukulia wengine. Ikiwa tutaruhusu watu kuingilia uhuru wa wengine, wanawez kufanya hivyo kwa njia nyingi (kwa kujua au kutokujua) kujinufaisha wenyewe badala ya mtu mwingine. Ndiyo maana maamuzi ya kumweka mtu kizuizini yameachiwa polisi na mahakama, ambao – kwenye jamii huru hasa, angalau – wanaweza kutokuwa na upendeleo kuhusu jambo husika.

Vyovypte tuwavyo, mahitaji yetu binafsi yanahudumiwa kwa namna bora zaidi kwa kuwa kwenye jamii ambako tuko huru. Kazi ya serikali kwenye jamii kama hiyo ni kulinda uhuru wetu dhidi ya kuharibiwa na wengine – na kwa kuusambaza kule usikofika bado na kuukuza pale ambapo haujatimia. Pale watu wanapokuja pamoja kuunda serikali au mamlaka yoyote juu yao, hiki ndicho huwa nacho kwenye mawazo yao: kulinda na kukuza uhuru wao, na si kuuzuia.

Mara nyingi hata hivyo serikali hazikuundwa kwa namna hii. Huwekwa juu ya watu na makundi yaliyo tayari kutumia nguvu kunufaisha maslahi yao wenyewe, na si kuongeza uhuru wa kila mtu. Unyama huo mara nyingi hutokea kukiwa na ushiriki kamili wa watu wengi, ambao wanaweza kujikuta wakinufaika kwa kuwanyonya walio wachache. Lakini uhuru siyo idadi: ili ulete maana yoyote, inabidi uwepo kwa usawa kwa watu wote.

Hata serikali ambazo zinajali maslahi ya jumla ya watu, mara nyingi hugandamiza uhuru kwa sababu hazielewi kikamilifu au kuheshimu kanuni ya kutodhuriana, wala hazioni madhara ambayo matendo yao yamesababisha. Udhibiti wa serikali kwa mfano, unaweza kuzuia mawazo fulani au maneno au picha kutangazwa au kusemwa, ikiaminika kuwa haya huweza kuleta madhara kwa watu. Lakini katika mchakato huo wanawadhuru waandishi, wasanii, watengeneza filamu, wanahabari na wengine wenye vipaji kwa kulemaza uhuru wao wa mawazo na kujieleza, wakikwamisha taaluma zao na kuwanyima fursa ya kufurahia matunda ya kazi, ubunifu na akili zao. Na mara kanuni ya udhibiti inapokubalika, inakuwa rahisi kwa wale waliopo madarakani kuiongeza – wakizuia ukosoaji wowote wa serikali yao, labda tuseme kwa kugandamiza mawazo yoyote wanayoona yanawatishia.

Na tena, mamlaka zenye nia nzuri tu, zinaweza kuanzisha kodi kwa lengo la kusawazisha kipato, na kutozingatia kuwa hili huondoa uhuru wa walipakodi kufurahia mali zao kama tu ambavyo wizi wa kawaida hufanya. Na kama ulivyo wizi wa kawaida, kitisho cha unyang'anywaji kama huo huwafanya watu wahofie kuweka akiba na kuwekeza – ambayo hatimaye huwa na matokea mabaya kwenye usalama na ustawi wa jumuiya yote.

Serikali hizo huweza kudai kuwa zinafanya kwa maslahi ya umma, lakini nani wa kujua maslahi ya umma ni yapi? Watu tofauti wana maslahi tofauti, ambayo mara nyingi hukinzana. Kuyawianisha maslahi hayo yanayokinzana ni kazi isiyowezekana. Lakini watu binafsi wanaweza zaidi kujua na kutendea kazi juu ya maslahi yao wenyewe kuliko mamlaka zilizoko mbali zinazotumia maafisa wenye nguvu kufnaya hivyo kwa niaba yao.

Mabavu ni uovu. Na japokuwa matumizi fulani ya nguvu – kama vile kuwadhibiti wanyanyasaji – kunaweza kuwa uovu unaohitajika, bado tunahitaji kutafuta kupunguza matumizi ya nguvu kwa kiwango cha chini kabisa. Watetezi wengi wa uhuru hudai kuwa watu wote wana 'haki za asili' – kama vile haki ya kuishi na haki ya kumiliki mali binafsi – ambazo huweka ukomo wa nguvu ya serikali juu yetu. Hatungewaruhusu watu wengine kutupora au kutuwekea vikwazo, sasa kwa nini turuhusu serikali kufanya hivyo?

Kiasi kikubwa cha historia ya binadamu hata hivyo, watu hawajakuwa huru. Serikali hazijaundwa kwa makubaliano ya hiyari baina ya watu binafsi, badala yake zimewekwa na wale walio tayari kutumia mabavu. Lakini hakuna mtu ambaye maisha yake yanaendeshwa kwa amri ya mamlaka fulani ni mtu kamili. Watu wako kamili kimaadili ikiwa wanafanya maamuzi yao wenyewe. Wana thamani ndogo ya maadili ikiwa wengine wanawachagulia. Wanakuwa tu vitu visivyo maana, na si binadamu kamili.

## Suala la maadili kwa uhuru

Uhuru huruhusu watu kuwa binadamu kamili kwa kutumia talanta zao na uwezo wao kama waonavyo inafaa – siyo tu kwa ajili yao wenyewe tu, lakini kwa ajili ya familia zao na wengine karibu yao. Jamii huru siyo mkusanyiko wa watu waliojitenga na wanaojali maslahi binafsi; ni mtandao wa watu wote wa kijamii kwa ujumla. Uwezo wake wa kusaidia binadamu unathibitisha kipimo cha kimaadili cha jamii huru.

*Mizizi ya kiroho na kiutamaduni ya uhuru*
Kama mchumi mshindi wa tuzo ya Nobel Amartya Sen

alivyoonesha, uhuru ni wazo la ulimwenguni pote.[1] Lina mizizi mirefu kwenye karibu kila dini na tamaduni, kuanzia Uislamu mpaka Ubudha, kuanzia Asia mpaka Magharibi. Mtawala wa kihindi, Ashoka alitaka uwepo wa uhuru na uvumilivu kisiasa zaidi ya karne ishirini zilizopita. Mtawala Akbar wa karne ya 16 wa Mughul alikuwa akifanya uchunguzi juu ya uvumilivu hata pale mahakama ya kidini *Inquisition* ilipokuwa ikiwashitaki wapinzani wa dini rasmi barani Ulaya. Uislamu, tangu mwanzoni kabisa, ulikuwa wazi kwa uhuru wa kiuchumi na biashara kabla masuala haya kuanza kuheshimiwa na nchi za Magharibi. Watawala wa Milki ya Uturuki walikuwa wavumilivu zaidi kuliko wafalme wa Ulaya.

Uhuru, kwa maneno mengine ni kupatana kikamilifu na tamaduni zote kuu na dini za ulimwengu. Siyo wazo la kimagharibi, au la ki-rasilimali zaidi, wala halipingani na jamii iliyojengwa kwenye maadili imara. Jamii huru hutegemea katika watu kukubali kwa hiyari maadili na kanuni ambazo huzuia madhara, ufisadi, unyonyaji na matumizi mabaya ya mamlaka – kanuni ambazo husaidia kutengeneza jamii yenye utaratibu mzuri unaowawezesha watu kuishi pamoja na kushirikiana. Ndani ya mfumo huo mpana, uhuru huruhusu watu muamua maadili yao wenyewe, kutunza utamaduni wao wenyewe na kufuata dini zao wenyewe. Hawalazimishwi kukubali maadili, utamaduni na matendo ya mamlaka fulani ya nchi.

*Utamaduni wa kuaminiana na ushirikiano*

Jamii huru haifanyi kazi kwenye misingi ya nguvu na mamlaka, lakini kwenye msingi wa kuaminiana na ushirikiano. Utajiri katika jamii huru huja kupitia

1 Amartya Sen, 'Universal truths: human rights and the Westernizing illusion', Harvard International Review, 20(3), 1998, uk. 40–43.

mbadilishano wa hiyari, kupitia watu kuzalisha bidhaa zinazohitajika na kuziuza kwa wengine. Hauji kwa mbinu za kinyama za wachache za uporaji, kwa kutumia nguvu yao kuchuma kodi kutoka kwa umma au kujipa ukiritimba na upendeleo wao wenyewe, familia zao na marafiki zao. Hiyo inaweza kuwa namna ambayo utajiri umejengwa kwenye nchi nyingi katika historia ya binadamu – kupitia unyonyaji ulioegemea matumizi ya nguvu. Jamii huru badala yake, hutegemea nia nzuri zaidi ya ushirikiano wa hiyari na biashara.

Ili kufanya kazi, ushirikiano na biashara ya hiyari huhitaji kuaminiana. Hakuna atakayefanya biashara na watu anaodhani ni laghai walafi – labda ikiwa amelazimishwa kufanywa hivyo, au hana mbadala (kwa mfano serikali au marafiki zao wanadhibiti uzalishaji). Katika jamii huria, watu wana chaguo na uhuru wa kupeleka biashara zao kwingine, hivyo wazalishaji wanalazimika kuwashawishi wateja – wa sasa na wa baadaye – kwamba wao ni watu wa kuaminika. Wanahitajika kutimiza hadi zao, la, watuharibu sifa yao na kufeli biashara. Na kwa watu wengi, uwezekano wa kupoteza kuaminika na hatimaye chanzo cha kipato chao ni jambo kubwa sana.

Jami huria haiongozwi kutokea juu na tabaka teule linalotumia mabavu. Hufanya kazi kiasili na kwa msukumo wa ndani kwa njia ya mahusiano ya hiyari ya watu wa kawaida – ikitegemezwa na utamaduni wa kuwa wenye kutegemeka na wakweli. Kanuni na desturi zinazoendesha ushirikiano huu unaojisukuma huja kwa namna ya asili kabisa kwenye jamii huru kiasi kwamba watu hawahitaji hata kufikiria kuihusu. Haihitajiki kwamba mamlaka fulani iwaambie watu kuwa wakweli na wafanisi, au kufnaya kazi kwa bidii na kushirikiana na wengine. Watu wanafanya hivyo kwa asili kabisa kila siku.

Uhitaji wa kuaminiana na ushirikiano kwenye jamii huria kunafanya uhusiano baina ya watu na makundi kuwa muhimu kuliko ilivyo kwenye jamii zinazoendehswa kidikteka. Mshikamano wa maadili ya kidini, kifamilia, urafiki, jumuiya, urithi, ujirani na ushirika wa watu wenye mapendeleo yanayofanana huwa muhimu zaidi. Serikali nyingi kwenye jamii zisizo huru huona ushirika wa aina hiyo kuwa hatari kwa mamlaka yao, na hutafuta kuudhofisha, kuufifisha au kuupiga marufuku. Ushirika wa hiyari ni muhimu sana kwa watu kiasi kwamba unakuwa na nguvu kuliko utiifu wa watu kwa mamlaka za serikali.

*Maslahi binafsi na kanuni*

Jamii huria haihitaji amri kutokea juu. Hufanya kazi kupitia watu wa kawaida kurekebisha mipango yao wenyewe na matendo ya kadri ya mipango na matendo ya watu wengine. Kinachowawezesha kufanya hivyo ni seti ya kanuni na maadili rahisi ya pamoja – kama vile ukweli na kutokuwepo vurugu – ambavyo huzuia mgogoro baina ya watu tofauti wenye maslahi binafsi tofauti.

Kanuni hizo za msingi na maadili ya pamoja hufanya zaidi ya kuwaruhusu watu kuishi kwa amani. Pia huwaacha watu huru kushirikiana ili kufanikisha maslahi ya kila mmoja. Kwa mfano, jamii huru huwaacha watu huru kufanya biashara baina yao, kufanya makubaliano ambayo kila upande utaona yana manufaa. Siyo juu ya mamlaka kuamua kipi kitawanufaisha, au kuamua namna gani maslahi yao tofauti yawianishwe, wala kuamua nini kifanyike kufanikisha maslahi yao, au kuwavuta watu kufuata mpango huo. Katika jamii huru, watu wenyewe huamua kipi ni cha maslahi kwao, na huchagua namna nzuri zaidi ya kufanikisha maslahi hayo kwa kushirikiana na

watu wengine. Na wako huru kuingia katika makubaliano yoyote wanayochagua, iwe tu kwamba hakuna mwingine anayeathirika na mchakato huo.

Baadhi ya wakosoaji hawawezi kuona namna gani jamii inaweza kufanya kazi na kustawi bila kuchagua malengo yanayofanana na kuwataka raia wote kufanya kazi kuyafikia. Wanahofia kuwa jamii huru itakuwa vilevile, isiyozalisha na yenye mgongano wa malengo tofauti ya watu binafsi – ambayo hupaswa kugandamizwa kuruhusu maslahi ya umma kuendelea.

Hili ni kosa. Jamii huru hukubali kuwa watu wana maslahi binafsi. Lakini pai hukubali kuwa maslahi bianfsi ni msukumo imara kiasi kwamba haiwezekani kugandamizwa. Watu huchukulia 'maslahi ya umma' – kama yanavyoelezewa na wanasiasa – kama vile yasiyo na haraka wala umuhimu kuliko maslahi yao wenyewe. Na tunapaswa kukumbuka kuwa maslahi binafsi ni msukumo muhimu: ikiwa watu binafsi watapuuzia mahitaji yao binafsi (kama vile chakula, kinywaji, makazi na mavazi), wasingeishi kwa muda mrefu, bila kujali wanaishi kwenye jamii yenye ukarimu kiasi gani.

Jamii huru huelekeza maslahi binafsi kwa njia za kufaa. Hailazimishi bure katika matumaini ya kuunda ukamilifu fulani wa kufikirika. Seti ya kanuni huhitaji tu kwamba watu kutoweka malengo yao juu ya watu wengine. Watu wako huru kufuata maslahi yao wenyewe, kama mtu binafsi, au kwa kushirikiana na wengine, ikiwa tu wanaheshimu uhuru wa wengine wanaofanya kama hivyo. Hawawezi kulazimisha wengine kukubali kutumikia malengo yao wenyewe.

Hofu ya wakosoaji kwamba jamii huru itakuwa

mapambano ya maslahi shindani inanyamazishwa na ukweli kwamba jamii zilizo huru hustawi – na karibu mara zote hustawi vema zaidi kuliko zile zinazoongozwa kibabe. Kwa kutumia seti ya kanuni rahisi ambazo watu huheshimu uhuru wa wengine, na huelekeza maslahi yao binafsi katika ushirikiano wenye manufaa.

Hofu ya kuwa watu kwenye jamii huru watafikiria kuendeleza maslahi yao tu pia imekosewa. Watu ni viumbe wa kijamii. Wana mshikamano wa asili na familia, marafiki na majirani, ambao maslahi yao huwazingatia katika matendo yao. Hutaka sana heshima na kutakiwa mema na marafiki, na heshima ya kuwa majirani wema. Hivyo huwa tayari kuachana na maslahi yao wenyewe ili kuwa na mahusiano mazuri na wengine. Kujali kwao hupewa thawabu, kwa sababu na wengine wanatarajiwa kuwasaidia pia.

Tunaweza kuona hili likifanya kazi zaidi kwenye jamii zilizo huru zaidi, kuwapa wengine , hata wageni kabisa, kupitia uhisani binafsi uko juu zaidi kwenye jamii huru zaidi kuliko zile zisizo huru sana – siyo tu kwa sababu watu wana utajiri zaidi, lakini kwa sababu jamii huru husisitiza kwenye kuwajibika kwa jamii kihiyari, badala ya kule kwa kulazimshwa.

*Ushirikiano kupitia kanuni zilizokubalika*

Kushirikiana kwa mafanikio na wengine, sote tunahitaji kufanya matendo yetu yenye kutabirika na kutegemeka. Ushirikiano utashindikana ikiwa watu wanabadili mawazo yao kila amra, na kuenenda kwa namna tofauti tofauti au kutotimiza ahadi. Jamii huru huruhusu watu kuenenda kadir wachaguavyo kwenye maisha yao binafsi, ikiwa tu hakuna wengine wanaoathiriwa. Lakini pia hutia

moyo hali ya uendelevu katika tabia za watu kitu kilicho muhimu kwenye ushirikiano wa kijamii.

Kwa mfano, jamii huru huwa na kanuni za kisheria kuhusu umiliki, udhibiti na uhamishaji wa mali. Hii huruhusu watu kupata mali na kuwekeza kwenye bidhaa mtaji – kama vile nyumba, viwanda na vifaa ambavyo vitaboresha maisha yao ya baadaye na kufanya uzalishaji kuwa rahisi zaidi na nafuu bila kutishwa na kuporwa au kunyonywa na watu wengine au maafisa. Kanuni hizi ('haki za mali') hazijabuniwa na serikali, lakini zimejengeka kwa miongo kadhaa. Ukomo wake umejaribiwa katika migogoro mingi kwenye mahakama tele, zikijenga sheria na kawaida ambayo hufanya watu kuwa na uhakika zaidi kwenye kushughulika na wengine – na hivyo kufanya ushirikiano kuwa rahisi na wenye matunda zaidi.

Jamii huru zaidi pia zimefikia kukubali kuwa kanuni na desturi nyingine ni muhimu katika uwepo wa ushirikiano mzuri wa kijamii. Kanuni za kimaadili huweka ukomo unaosaidia kufanya mahusiano ya kijamii kuwa rahisi kwa kila mmoja. Na kuna viwango vya jumla vya tabia ya kijamii – mwenendo, upole na desturi za utendaji mzuri wa biashara – ambao umekua kwa kwa kipindi kirefu cha mahusiano ya watu. Desturi hizo za manufaa, japo ni za kawaida kwenye jamii huru, huweza kuwa ngumu au kutowezekana kwa serikali za nchi zisizo huru kuziweka.

Wananchi kwenye jamii huru pia wana haki fulani za msingi za kiraia. Muundo wake halisi unaweza kuwa tofauti, lakini desturi hizi zilizokubalika hujumuisha uhuru dhidi ya kulazimishwa kuwa fanyika kazi au utumwa, uhuru dhidi ya kunyanyaswa au adhabu zisizoendana na makosa. Hujumuisha uhuru wa kuwaza na wa imani – uhuru wa kushikilia mawazo yaki kuhusu dini au siasa,

uhuru wa kuabudu na kushiriki kwenye siasa pasipo vitisho au kunyanyaswa. Hujumuisha uhuru wa kuongea – uhuru wa kujieleza na uhuru wa njia za mawasiliano (redio, televisheni, magazeti na intaneti) kuripoti na kutoa maoni kadri wanavyochagua. Hujumuisha uhuru wa kukusanyika na kufanya ushirika na yeyote unayetaka. Na huhusisha faragha – kutochunguzwa au kufuatiliwa na wengine, hasa wale walioko madarakani. Kwa kifupi, jamii huru hutarajia raia wake kuwa wavumilivu kwa mawazo ya watu wengine, imani zao, mtindo wao wa maisha na matendo yao, na kutowaingilia, kadri ya kanuni ya kutodhuru wengine.

*Haki na utawala wa sheria*

Jamii huru huwa na kanuni za haki. Kuna adhabu kwa kuwadhuru watu wengine, siyo tu kuwadhuru kimwili, bali pia ufisadi na madhara mengine pia. Na pengine, muhimu zaidi, jamii huria hutunza utawala wa sheria. Tatizo kubwa la asasi za kisiasa siyo namna gani tunachagua viongozi wetu – jambo ambalo ni rahisi – bali ni namna gani wanawadhibiti. Katika jamii huria, majukumu na mamlaka ya wakala za serikali yamedhibitiwa sana. Hii huhakikisha kuwa mamlaka waliyopewa kuwalinda raia dhidi ya ubabe na kuwaadhibu watenda makosa hayatumiwi watakavyo wao au kwa maslahi binafsi ya wenye madaraka.

Jamii huru zimetengeneza mbinu za aina zote – kama vile sheria ya uchaguzi, katiba na ugawanyaji wa madaraka – ili kudhibiti madaraka ya maafisa. Lakini njia ya msingi ya kuwalinda wananchi dhidi ya unyonyaji wa watawala wao ni kuhakikisha sheria zinauata mkondo wake kwa wote kwa usawa. Hii inajulikana kama utawala wa sheria. Chini ya kanuni hii, serikali haziwezi kutoa upendeleo kwa

makabila fulani kwa mfano, au kutoza kodi kwa makundi fulani ya kijamii, na sheria zinapaswa kufanya kazi kwa serikali yenyewe na kwa umma.

Vivyo hivyo huwa kwa utekelezaji wa sheria hizi. Ili kuhakikisha kuwa nguvu ya mahakama inatumika ipasavyo na si kwa kufuata hisia, kanuni za haki zinafanya kazi sawa kwa wote katika jamii huria. Raia wana haki ya kutendewa kwa usawa na kupata mchakato sawa wa haki. Hiyo hujuisha kutokamatwa ovyo, kutofungwa jela pasipo mashtaka, kuendesha kesi bila upendeleo kulingana na kanuni za ushahidi, hukumu iliyofanywa na baraza la raia wa kawaida badala ya maafisa wateule na kutoshtakiwa kwa kesi hiyo hiyo mara kwa mara.

Matokeo ya udhibiti huu kwa wanasiasa, maafisa na majaji ni kupunguza utumizi mbaya wa madaraka na wale walioko madarakani, na kuzuia upendeleo maalumu na kupunguza maovu ya matumizi ya nguvu. Na pamoja na yote, jukumu la serikali katika jamii huru ni kulinda raia na kupanua wigo wa uhuru kwa watu, na si kuuzimisha.

## Suala la uchumi kwa uhuru

*Kukua sana kwa viwango vya maisha*

Mpaka miaka ya 1750, maisha ya bianadamu hayakuwa yamebadilika sana. Karibu kila mtu alifanya kazi nje, kwenye mashamba, kazi ya kutumia nguvu ambayo haikuwa na uhakika, yeny kutegemea hali ya hewa, kazi ya kulima chakula. Njia za kilimo zilikuwa karibu vilevile kama ilivyokuwa enzi za farao. Watu wengi hawakuwa na fedha kwa mambo ya kifahari kama vile nguo ya ziada. Wachache waliweza kumudu kununua nyama. Matajiri wa kuonekana wachache tu walikuwa wale waliozaliwa

kwenye utajiri. Na kawaida, utajiri huo ulianzia kwenye uwepo wa nguvu ya kuwatoza kodi wakulima wadogo kwa manufaa yako mwenyewe au kwa kuwa mtumishi au rafiki wa mtu mwenye nguvu hiyo.

Kwa watu wengi, ilikuwa kuishi kwa taabu sana. Mchumi Deirdre McCloskey anapiga hesabu kuwa, mwaka 1800, kipato cha raia wa kawaida duniani kilikuwa kati ya dola 1 hadi 5 kwa siku – vigumu hata kutosha kikombe cha kahawa katika majiji makubwa ya dunia leo hii.[2] Sasa, wastani w kipato ni karibu dola 50 kwa siku. Huu ni ukuaji mkubwa wa ustawi.

Hata hivyo, hiyo ni wastani tu ambao unaficha ustawi ambao badhi ya nchi – japo siyo nyingine – zimefanikiwa. Wastani wa kipato nchini Tajikistan, moja ya nchi zisizo huru zaidi duniani, unasalia kuwa zaidi kidogo tu ya dola 7 kwa siku. Lakini wastani wa kipato nchini Marekani, moja ya nchi huru zaidi sasa ni zaidi ya dola 100 kwa siku. Shukrani kwa manufaa ya uhuru, Wamarekani leo ni matajiri mara 14 zaidi ya wale wa Tajikistan, na ni kati ya mara 20 hadi 100 zaidi ya watangulizi wao walivyokuwa miaka ya 1800. Nchini Uswisi, Australia, Canada na Uingereza – zote zimetajwa na ripoti ya uhuruwa kiuchumi (*The Economic Freedom of the World Report)* kama miongoni mwa nchi huru zaidi duniani – zikiwa na wastani wa kipato kwa mtu wa dola 90 kwa siku. Uhuru huenda sambamba na ustawi.[3]

2 Deirdre N. McCloskey, 'Liberty and dignity explain the modern world', inTom G. Palmer (ed.), The Morality of Capitalism, Students for Liberty and AtlasFoundation, Arlington, VA, 2011.

3 Fraser Institute, Economic Freedom of the World 2012 Annual Report, FraserInstitute, Vancouver, BC, 2012.

Haishangazi hivyo, watu kuhama kutoka nchi masikini, zisizo huru sana na kwenda kwenye nchi tajiri na huru zaidi. Kila mwaka, nchi masikini zaidi 20 zinashuhudia 1.12 kati ya watu 1000 wakihama kuliko kuhamia. Kinyume chake, katika nchi huru zaidi, 3.81 ya watu kati ya 100 huhamia kuliko wanaohama.[4] Na nchi huru zaidi kiuchumi katika hizo 20hushuhudia uhamiaji zaidi wa watu. Kwa wastani, nchi zilizo nusu ya chini ya kipimo cha uhuru hupoteza whamaji, wakti zile zilizo nusu ya juu huwapata wahamiaji wengi.

Kwa maneno mengine watu wanapiga kura kwa ajili ya uhuru kwa kutumia miguu yao. Na wanafanya hivyo bila kujali jitihada za nchi zisizo huru kuwazuia watu kuhama na nchi zilizo huru zaidi kuwazuia kuingia ndani mwao.

*Uhuru na ufadhili*

Siyo unyonyaji wa masikini wao wenyewe unaozifanya nchi huru kuwa tajiri. Kama ambavyo mwanafalsafa wa maadili wa Urusi, Leonid Nikonov alichunguza, wastani wa kipato cha taifa kwa kila mtu kiendacho kwa asilimia kumi ya walio masikini zaidi kwenye nchi huru zaidi na zisizo huru zaidi kilikuwa karibu na sawa (asilimia 2.58 na 2.47 mtawalia). Lakini inasalia kuwa bora zaidi kuwa masikini kwenye nchi tajiri (mbako asilimia kumi ya walio masikini zaidi wanapata dola 23 kwa siku) kuliko kuwa masikini kwenye nchi masikini (ambako asilimia kumi ya walio masikini zaidi wanavuna dola 2.50 kwa siku).[5]

4 Gabriel Openshaw, 'Free markets and social welfare', Mises Daily, 4 October2005, http://www.mises.org/daily/1915#_edn2.

5 Leonid Nikonov, 'The moral logic of equality and inequality in market society', inTom G. Palmer (ed.), The Morality of Capitalism, Students for Liberty and AtlasFoundation, Arlington, VA, 2011.

Utajiri katika nchi huru, tajiri unapatikana kirahisi zaidi kwa watu. Wananchi wao masikini hawajatengwa jumla kutoka katika kujipatia utajiri – tofauti na wale walio nchi zisizo huru ambao hujikuta kuwa hawatokei kwenye familia, tabaka, rangi, dini au kundi sahihi la kisiasa. Kuna mabadiliko makubwa zaidi ya kijamii kwenye nchi huru zaidi. Mtu tajiri zaidi duniani, mwanzilishi wa Microsoft, Bill Gates, anajulikana kwa kuanzishia biashara yake ya programu za kompyuta kwenye gereji.

Sasa hivi, Gates analenga kutoa utajiri wake wote kwa ajili ya masuala mazuri. Hilo pia ni la kawaida kabisa: ufadhili binafsi ni mkubwa zaidi kwenye nchi tajiri zaidi. Utafiti wa utajiri uliofanywa na Barclays ulibaini kuwa mbili ya tano ya Wamarekani tajiri zaidi waliripoti kuwa ufadhili ni moja ya vipaumbele vitatu vya matumizi yao.[6]

Kwa mujibu wa 'Charities Aid Foundation' ya Uingereza, nchi tano za juu ambako watu wanatarajiwa zaidi kujitolea fedha na muda kwa masuala ya ufadhili wa msaada ni Australia, Ireland, Canada, New Zealand na Marekani, zote zikiwa juu kwenye viwango vya uhuru.[7] Na nchi zina utajiri mkubwa zaidi wa kutoa kuliko wananchi wan chi masikini, zisizo huru zaidi.

*Uhuru huzuia ubaguzi*

Katika nchi zisizo huru, ubaguzi umesambaa. Inaweza kuwa vigumu kupata kazi nzuri, au kupata huduma nzuri ikiwa hauko kwenye tabaka, dini, jinsia au familia sahihi. Lakini uchumi wa soko huria hubinya ubaguzi. Wazalishaji

6 Barclays Wealth, Global Giving: The Culture of Philanthropy, London, 2010.

7 Charities Aid Foundation, World Giving Index 2012, Charities Aid Foundation, West Malling, 2012.

kwenye jamii huru hawawezi kubagua wakati wakichagua yupi wafanye naye biashara au yupi wamuajiri.[8]

Waajiri kwa mfano, wanaweza kuwachukia wahamiaji, hasa ikiwa wametokea kwenye utamaduni, mbari au dini ya tofauti. Lakini wahamiaji wanaweza – na mara nyingi huitikia kwa kukubali mshahara wa chini zaidi kwa kazi hiyo hiyo. Hivyo, waajiri waobagua kwa kuajiri watu wa ndani pekee watajikuta wako katika upande wa hasara kiushindani. Malipo yao ya mishahara yatakuwa juu zaidi kuliko wale walio tayari kuajiri wahamiaji. Faida zao zitakuwa chini zaidi, au watahitajika kutoza gharama kubwa sana na kuwa hatarini kupoteza biashara zao. Hii ni mbaya kwa biashara. Haiko kwa upande mzuri kwa maslahi ya kibiashara kwa waajiri kubagua.

**Swali: Je, jamii huria siyo tu zinajali zaidi mali?**

Hapana. Uhuru wa kiuchumi huwapa watu machaguo na fursa. Huwapa watu mahitaji yao ya msingi – chakula, makazi na mavazi – kwa ubora zaidi. Na huwapa furs ambazo hazijawahi kufikirika kabla ya kuibuka biashara na masoko huria. Badala ya kuwafunga watu kwenye kazi ngumu ya kuchosha maisha yote, inawauruhusu watu kufurahia vitu wanachukulia kuwa vya kuinua, kama vile kusafiri, muziki, sanaa, utamaduni na shughuli za kijamii. Inawawezesha kumudu huduma bora zaidi ya afya na elimu.

Utajiri ni kifaa tu kinachotupa kuvipata vitu tunavyothamini hasa – siyo tu starehe ya mali, lakini pia tunavyothamini kitamaduni na kijamii. Ndiyo maana nchi tajiri na huru zaidi zina viwanja zaidi vya michezo, kumbi za sherehe, vyuo, maktaba na makumbuso nyingi zaidi.

8 Kwa maelezo mazuri ya hili, ona kitabu cha Milton Friedman na Rose Friedman, Capitalism and Freedom, University of Chicago Press, Chicago, IL, 1962.

Hata pamoja na nguvukazi ya ndani, uchumi wa soko huria huondosha ubaguzi. Kwa mfano, kunaweza kuepo upinzani wa kiutamaduni dhidi ya wanawake kwenda kazini, hivyo kufanya iwe vigumu zaidi kwao kupata kazi. Lakini waajiri wanaobagua wanawake watakuwa na watu wachache zaidi wanakoweza kuchota vipaji ukilinganisha na washindani wao wasiobagua. Mfano mwingine mzuri ni mgawanyo wa matabaka nchini India. Ukuaji wa viwanda vya teknolojia ya hali ya juu, hasa kwenye vituo kama Hyderabad umekuza sana nafasi ya ajira kwa watu wa tabaka la chini. Waajiri katika sekta hii yeny ushindani wanataka watu kwa nguvu yao ya ubongo. Hawana uwezo wakubagua kimatabaka au kwa kigezo chochote cha kiutamaduni. Kile ambacho sheria dhidi ya ubaguzi kimeshindwa kufanikisha kwa miongo kadhaa, wafanyabiashara binafsi wenye maslahi binafsi wamefanikiwa ndani ya miaka michache.

*Ubunifu wa watu huru*

Sababu mojawapo kwa nini uchumi huria zaidi uko na utajiri zaidi ni kwamba unatumia vipaji vyote vilivyopo. Kukiwa na ubaguzi kidogo zaidi kuwazuia, raia wote wa jamii huru wako huru kuweka akili na uwezo wao katika kazi. Ikiwa watabuni, wataboresha au kusambaza bidhaa ambazo zitafanya maisha yaw engine kuwa bora, watu hao watawapa thawabu kwa kununua bidhaa zao. Hivyo, jamii huru zina ubunifu zaidi na uanzishaji mambo mapya zaidi, hivyo huendelea haraka.

Uhuru wa kiuchumi huelekeza maslahi binafsi ya watu kwenye mwelekeo wa manufaa. Unachuma fedha kwa kuzalisha kile watu wengine wanataka na wako tayari kukilipia. Na unahitaji waje tena kwa zaidi, na kuwaambia rafiki zao namna ulivyo vizuri. Hiyo huwaelekeza

wazalishaji kwa wateja wao zaidi kuliko kwao wenyewe. Wengi wa wafanyabiashara wanaojulikana wanasema wamezifanya biashara zao kuwa za mafanikio kwa kutimiza matakwa na mahitaji ya wateja wao badala ya kujaribu kuchuma faida zaidi kutoka kwao.

Ukweli huu ni mbali kabisa na kikaragosi cha ‘mbwa kumla mbwa’ ya uchumi huria. Uchumi huria wa dhati ni wa mfumo wa ushirikiano zaidi, ukiweka misingi si kwenye mabavu, bali biashara ya huyari baina ya watu huru.

*Uundaji wa mitaji*

Pamoja na kuchochea ubunifu na huduma kwa wateja, uchumi huri huwa tajiri kwa kujenga mitaji ya uzalishaji. Ni rahisi zaidi kumkamata samaki kwa nyavu kuliko kwa mkono, lakini hii inamaanisha kukamata samaki wachache zaidi wakati ukitaabika kutengeneza nyavu zako. Kwa kuahirisha matumizi, unaweza kujenga mtaji wako na kufny uzalishaji wa baadaye kuwa wa ufanisi zaidi.

Huu ni msingi wa ubepari. Watu wanajenga mtaji kama vile nyumba, viwanda na mashine, na kufanya maisha kuwa rahisi na nguvukazi kuwa ya manufaa zaidi (mara nyingi huwa zenye uzalishaji sana, badala ya majembe ya mkono). Na mchakato huo ni wa kulimbikiza: kila ongezeko na uboreshwaji wa teknolojia ya uzalishaji huongeza uzalishaji na hupunguza jitihada za kutaabika hata zaidi.

Jamii huru inaweza kulimbikiza mtaji huu wa uzalishaji na kuendelea kuongeza uzalishaji wake na ustawi wke kwa sababu tu imewapa watu uwezo wa kumiliki nyumba,

viwanda, mashine na bidhaa nyingine za kimtaji pasipo hofu ya kunyang'anywa au kuibiwa. Inawalinda watu dhidi ya uporaji, na ina kanuni za kimaadili na kisheria kuhusu umiliki mali ambazo hufanya wizi kuwa na nafasi ndogo kutokea.

Ulinzi huu wa umiliki mali, kupitia sheria na utamaduni, ni sifa muhimu ya jamii na uchumi huru. Tangiapo, wakulima wachache waatarajiwa kujibidiisha kwenye kuandaa mbegu, kupanda, kulima na kutunza mazao yao ikiwa wanajua kuwa mavuno yao yana nafasi kubwa ya kuibiwa na wahuni. Vivyo hivyo, watu wachache wanatarajiwa kufanya kazi zaidi ya wanavyotakiwa ikiwa sehemu kubwa ya kipato chao kinachukuliwa kwenye kodi. Familia hazitatunza akiba ikiwa zitadanganywa kuhusu fedha zao kwa uongezaji wa kimyakimya wa kodi. Wajasiriamali hawatarajiwi kuwekeza kwenye biashara zao ikiwa mali zao zinaweza kutaifishwa pasipo fidia. Upendeleo ambao hupindisha soko kuwanufaisha watu wachache utafanya iwe vigumu kwa mtu mwingine kuanzisha biashara mpya.

Na unyonyaji huu wa wezi au serikali unapokuwa mkubwa zaidi, ndivyo motisha ya kazi, kuweka akiba na maendeleo hushuka. Ibn Khaldun, mwanazuoni wa kiislamu wa karne ya 14 na mwanasheria, alielewa hilo vyema sana. Aliandika:

> Inapaswa kujulikana kuwa mashambulizi dhidi ya mali za watu huondoa motisha ya kutafuta na kupata mali. Watu hviyo huwa na mawazo kuwa kusudi na mwisho wa kutafuta mali ili zichukuliwe kutoka kwao. Pale motisha ya kutafuta

> na kupata mali inapoondoka, watu huacha kufanya juhudi ya kutafuta. Kiasi ambacho haki za mali hukandamizwa kinabainisha kiwango ambacho juhudi za watu kutafuta mali kunadhoofu.[9]

*Mali na maendeleo*

Lakini kuwa na uhakika juu ya umiliki wako wa mali hukupa uhakika wa kesho yako nay a familia yako. Kwa mfano, ikiwa unaweza kumiliki nyumba yako – kitu ambacho watu wan chi nyingi hawawezi – kwa namna fulani unakuwa na hakikisho la namna unaendesha maisha yako. Pia una mali ambayo inaweza kutumika kukopa ili kuanzisha biashara na unaweza kujenga mtaji wako mwenyewe wa uzalishaji, badala ya kutegemea huruma ya matajiri wachache milele. Inakupa mto wa kifedha ambao unakuruhusu kujaribu vitu vipya – tuseme kuacha ajira yako na kutafuta nyingine, au kudhamini mpango wako mpya wa biashara.

Uhakika wa umiliki mali huchochea ubobeaji kwenye biashara, ambayo huongeza uzalishaji wa watu na kuwaongezea ustawi. Maisha yetu yangekuwa ya kimasikini sana ikiwa tungelazimika kufanya kila kitu wenyewe – kuzalisha chakula chetu, kuchota maji, kutafuta nishati, kutengeneza nguo zetu, kujenga nyumba zetu, au kijulinda dhidi ya mashambulizi. Wachache wetu wana ujuzi wa kufanya mambo yote haya, na tunahitaji vifaa sahihi kabisa kufanya haya yote kwa urahisi na ufanisi. Lakini ikiwa umiliki mali wa watu ukiheshimiwa, hatuna haja ya kufanya kila kitu sisi wenyewe. Watu wanaweza kutengeneza vifaa maalumu wanavyohitaji kufanyia kazi

9 Ibn Khaldun, Muqaddimah: An Introduction to History, 1377.

moja kwa ufanisi sana, na kuviuza vifaa hivyo kwetu wengine. Mkulima anaweza kuwekeza kwenye plau na matrekta, mwashi kwenye ngazi na chepe, mtengeneza mavazi kwenye vitambaa na cherehani. Na wanaweza wakawa wajuzi sana kwenye taaluma yao na mameneja wazuri wa uzalishaji wao kuliko wale wajinga wanaotaka kujitegemea kwa kila kitu wanavyoweza kutumainia kuwa. Kupitia mgawanyo huu wa kazi, sote tunafurahia bidhaa zenye ubora zaidi, gharama za chini zaidi na maisha mazuri zaidi.

Lakini tena, hili linawezekana ikiwa tu watu wana uhakika wa kutosha kujenga mitaji yao ya uzalishaji na kujihusisha kwenye biashara, wakiwa na hakika kuwa hawatanyang'anywa au kulaghaiwa. Mbadala wake ni mkosi. Kam ambavyo Ibn Khaldun aliendelea kusema: 'Watu wanapoacha kuwa kwenye biashara kwa ajili ya kutafuta maisha, na wanapoacha kufanya shughuli zote manufaa, ustaarabu wa biashara huporomoka, na kila kitu huoza. Watu husambaa kila kona wakitafuta kujikimu, maeneo nje kabisa na mamlaka ya serikali yao ya sasa'. Hilo ni jambo ambalo ni dhahiri sana leo tukitazama uhamaji kutoka nchi ambazo haziko huru sana kwenda nchi zilizo huru zaidi.

*Kutengeneza utajiri pasipo kumgharimu mtu mwingine*

Baadhi ya watu wanadhani kuwa mali za mtu mmoja zinakuja tu kwa gharama ya mtu mwingine. Hiyo siyo hivyo. Uchumi huria kutengeneza mali na huongeza thamani ya mali zilizopo.

Thamani siyo ubora unaoonekana wa vitu. Ni namna watu wanafikiria kuhusu vitu. Wauzaji wanaachana na vitu

kwa kuwa hawavithamini kama fedha kutoka kwa mteja wao. Wateja huachana na fedha kwa kuwa wanathamini bidhaa wanazonunua kuliko fedha wanayolipia. Hata watoto wa shule hubadilishana vifaaa vya kuchezea kwa kuwa kila mmoja hudai hufaidika kwa kubadilishana kitu walichokichoka kwa kitu wanachokitaka. Ubadilishanaji wao umetengeneza thamani. Hakuna aliyeachwa vibaya kwa mbadilishano huo: na hakuna upande ungekubali hivyo ikiwa ungedhani unapoteza katika hilo.

Vivyo hivyo, ikiwa mtu fulani anapanda mbegu na kukuza mazao ambayo hayakuwepo kabla na watu wengine wako tayari kuyalipia, wanatengeneza thamani mpya kutoka kwenye kitu ambacho awali hakikuwa na maana. Utajiri umetengenezwa na hakuna aliyeporwa.

Na tena, ikiwa mjasiriamali atajenga kiwanda kutengeneza viatu au nguo au magari au kitu kipya ambacho watu wako tayari kununua – na akatengeneza pesa katika mchakato huo – nani ameporwa? Wanaweza kuwa wamelimbikiza utajiri, lakini hawajaiba kitu kwa mtu yeyote. Kinyume chake, wametenegeneza na kusambaza thamani ambapo haikuwepo awali.[10]

*Jamii huria na siyo ubepari wa kidanganyifu*

Baadhi ya watu hudai kuwa kwenye ubepari, maslahi ya makampuni tajiri huwanyonya masikini na wanasiasa huiba utajiri kutoka kwa watu kwa kuwapa ukiritimba, upendeleo, idhini na ruzuku kwa marafiki zao wa kibiashara.

---

10 Hii imeongolewa vizuri zaidi na mfanyabiashara wa Uingereza, Sir Ernest Benn kwenyekitabu 'Why FreedomWorks', Sir Ernest Benn Ltd, London, 1964.

Lakini katika jamii huru hasa, ushindani hufanya unyonyaji na 'ubepari wa kidanganyifu' kutowezekana. Biashara hutegemea wateja ili iendelee kuwepo. Ikiwa hazihudumii vizuri, wateja hao wataziacha na kufuata wahudumiaji wengine. Na kutakuwa na msambazaji mwingine tu kwa kuwa katika jamii huru serikali hazina nguvu ya kutengeneza ukiritimba, kulinda makampuni fulani au kuwazuia watu kuanzisha baishara mpya. Uchumi huru wa dhati huzalisha ushindani, ambao huwawezesha watumiaji zaidi ya wazalishaji: makampuni yatafilisika ikiwa hayazalishi bidhaa zenye thamani ya pesa ya watumiaji ambazo wanazotaka. Baadhi ya makampuni yanaweza kuwa makubwa mno – kwa mfano sekta kama uzlishaji magari, ambayo huhitaji uwekezaji wa mtaji mkubwa. Lakini bado yanakabiliana na ushindani uliopo na unaotarajiwa kutoka kwa wawekezaji wengine wakubwa wanaodhani wanaweza kufanya vema zaidi. Matatizo huanza tu pale mamlaka zinapotibua ushindani na kunyong'nyeza au kuzuia washindani wapya kuingia.

Ni dhahiri, ushindani wa dhati na wazi ni vigumu kuudumisha. Hata katika nchi huru zaidi z dunia ya leo, wanasiasa wanaweka kanuni na utaratibu ambao – mara nyingi kwa kukusudia – hupunguza ushindani na hivyo kupunguza nguvu waliyonayo walaji juu ya wazalishaji. Na wazalishaji pia mara nyingi hufanya hila kwa hili kutokea. Kwa mfano, makampuni yaliyojichimbia mizizi yanaweza kushinikiza wanasiasa kuleta utaratibu fulani juu ya ubora wa biadhaa na viwango vya uzalishaji, ikielezea kitu gani kizalishwe vipi. Wanaweza kudai kuwa kanuni hizi zinahitajika kuulinda umma dhidi ya bidhaa hafifu. Lakini matokeo halisi ni kulinda bidhaa zao dhidi ya wasambazaji wapya au wadogo ambao wanaweza kuzalisha bidhaa mpya kwa njia za ubunifu ambao haujaainishwa kwenye kanuni. Au tena, wanasiasa wanaweza kuingilia kwa kutumia fedha

ya umma kuvisaidia viwanda vinavyoelekea kufilisika au vinavyotishiwa na ushindani kutoka nje, kwa maelezo kuwa ajira za ndani zinapaswa kulindwa. Wanaweza hata kuzuia bidhaa kutoka nje kwa ajili ya kulinda viwanda vya ndani. Hicho kinaweza kuleta nafuu ya muda mfupi kwa wale wafanyao kazi kwenye viwanda hivyo – lakini kwa kuwagharimu walipakodi na umma, ambao wana sauti ndogo na wanakabiliwa na ulipaji mkubwa kuliko inavyostahili, tena kwa bidhaa zenye ubora hafifu.

Kwa kadri jamii inapoenda mbali na uhuru na kuwapa nguvu ya kiuchumi wenye mamlaka, ndivyo kunakuwa na nafasi zaidi kwa wazalishaji na wanasiasa kufanya hila kuwanyonya watu kwa manufaa yao wenyewe. Historia ya ubepari wa hila kama huo inapatikana kote, lakini tatizo ni kubwa zaidi kwenye nchi zisizo huru zaidi. Mara nyingi, huchukuliwa kirahisi tu kuwa wanaopata madaraka watayatumia kujitajirisha wao na familia na marafiki zao. Inaweza kuchukuliwa kama ishara ya udhaifu ikiwa hawatafanya hivyo.

Lakini katika jamii huria ya dhati, mamlaka haziruhusiwi kutumia nguvu yao ya kutunga sheria fedha za walipa kodi kuwapa upendeleo wa kiuchumi kwa walaghai. Kuna kanuni kali juu ya namna kutumia mamlaka na wapi fedha za umma zinapaswa kutumika. Wazalishaji hawawezi kushawishi kwa mafanikio wale waliopo madarakani kupata ruzuku na ulinzi, kwa kuwa nguvu ya kutoa upendleo huo haipo kabisa. Kinachoyapa makampuni na wanasiasa nguvu ya kuwanyonya watu wa kawaida ni ukosefu wa uhuru na wala siyo ubepari wa kiushindani.

*Ushindi wa uhuru*

Japokuwa uhuru wa kiuchumi na biashara mara chache

kuwa huru kabisa, lakini bado umesaidia kuwaibua takribani watu bilioni mbili kutoka kwenye umasikini wa kupindukia kabisa kwa miaka 30 iliyopita. Hicho ni kitu ambacho serikali zenye nguvu zilizoshikilia madaraka mengi za Urusi, China na Kusini-Mashariki mwa Asia hazijawahi kufanikiwa pamoja na takribani nusu ya karne ya kujaribu kufanya hivyo. Lakini kama ambavyo kuta na vikwazo vya kibiashara vimeanguka, nchi nyingi zaidi zimeingia kwenye mfumo wa biashara wa kimataifa, na utajiriu umesambaa. Umesambaa hasa kwa watu masikini zaidi ambazo zimepokea uhuru wa kufanya biashara kimataifa. Kunaweza kuwepo kanuni njema na yenye manufaa ulimwenguni zaidi ya uhuru?

# 3 TAASISI ZA JAMII HURIA

## Jamii bila serikali

*Uhuru na utamaduni*

Katika jamii huria, sehemu kubwa ya maisha ya watu wanaishi pasipo serikali. Hii siyo tu kwa sababu ya mzaha wa kale wa kihindi: 'Uchumi hukua usiku – wakati serikali imelala'. Badala yake, ni kwamba serikali haina jukumu kabisa katika nyingi ya shughuli ambazo ndiyo muhimu sana kwa watu.

Watu kwenye jamii huria siyo watu waliojitenga. Kinyume chake, ni watu wa kijamii. Wanatafuta ushirika na wengine, wakijaribu kuendana na wengine na kushirikiana na wengine kwa njia nyingi. Wanaweza kuwa waumini hai wa kikundi fulani cha kidini. Kwenye klabu na jumuiya wanashirikiana na wengine ambao wanafurahia vitu vinavyofanana na vya kwao, iwe kuimba, kusoma, kupika, kuvua samaki, kucheza na kutazama michezo au ukusanyaji wa vitu. Hujumuika na kuunda makundi na wengine kama wao, iwe wadodo, wakubwa, marafiki wa shule, wazazi wapya au watu wenye ulemavu kama wao. Wanaweza kuanzisha sehemu za kuwalisha wasio na makazi au hosteli kwa ajili ya wahitaji na wasio na makazi. Hii ndiyo huitwa asasi za kiraia.

Na mbali na uhuru wa kutenda na kusafiri ambao watu

hufurahia kwenye nchi zilizo huru zaidi, raia wake mara nyingi huwa na maadili, utamaduni na mila zinazofanana wanazoshikilia. Watu huru, hasa vijana, mara nyingine huweza kukosoa njia za zamani – na hiyo ndiyo hasa njia bora ya kufanya vitu vivumbuliwe na maendeleo kufanyika. Lakini uhuru siyo adui wa utamaduni. Hata wahamiaji ambao hawashiriki utamaduni fulani, angalau waheshimu utamaduni uliopo ikiwa wanataka kukubalika kwenye jamii. Wanaweza kuhitaji kujifunz lugha mpya ili waweze kupata ajira. Na wakati mwanzoni wanaweza kutoelewa tamaduni na kanuni za kimaadili za nchi walikohamia, watahitajika kufanya hivyo haraka ili wakwepe kudhalilika na waweza kustawi. Siyo kwamba watabaguliwa kabisa: kwenye jamii huru, watu hutendewa kwa usawa. Lakini hakuna yeyote kati ya wakazi – au yeyote mwingine – anahitajika kutafuta ushirika na wengine anaowaona kuwa hakubaliani nao, au ambao ambao hawaheshimu njia zao au wasioweza kuwasiliana nao ipasavyo.

Binadamu hupenda ushirika, na wanauhitaji kama njia ya kujihakikishia fursa na kuendeleza maslahi yao wenyewe. Hivyo, kuwa mtu wa ki-peke yako kunakuweka kwenye hali mbaya. Watu kwenye jamii huria wanaweza kutothamini maadili yanayolingana, lakini kwa mtazamo wa kawaida wa kibinadamu, inalipa kuwavumilia. Uhuru wa mawazo na usemi na matendo ambao watu wanao kwenye jamii huria, kwa umuhimu, hutoa heshima kwa utamaduni, maadili na desturi zilizopo.

*Nani anayehitaji serikali?*

Mtandao huu usio rasmi wa maslahi yanayofanana, ushirikiano, kuwajibika, kuaminiana na kutegemeana unayawezesha maisha yetu pakubwa. Lakini hauhitaji serikali ili kufanya kazi. Tunashirikiana na kila mmoja

wetu na kustawi kupitia uanachama wetu kwenye makundi mbalimbali, pasipo mamlaka zozote kuhusishwa.

Hata katika suala la sheria, ambalo mtu anaweza kusema bila ubishi ni kazi ya serikali, tunaamua mambo mengi baina yetu wenyewe. Mikataba katika jamii huria haijaundwa au kuwekwa na serikali lakini hutengenezwa na sehemu husika ambao ndiyo husema vigezo walivyo tayari kuvikubali kwa hiyari. Wale wanaoingia kwenye mikataba mara nyingi hukubaliana kutatua migogoro baina yao kwa njia nyingine tofauti na mahakama zinazoendeshwa na serikali, ambazo huweza kuwa taratibu zaidi, na gharama zaidi na zisizo na haki kuliko mbadala wa binafsi.

Inasaidia kuunda mahusiano ya ushirikiano wa kijamii kama hayo ikiwa idadi kubwa ya watu wanalingana. Ikiwa watu wengi wanatoka kwenye dini au mbari inayofanana, watakuwa na maadili mengi ya kufanana na wataona ni rahisi kuingia kwenye makubaliano kwa kujiamini. Hilo halikusaidiwa na tawala za kikoloni na mikutano ya makubaliano ya kimataifa baada ya vita kuu ambayo yalitengeneza tena mipaka ya asili na kuwachanganya watu wa makundi tofauti pamoja. Nchi nyingi ambavyo zimegawanyika kwa vita sasa hivi kama vile Syria, Libya, Lebanon au Iraq hazikuwepo karne iliyopita; zimeundwa na wanasiasa na siyo watu. Waingereza walifany makosa kama hayo pia Afrika na Barahindi, kuwarundika watu wa makundi tofauti ya kikabila kwenye koloni moja la kiutawala.

Haishangazi kuwa tuna nchi nyingi sana dhaifu, ambako serikali haziwezi hata kulina maisha na mali za raia wake. Haya ni mazingira magumu kujenga jamii na uchumi huria. Siyo rahisi kuunda tena utamadni wa

kiushirika pale unapotibuliwa na kunapokuwa hakuna kiunganishi cha kuheshimiana na kuaminiana ambacho kingekuwa msingi wa ushirikiano wetu. Kizuri zaidi tunachoweza kutarajia ni mkaundi tofauti kutengeneza makubaliano yatakayowawezesha kuishi pamoja, hata ikiwa hawashirikiani kikamilifu. Lakini kuishi pmoja na kushirikiana miongoni mwa watu tofauti kutaendelea kuwa rahisi ikiwa mazingira ya jamii huru yatawekwa, kukitarajiwa matokeo ya kunufaisha pande zote husika.

## Kwa nini seriali ziwe na ukomo

*Serikali zifanye nini?*

Watu wachache leo wanaamini serikali ziongoze kila sehemu ya maisha yetu. Sote tunaamini kazi ya serikali idhibitiwe kwa namna fulani. Watu wengi wanakubali kuwa tunahitaji serikali kuamua au kufanya vitu vinavyohitaji kuamuliwa au kufanywa kwa pamoja, lakini isiingilie mambo ambayotunaweza kufanya vyema wenyewe. Na wengi ya watu wanaofikiria wanahitimisha kuwa kunapaswa kuwepo vidhibiti kwa viongozi wetu ili kuwazuia kutenda zaidi ya madaraka yao.

Suala siyo ukubwa wa serikali, lakini kipi wanachokiamua na kukifanya, na namna gani inaamua na kufanya mambo hayo. Kwa kuwa jamii huria na uchumi wake vimeegemea kwenye uaminifu, wananchi wa jamii huru hutarajia tu serikali yao kuwalinda dhidi ya ufisadi na wizi. Lakini hatungependa mamlaka kuwapa watu vifungo vya maisha kwa kukwepa nauli ya basi au kuweka kamera ya upelelezi kwenye nyumba ya kila mmoja ili kuona ikiwa wanashusha nyimbo kutoka kwenye mitandao ya kijamii. Matendo ya serikali lazima yaendane na matatizo yaliyopo.

Sababu nyingine kwa nini serikali inapaswa kuwa na ukomo kwenye uwanda wake ni kwamba maamuzi yafanywayo na watu – ikiwa wauze bidhaa fulani tuseme – huwa hiyari kabisa. Lakini maamuzi ya serikali – tuseme kuwazuia watu kuuz bidhaa fulani – huhitaji matumizi ya nguvu ili kutekeleza kikamilifu. Matumizi ya nguvu ni uovu, hata ikiwa ni muhimu wakati mwingine. Wakati tunafanya maamuzi kisiasa, tunapaswa kuwianisha na manufaa wanayopata kwa kulinganisha na uovu wa kiasi cha nguvu itakayohusika. Hatupaswi kukimbilia kufuata manufaa pasipo kufikiria madhara yake.

Na maisha ya kiuchumi na kijamii yanahitaji uhuru ili kukua. Hukua kupitia mchakato wa hatua kwa hatua wa kujaribu na kusshindwa. Wabunifu wengi hujaribu mawazo kadhaa – bidhaa mpya kwa mfano, au njia mpya ya kufundishia. Mawazo yasiyofanya kazi hutupwa mara moja, lakini yale ambayo yanaimarisha maisha huigwa na wengine na kusambazwa. Lakini taasisi za kiuchumi na kijamii kudhibitiwa na serikali ni kuwanyima wavumbuzi uwanda wowote: mchakato endelevu wa kujaribu na kushindwa kasha kurekebisha hupozwa mwendo.

Zaidi ya hayo, pale serikali inapoingilia kati, mara nyingi huwa ni kwa kiwango kikubwa. Hufanya maamuzi kwa watu wote kwenye masuala kama bidhaa gani zinapaswa kuzalishwa, au mbinu gani za ufundishaji zitumike. Haikwepeki kwamba hii huchelewesha uvumbuzi na maendeleo pia. Na pale serikali inapofanya makosa – kama ambavyo haikwepeki kuwa itafanya – huwa na madhara makubwa sana.

*Kwa nini kuwepo serikali basi?*

Bado kuna sababu nzuri za kuwepo serikali kufanya baadhi ya masuala. Tunaweza kuhitaji mamlaka kuamua na kufanyia kazi baadhi ya kanuni muhimu za namna

gani tunaenenda – kuamua upande gani wa barabara tunaendesha kwa mfano, au kuhakikisha tunaheshimu mikataba yetu.

Kwa kuongezea, kunaweza kuwepo miradi kadhaa ambayo ni kwa maslahi ya kila mtu kwamba inapaswa kufanywa, lakini huenda isifanywe (au isifanywe vizuri) na mtu fulani mmoja. Haya huitwa mali za umma. Ulinzi na usalama kwa mfano: wakati kila mtu anafaidika na kuimarishwa kwa usalama, kwa nini yeyote ajitolee kuhudumia? Mfano mwingine ni uchafuzi wa hewa ambao huharibu hewa ya majiji katika nchi nyingi zinazoendelea. Kutumia nishati zisizotoa moshi, kutumia vibadilisha hewa kwenye magari, kuweka vichuja uchafu kwenye mabomba ya moshi ya viwanda kunaweza kutatua tatizo na kufanya maisha kuwa bora kwa watu wote. Lakini watu wanaweza wasijitolee kwa gharama ya kufanya hivyo, wakijua kuwa kila mtu anaweza tu kufaidi bure kujitoa kwao muhanaga, wakifurahia hewa safi kwa gharama yake. Hivyo badala yake tunaamua masuala kama hayo kisiasa, na kumlazimisha kila mmoja kupunguza uchafuzi wake, au kuwatoza kodi ili kulipia gharama za ulinzi na usalama. Hivyo tunafanikiwa kwa vitu vinavyoleta faida kwa wengi, kitu ambacho soko haliwezi kutoa.

Baadhi ya watetezi wa uhuru – tunaweza kuwaita maliberali – watadai kuwa hatuhitaji serikali kabisa. Wanadai jamii huru ziko vizuri sana katika kutafuta njia za kushirikiana na njia za kusambaza manufaa kwa kila mmoja, kwa mfano, kwa njia za kutoa ufadhili, au kwa kutafuta njia ya kiakili ya kukatisha tama wanufaika bure kwa kudhibiti manufaa kwa wale watu wanaolipia. Hawajashawishika hata kuwa tunahitaji serikali kusimamia utekelezaji wa makubaliano au kulinda maisha yetu au mali zetu dhidi ya wizi, wakisema watu au makundi binafsi wanaweza wenyewe kufanya shughuli hizo vyema kabisa.

Watetezi wengine wa jamii huria – maliberali wa kale – wanadai kuwa kiwango fulani cha maamuzi ya kisiasa na nguvu fulani ya serikali inahitajika ili kutulinda, na kusimamia utekelezaji wa makubaliano na kutoa mali za umma – japo inapaswa kuwa na ukomo kwenye shughuli hizo. Maliberali hata hivyo, bado wanahofia kuwa ikiwa utazipa serikali inchi moja watachukua maili nzima: karibu serikali zote ulimwenguni sasa hivi zimejitafutia kazi zao wenyewe – kwa gharama ya umma – na zikienda mbali zaidi ya kazi hizi kuu.

*Mtazamo juu ya uhuru binafsi na wa kiuchumi*

Kuamua kazi za serikali zifikie wapi siyo jambo rahisi la 'kushoto' dhidi ya 'kulia'. Watu hutofautiana siyo tu ikiwa maamuzi yafanywe na watu binafsi au kwa pamoja, lakini pia ikiwa yafanye kazi kwenye maamuzi yote, ya binafsi nay a kiuchumi.

**Swali: Serikali zinalazimika kutoa ulinzi?**

Hapana. Kuna baadhi ya mambo hupaswa *kuamuliwa* kwa pamoja, kama vile ikiwa waende vitani, lakini kuna mambo machache ambayo hayawezi *kutolewa* na watu binafsi. Nchi nyingi hutoa tenda za angalau baadhi ya masuala yake ya ulinzi kwa makampuni binafsi. Ambayo hutengeneza magari yake, meli, ndege na vifaa, kujenga na kutunza kambi pamoja na kuhudumia vyakula na mipangilio.

Si zamani sana tulipokuwa tumezoea kudhani ni serikali pekee inaweza kufikisha barua, kuendesha mfumo wa simu, reli, maji, gesi, umeme, kujenga barabara, hospitali na magereza au hata kufua vyuma na kutengeneza magari. Sasa hivi makampuni binafsi yanaweza kufanya vitu vyote hivi. Na kwa kuwa hukabiliana na ushindani ubora wanaopaswa kuuzalisha ni wa hali ya juu zaidi.

Tunaweza kuona mitazamo minne tofauti.

- Kundi la kwanza tunaweza kuliita wabinafsi. Wao hudai kuwa watu binafsi hupaswa kuwa huru kufanya maamuzi yao wenyewe kuhusiana na maisha yao binafsi nay a kiuchumi.

- Kinyume cha hao ni watawala wa mabavu, ambao hutetea udhibiti wa pamoja juu ya yote, mambo binafsi na ya kiuchumi.

- Kundi la tatu ni lile linalotetea uhuru binafsi kwenye masuala ya kiuchumi lakini mamlaka ya pamoja kwenye maamuzi binafsi ya watu. Hawa tunaweza kuwaita wasiobadilika. Mchanganyiko huu wa uhuru wa kiuchumi lakini udhibiti wa kijamii upo sana kwenye mataifa ya Asia

- Kundi la mwisho la wale wanaotaka udhibiti wa pamoja kwa masuala ya kiuchumi, lakini kuacha watu binafsi kuendesha kuhusu maisha yao binafsi.

Ni vigumu sana kutafuta jina zuri la kundi hili la mwisho. Nchini Marekani wangeitwa maliberali, lakini huo ni upotoshaji wa matumizi ya neno hilo. Kwenye nchi nyingine nyingi, uliberali una maana ya ule wa kale – wazo la kwamba mfumo fulani wa kanuni za serikali unahitajika, lakini maamuzi mengi ya kiuchumi na kibinafsi yaachiwe watu wenyewe. Matokeo yake, neno hilo limetekwa nyara na wanasiasa wa kimarekani wanaoamini uhuru binafsi lakini wakitaka serikali kuwa na udhibiti zaidi wa maisha ya kiuchumi.

Maelezo haya yote na neno moja siyo njia sahihi sana za kuelezea kilichopo kwenye sepkra ya mitazamo ya

kiuchumi na kijamii. kuna uwanda mpana wa mtazamo hata ndani ya kila kundi. (Wabinafsi kwa mfano, wamesambaa kuanzia maliberali amabao hudai uhuru kamili mpaka maliberali wa kale, ambao hutaka serikali yenye madaraka kidogo. Watumizi mabavu kwa upande wao wapo kuanzia madikteta ambao hutaka udhibiti wa kiujumla wa serikali, mpaka kwa waamini taifa ambao hudai nafasi fulani ndogo kwa ajili ya kufanya maamuzi ya mambo binafsi)

Hata hivyo, ni muhimu kutambua kwamba mitazamo ya kisiasa haiwezi kutosha kuelezewa kirahisi kwa spectra ya 'mrengo wa kushoto na kulia', ambayo ingejumuisha watu wenye mitazamo tofauti kabisa ya jamii. Ni muhimu kuhfikiria kwa mtazamo wa namna ya kiasi cha uhuru ambacho watu wanadhani unahitajika kwenye maeneo mawili tofauti ya maisha, eneo la *kiuchumi* na *binafsi*.

*Kwa nini chaguo binafsi?*

Kuna sababu za msingi kutaka uhuru kwenye mambo yote ya maisha ya kiuchumi na binafsi. Kwa kuanzia, watu wanajua kuhusu mahitaji yao vema zaidi kuliko serikali zilizo mbali zinavyoweza kujua. Wanajua matumaini yao, hofu zao, ndoto, matamanio, mahitaji na shauku zao. Wanajua zaidi kuhusu hali zao na za marafiki zao, familia na jumuiya wanazozipenda na wanazojaribu kuzisaidia. Wanajua vyema zaidi fursa zilizo wazi mbele yao na matatizo ambayo matendo tofauti yanaweza kusababisha. Hivyo wako katika nafasi bora zaidi kufanya maamuzi kuhusu maisha yao na baadaye yao.

Pia kuna jambo la kimaadili kwamba watu ambao maamuzi yao hufanywa kwa niaba yao siyo binadamu kamili, bali ni watumwa. Na kutokuwa na uwajibikaji binafsi juu ya

kipi kinatokea, hawawezi kujifunza kutokana mafanikio na makosa. Wanaweza kutaabika na maovu ya sera mbaya iliyotengenezwa na mamlaka, lakini hawawezi kufanya kitu kikubwa cha kuzuia hayo kutokea tena, hivyo hawaoni sababu ya kujaribu. Lakini watu wanaofurahia manufaa ya mafanikio yao, na kutaabika na gharama ya makosa yao, wana msukumo zaidi wa kujua yapi warudie na yapi wasirudie kufanya.

*Utofauti huchochea maendeleo*

Kuna faida pia kwenye utofauti. Watu walio huru kufanya maamuzi yao wenyewe wataenenda kwa namna tofauti. Wanaweza kuchagua matendo ambayo wanadhani ni sahihi kwa ajili ya masuala yao wenyewe. Wanaweza kujaribu aina tofauti ya mitindo ya maisha – 'majaribio katika kuishi', kama ambavyo mwanafalsafa wa Uingereza John Stuart Mill aliita kwenye insha yake ya mwaka 1859 '*On Liberty*'.[11] Wengine wanaweza kufanikiwa na wengine wasifanikiwe. Lakini sote tunaweza kujifunza kutoka kwao na kuendeleza mambo yetu wenyewe, tukifanya zaidi kwa kile kinachoonekana kuzalisha na kufanya kidogo kwa kile kisichozalisha.

Kwenye jamii ya kidikteta kinyume chake, kuna njia moja tu ya kufanya mambo kwa sababu maamuzi hufanywa kwa pamoja. Makosa yoyote huwa na madhara kwa watu wote. Na hata ikiwa njia rasmi ikifanikiwa, haturuhusiwi kujaribu mambo mengine ambayo yanaweza kuwa ya mafanikio zaidi. Ufanyaji maamuzi unakuwa taratibu zaidi na wa kirasimu zaidi. Maendeleo yetu kwenye ulimwengu kama huo yatakuwa taratibu na yenye maumivu.

11 John Stuart Mill, *'On liberty'*, 1859, kwenye insha za John Stuart Mill, *On Liberty and Other Essays*, Oxford University Press, Oxford, 2008.

Kwenye uchumi huria, wazalishaji hupata mrejesho endelevu kutoka kwa wateja wao. Kila muda wa kila siku watu wanachagua bidhaa wanazozipenda kuliko nyingine. Muda wote huwa wanapima bei, utegemekaji, ukubwa, umbo, rangi na vitu vingi kwa kila bidhaa wanayonunua. Mapendeleo hayo tofauti huwa yanawafikia wazalishaji mara moja, ambao huona kipi kinauzika na kipi hakiuziki. Kwa kujua washindani wanafanya hivyo hivyo, wasambazaji huenda kwa haraka kadri wawezavyo kuzalisha zaidi kile watu wanachotaka na kidogo wasichokitaka zaidi. Na watachochewa kujaribu kwa kuleta bidhaa mpya na tofauti kwa matumaini kuwa wateja watapenda zaidi.

Kinyume na hayo tena, ni uchumi ambao mamlaka zinaamua kipi kizalishwe. Haijalishi ikiwa wanadhibiti uchumi wote au sehemu yake tu kama ambavyo mara nyingi huwa: ufanyaji maamuzi kuhusu kipi kizalishwe na kwa namna gani inaweza kuwa biashara ya taratibu na goigoi. Kiwango cha juu zaidi, wateja wanaweza kupata nafasi ya kuelezea machaguo yao kila baad ya miaka michache kwenye uchaguzi. Lakini hawatakuwa wakipigia kura bidhaa au ubora binafsi: ikiwa watapata chaguo halisi basi litakuwa fungu zima la sera zinazoweza kujumuisha kila kitu kuanzia ulinzi, shule, huduma ya afya mpaka umwagiliaji, kilimo na usafirishaji maeneo ya vijijini. Mamlaka hazina kitu kama mrejesho wa papo hapo ambao wateja huwapa wazalishaji kwenye mfumo wa uchumi wa soko. Kuna msukumo mdogo kwa mamlaka kuvumbua na wateja hawapati kile hasa wanakitaka.

*Athari gandamizi za uingiliaji wa serikali*

Kuna nchi chache ulimwenguni siku hizi ambako serikali huendesha – au hujaribu kuendesha – mfumo mzima wa uzalishaji katika nchi. Zaidi ni kwamba serikali huendesha

baahi ya sekta – hasa zile zinazoonekana kuwa muhimu zaidi, kama vile afya, elimu, kilimo, au usalama – au hujaribu kuongoza uzalishaji kwa ujumla kupitia ruzuku na udhibiti bei kwenye biashara.

Hata pale serikali inapojaribu kuendesha sekta chache tu, matatizo ya ufanyaji maamuzi taratibu na kigoigoi husalia, hasa pale sekta hizo zinapokuwa zile zenye umuhimu mkubwa. Serikali inaweza kujaribu kuendesha uzalishaji wa chakula peke yake kwa mfano: lakini ikishindwa kuzalisha chakula cha kutosha kiasi cha mahitaji ya watu, matokeo yake yatakuwa msambao wa njaa kali.

Vivyo hivyo, jitihada za serikali kuongoza uzalishaji kwa ujumla hutokeza kutowiana huko huko katika ya uzalishaji na mahitaji. Kw amfano, wanasiasa huweza kujaribu kushusha bei kwa baadhi ya bidhaa na huduma – tuseme chakula, afya au riba – kwa kuweka bei ya ukomo. Lakini wazalishaji hivyo huchuma kidogo zaidi kwa kuuza vitu hivyo. Bei wanayopata haiendani na juhudi wanazotumia kwenye uzalishaji. Hivyo wanaamua kuzalisha kidogo zaidi au kuachana na sekta hiyo moja kwa moja.

Matokeo yake ni uhaba. Pale kunapowekwa bei ndogo kwa sheria, wazalishaji watazalisha kidogo zaidi, lakini walaji watataka kununua zaidi. Chakula kinaweza kuwa bei ndogo kwa mujibu wa sheria, lakini hakipo madukani; riba zinaweza kushushwa sana lakini mikopo ikawa vigumu kupatikana; huduma ya afya inaweza kuwa bure, lakini inakubidi kupanga foleni ndefu sana kuipata.

Kuna matatizo kama hayo pale serikali zinapojaribu kuongoza uzalishaji kwa kutoa ruzuku ya uzalishaji wa badhi ya huduma na bidhaa. Umoja wa Ulaya kwa mfano, kwa muda mrefu imekuwa ikiruzuku sekta yake

ya kilimo, ikidaiwa ni kwa ajili ya kuhakikisha upatikanaji wa uhakika na endelevu wa chakula, lakini kiuhalisia ni kujaribu kuwalinda wakulima wasio na ufanisi wa Ulaya dhidi ya ushindani wa kimataifa (na kujaribu kupata uungwaji mkono wa kundi hili muhimu kisiasa). Ruzuku imechangia uzalishaji uliopitiliza – ambao umepelekea ‘milima’ ya siagi isiyotakiwa na ‘maziwa’ ya mvinyo usiouzika.

Lakini kuna matoke mengine ambayo hayaonekani zaidi kama haya. Wanufaikaji wakubwa zaidi wa ruzuku za kilimo Ulaya wamekuwa wamiliki ardhi wakubwa, na siyo wakulima masikini zaii. Na rushwa imekuwa sugu, wakulima wakidai ruzuku ya chakula ambacho hawajawahi kukizalisha. Kuna stori zisizo na idadi kama hizo duniani kote, na pia kutoka kwenye historia: kwenye kitabu chake cha mwaka 1776, *Wealth of Nations,* mchumi wa Kiskochi, Adam Smith alilalamikia boti za uvuvi kuwekwa vifaa ili kuongeza ruzuku yao badala ya uvuvi wao.[12]

Kuruzuku aina yoyote ya uzalishaji huelekeza rasilimali kwenye sekta hiyo kutoka kwenye nyingine ambako juhudi na mitaji ingeweza kutumika vyema zaidi. Kwa mfano, serikali nyingi sasa hivi zinaruzuku miradi ya gharama ya umeme wa upepo na wa jua wakichukua fedha kutoka kwa biashara na watu binafsi ambao wangetafuta njia mbadala ya kuwekeza yenye unafuu zaidi. Hii ni kuchelewesha ukuaji wa kiuchumi ambao hugandamiza ustawi wa muda mrefu wa jamii.

*Maamuzi ya wachache*

Sababu nyingine ya kutaka maamuzi ya watu binafsi badala ya mamlaka ni kwamba maamuzi hufanywa na

12 Adam Smith, The Wealth of Nations, 1776, Book IV, ch. V.

wengi badala ya wachaceh wenye nguvu. Haiepukiki kwamba mamlaka zinapohitaji kufanya maamuzi kwa ajii ya kila mtu, zitahitaji kuwa na nguvu ya kutekeleza maamuzi yao. Lakini mamlaka pia zimeundwa na binadamu; na inawataka kupita kiasi, kuzuia vishawishi vya kutumia nguvu hiyo kuendeleza maslahi yao wenyewe nay ale ya familia na marafiki zao au majirani zao, ukoo au vyama vyao vya siasa. Tenda za miradi na ukiritimba hupewa washirika wao. Kiwango kikubwa cha matumizi ya umma huenda kwenye maeneo ya wanasiasa wakubwa. Ajira za serikalini, polisi na mahakama huenda kwa wale waliopendelewa badala ya kutolewa kwa vigezo na ubora.

Lakini ikiwa vichache zaidi vitaamuliwa kisiasa na zaidi na watu binafsi, kunakuwa na nafsi finyu zaidi kutokea rushwa ya aina hiyo. Serikali hujielekeza zaidi kwenye kazi yake ya msingi ya kupunguza mabavu – badala ya kujinufaisha kutoka kwenye hilo.

Mara nyingine kujinufaisha ni tata sana kuweza kuona. 'Hakuna sanaa ambayo serikali moja hujifunza haraka zaidi kutoka kwa nyingine, kama ile ya kuvuna fedha kutoka mifuko ya watu' aliandika baba wa uchumi wa kisasa, Adam Smith.[13] Kwa kukopa kwa mfano serikali huweza kutumia fedha kwenye miradi itakayowapa ushindi kwenye uchaguzi na kunufaisha waungaji mkono wake, na kupeleke gharama kwa wengine. Wanaweza hata kusogeza gharama mbele kwa kizazi kinachofuata. Ikiwa madeni yake ni makubwa mno, wanaweza kuchapisha fedha na kulipa wadai wao kwa fedha iliyoshuka thamani. Lakini wii huo, uwe wazi au wa kificho, hukatisha watu kutengeneza utajiri. Hivyo wanakuwa wanatarajiwa kwa kiasa kidogo zaidi kuanzisha biashar mpya na kujenga

13 Ibid., Kitabu cha V, Sura ya II, Sehemu ya II, Faharisi ya Makala I & II.

mtaji wa uzalishaji, na jamii nzima inawekwa taabuni.

Serikali ya jamii huria ya dhati haiwezi kuruhusiwa kukopa labda tu kwenye hali mbaya kabisa, na hata hiyo inapaswa kuwa yenye kudhibitiwa. Na wala haitakuwa na ukiritimba juu ya fedha na kuweza kuchapisha fedha zaidi pale inapohitaji zaidi. Na kodi katika jamii huria zitakuwa chini na kutozwa kwa msingi mpana – na siyo kuelemezwa kwa wapinzani wa kisiasa au walio wachaceh kama vile 'matajiri'. Kodi zitakuwa rahisi, wazi, rahisi kulipa na kutabiri uelekeo wake. Hazitakuwa zile za 'kulimwa' na mawakala wa umma au binafsi wenye maslahi ya kuongeza kiwango wanachovuna kutoka kwa walipa kodi.

*Mjadala wa kutawala kibaba*

Mtazamo wa kawaida miongoni mwa tabaka tawala ni kwamba wanahitaji kufanya maamuzi yote kwa sababu umma, kama walivyo watoto, hauwezi kufanya maamuzi yake yenyewe. Hii inajipinga yenyewe: inawashusha 'watu' ambao mamlaka ya serikali yanapaswa kutokea. Na haina maana kupendekeza kuwa watu wana busara ya pamoja ya kutosha kuchagua serikali sahihi lakini si busara ya kutosha ya kila mtu kuweza kuendesha maisha yake.

Kuna baadhi ya mambo ambayo jamii nzima ingeweza kunufaika ikiwa watu wangeenenda kwa namna bora zaidi kidogo. Lakini mengi ya masuala haya ni mambo ya kimaadili ambayo siyo kazi ya sheria kuyasimamia. Japo tunaweza kuwataka watu kimaadili kufanya mambo yanayoweza kuwasaidia wengine, serikali ya jamii huria haiwezi kuyafanya. Imepewa mamlaka tu ya kuzuia madhara kufanywa kwa wengine, na siyo kulazimisha manufaa kwa wengine. Kuna mjadala wa 'mali za umma' kwa kuwafanya watu kuchangia kwenye miradi ya pamoja

kama vile ulinzi, lakini hayo pia ni machache.

Ni kweli kuwa watu mara nyingi huonyesha kukosa kuvutiwa na masuala kama vile namna gani huduma hutolewa na serikali. Lakini hiyo mara nyingi ni kwa sababu wanajua kuwa kulalamika ni kupoteza nguvu tu, kwa kuwa hakuna kitakachobadilika. Ikiwa chochote kitabadilika kama matokeo ya watu kuhusika, basi wengi zaidi watahusika.

**Swali: Ni kweli sote tunawajibika kwa serikali?**

Hapana. Kwenye jamii huria serikali inawajibika kwetu. Sehemu nyingi serikali zilianzishwa na zinasalia madarakani kwa kutumia nguvu pekee. Hiyo siyo serikali halali. Serikali ya jamii huria huundwa na watu kama wakal wake wa kuamua na kufanya mambo yale machache ambayo yanapaswa kuamuliwa au kufanywa kwa pamoja (kama vile ulinzi) au yale ya kutoegemea upande (kama vile utoaji haki). Iko kuwahudumia wananchi – na siyo vinginevyo.

## Njia za kudhibiti serikali

*Demokrasia*

Kwenye maeneo machache ambako maamuzi ya pamoja hayakwepeki, jamii huria hutafuta maoni ya watu wote, kwa kuwa wote huguswa na matokeo yake. Kwa maneno mengine, kuna namna fulani ya demokrasia.

Inaweza isiwe kwamba watu waote wanafanya kila uamuzi – hilo litakuwa gumu mno na lenye kutumia muda mwingi sana. Kwa kawaida, jamii nzima huchagua wawakilishi ambao huamua kwa niaba yao. Wawakilishi hao siyo wajumbe tu, wakitarajiwa kuakisi maoni ya wapigakura

wao tu; huleta na maoni yao pia kwenye mchakato huo.

Demokrasia siyo sawa kama wingi. Wengi katika umma wanaweza kuamini kuwa makundi fulani ya makabila na dini ndogo wanapaswa kuchinjwa, lakini serikali ya jamii huria haiwezi kufanywa hivyo. Ipo kwa ajili ya kuzuia madhara kufanywa kwa wengine, na siyo kuyafanikisha. Mzaha wa kale unaelezea demokrasia kama mbwa mwitu wawili na kondoo wanaoamua kuhusu chakula cha jioni. Lakini katika jamii huria, kuna udhibiti wa nguvu ya walio wengi ili kuwalinda walio wachache.

Tatizo kubwa zaidi siyo namna tunavyozichagua serikali hizo, lakini namna gani tunazidhibiti. Wao ni binadamu tu, nguvu waliyonayo inaweza kuwaharibu. Ikiwa uhuru unahitajika kulindwa, kunapaswa kuwepo aina fulani ya kuwaondoa viongozi wetu, chaguzi kwenye jamii huria siyo tu kwa ajili ya kuchagua viongozi, lakini pia ni kwa ajili ya kuwaondoa.

Baadhi ya wapenda mabavu hudai chaguzi zinaleta tu udhaifu kwa kuwa serikali tofauti, pengine zenye sera tofauti kabisa huingia na kutoka. Lakini kwa kuwa nguvu ya serikali hizo hudhibitiwa kwenye jamii huru, kiwango cha kutokea udhaifu wowote wa aina hiyo hupunguzwa. Ikiwa serikali zitachukuliwa kuwa halali, nafasi ya kutokea ukosefu wa utulivu ni finyu sana, siyo kubwa zaidi kuliko ikiwa serikali zikionekana si halali. Kupitia ubavu wa silaha, serikali isiyo halali inaweza kusalia madarakani kwa kipindi kirefu; lakini mbdala wa kweli upo kwa msimu, uchaguzi wa amani, au mara chache, mapinduzi yenye umwagaji damu. Kwenye jamii huru, chaguzi ndizo hupendelewa, na hivyo kupunguza mabavu na vurugu, zikiruhusu mabadiliko na maendeleo kutokea haraka zaidi.

Mashartifulani huhitajika kutimizwa ili chaguzi zionekane halali. Kunapaswa kuwepo kwa mfano, vyama halisi vya kuchagua. Hautakuwa uchaguzi halali ikiwa kuna mgombea mmoja tu wa kupigiwa kura: kwnenye jamii huria mara zote huwa kunakuwepo na utofauti wa mawazo. Hilo pia humaanisha wagombea tofauti wanapaswa kuweza kuelezea na kutangaza maoni yao, na kuwa huru kukosoa wagombea na vyama vingine. Na watu wanapaswa kuweza kupigia kura mgombea wanayempenda pasipo hofu ya kisasi – hivyo kura zinapaswa kuwa za siri. Baadhi ya nchi huweka ukomo wa matumizi ya kampeni ili kuhakikisha wagombea matajiri hawaitumii hiyo kama fursa dhidi yaw engine. Wengi wanaweka ukomo wa muhula baina ya chaguzi, badala ya kuachia serikali iliyoko madarakani kuamua uchaguzi ufanywe lini.

*Ufanyaji maamuzi ya umma*

Serikali za nchi zisizo huru zaidi huingia madarakani kimabavu. Na nyingine husalia humo kwa kutumia nguvu, japo nyingi zimepata namna ya kujipa mwonekano wa uhalali – kwa kujifanya ndiyo walinzi pekee wa urithi wao wa kitamaduni na kidini kwa mfano. Kinyume chake, katika jamii huru, serikali zipo kwa ajili ya makusudi machache yaliyolengwa na huja kwa kibali cha umma.

Hata hivyo, serikali mara nyingi huenda mbali kuliko makusudi yake ya kuzuia madhara kutokea na kufanya mambo ya pamoja ambayo hayawezi kufanywa kibinafsi. Kwa mfano, hufanya ukiritimba wa utoaji wa huduma za umma. Japokuwa maamuzi ya aina gani za bidhaa za umma zitolewe yanaweza kufanywa kwa pamoja, lakini huwez kutolewa kwa jumla au kwa sehemu ya mawakala binafsi. Mifuko ya hisani kwa mfano, inaweza kushughulikia kuwajali masikini na wagonjwa. Na kwenye

kuzuia madhara kwa wengine – kama vile madhara ya uchafuzi – kiwango cha madhara kinachotokea kinweza kuwa vigumu kupima, na mwingilio wa serikali unaweza kutokuwa na uhalali kabisa.

Ikiwa baadhi ya maamuzi lazima yafanywe kwa pamoja, kwa kanuni gani maamuzi haya yanapaswa kufanywa? Njia bora zaidi inaweza kuwa makubaliano ya pamoja: kila mmoja anashiriki kwenye ufanyaji maamuzi, na hakuna hatua inachukuliwa isipokuwa kila mmoja amekubali. Kwa kuwa haitazamiwi watu kupigia kura maamuzi ya pamoja wanayoona yatawadhuru, kunakuwa na nafasi finyu kwa watu au kundi lolote kudhurika na maamuzi ya pamoja.

Lakini makubaliano ya watu wote ni vigumu kufikiwa. Kwa kuania, inaweza kutumia muda mrefu kwa kila mtu kusoma na kupigia kura kila pendekezo. Ndiyo maana huwa tunachagua wawakilishi badala yake. Na kufikia makubaliano yoyote inaweza kuwa vigumu, kwa kuwa yeyote tu mmoja anaweza kukwamisha mchakato. Hivyo, maamuzi ya pamoja – iwe yamefanywa kupitia uchaguzi, kura ya maoni au kura kwenye bunge – kwa ujumla yamefanywa na umma. Inaweza kuwa wingi wa kawaida wa asilimia 51 au wa kiwango kama vile theluthi mbili. Hilo hupunguza ugumu wa kufanya maamuzi, wakati huohuo ikihakikishwa kuwa maamuzi yanafanywa na kiasi kikubwa cha watu badala ya wateule wachache.[14]

---

14 Kwa muhtasari wenye taarifa zaidi kuhusu hili na masuala yaliyofuata, ona kitabu cha EamonnButler, *Public Choice – a Primer*, Institute of Economic Affairs, London, 2012.

*Maslahi binafsi ya wapigakura*

Kuna hadithi kuhusu mtawala wa Kirumi ambaye aliombwa kuwa jaji kwenye fainali za mashindano ya kuimba, alimsikia mmoja na kumpa zawadi mwingine kwa madai kuwa wa pili asingeweza kuwa vibaya. Na leo, watu wana kawaida ya kudhani kuwa kila tunapokuwa hatujaridhika na kile jamii huru na uchumi huria vinazalisha, uingiliaji kait wa serikali utaboresha mambo. Ikiwa soko litashindwa kutoa bidhaa kwa umma kama vile ulinzi au ustawi kwa mfano, serikali ivitoe badala yake. Au ikiw kiwnda kitazalisha hewa chafu, matendo ya serikali yanahitajika kumaliza hilo. Lakini hii siyo kwamba huwa hivyo.

Masoko yanaweza kweli kushindwa kufikia mahitaji yetu wakati fulani. Lakini tunapoongelea ‘kushindwa kwa soko’ tunapaswa kukumbuka kuwa kuna kushindwa kwa serikali pia. Hata katika jamii ambazo angalau ni huru, serikali siyo zenye kukosa upendeleo, zinazopimika, zisizoendeshwa kwa hisia na zinazosukumwa na umma. Maslahi binafsi yapo serikalini kuanzia ngazi ya juu mpaka chini.

Watu huona uchaguzi kama njia ya kutambua ‘maslahi ya umma’ na kuyaweka kwenye matendo. Lakini katika jamii huria, kuna mslahi mengi tofauti – na maslahi hayo hukinzana. Wapigakura ambao wanataka kodi ndogo hukinzana na wengine wanaotaka matumizi ya umma kuongezeka. Wale ambao wangenufaika kutokana na ujenzi wa barabara mpya hupingana na wale ambao nyumba zao zitabomolewa. Chaguzi huwa hazionyeshi ‘maslahi ya umma’. Huwa tu zinawianisha maslahi yanayokinzana. Maamuzi ya pamoja hufanywa kwenye msingi huu wa mgongano.

*Maslahi binafsi ya wanasiasa*

Kama ambavyo wapigakura wana maslahi yao binafsi ya kuyahudumia, na wanasiasa pia wanayo. Wengi huona ofisi ya umma kama njia ya kuwa tajiri au kuwaumiza maadui zao. Wanaweza hata kuchukuliwa kuwa wadhaifu ikiwa hawatatumia fursa ya ofisi yao namna kama hii. Na hata katika jamii huru zaidi, rushwa inaweza kuwa tatizo.

Hata ikiwa wanasiasa wanataka kweli kuhudumia umma, kwanza huhitaji kupata mamlaka. Wanahitaji kukusanya kura za kutosha ili kuchaguliwa. Lakini hii haimaanishi kuwa zinawakilisha maoni ya wengi. Wanaweza kushinda kura nyingi kwa kukubaliwa na kundi dogo, lisilowakilisha watu.

Makundi madogo yenye ushawishi mkubwa hutawala mchakato wa kisias kw sababu yana kitu fulani mahususi yanachokipata kwa kufanya sera fulani kuwepo – kama vile kupata ruzuku ya viwanda vyao.

Kwa kuwa madogo na yenye motisha kubwa, ni rahisi kuwaweka sawa na wanatarajiwa zaidi kuweka jitihada yao kwenye kampeni na ushawishi. Lakini kwa makundi makubwa zaidi, kama vile walaji na walipa kodi, ambao hawana mtazamo mahsusi, ni vigumu zaidi kuwapangilia. Na wana motisha ya chini zaidi, kwa sababu ya gharama za sera kama ruzuku kwa viwanda fulani zimegawanyika kidogo kidogo miongoni mwao wote.

*Miungano na ulipanaji fadhila*

Kutawala kwa maoni ya wachache kunaongezeka zaidi pale makundi maslahi yanapofanya makubaliano na wengine ili kuongeza nguvu yao ya kura. Muungano wa makundi kadhaa, yanayotishia kumtupa mgombea,

yana nguvu kubwa zaidi juu ya mgombea kuliko kundi mojawapo peke yake.

Kutoa fadhila huku kwa maslahi maalumu hutokea pia kwenye bunge. Wanasiasa ambao hutaka sana miradi inayofadhiliwa na pesa ya umma kwenye maeneo yao huweza kuuziana kura na wengine ambao pia wanataka miradi kwenye maeneo yao. Lakini matokeo haya ya 'nipigie kura mpango wangu nitaupigia kura wa kwako' – yajulikanayo kama ulipanaji fadhila – ni kwamba miswada mingi kama hiyo hufanikiwa na serikali inazidi kuwa kubwa kuliko atakavyo yeyote.

Na pale sheria hizi zinapotekelezwa, maslahi binafsi zaidi yanaingia kati. Maafisa ambao wamepewa kusimamia miradi hiyo watakuwa na maslahi yao wenyewe. Hadhi na malipo yao yanategemea kwa sehemu kuwa na wafanyakazo wengi, na – kwa kujua au kutokujua – wanaweza kufanya mchakato wa urasimu kuwa tata zaidi ili wahalalishe kuhitaji wafanyakazi wengi zaidi, mchakato uitwao kujenga milki. Na tena, watapokea ushawishi zaidi kutoka kwa makundi maslahi madogo kuliko kutoka kwa umma, hivyo wanaweza kuegemea zaidi kwenye maslahi maalumu, na pengine hata kuchukua rushwa kutoka kwao.

## Kuweka kanuni

Kwa ujumla, katika kuchagua serikali, kutengeneza sheria na kusimamia sheria, wachache wenye maslahi yenye nguvu zaidi huhesabika zaidi kuliko wengi walio na maslahi yaliyotawanyika. Maamuzi yanayofanywa kisiasa hayako na nguvu ya kuonyesha maoni mapana ya umma. Na sekta ya serikali ina kawaida iliyozoeleka ya

kukua kuliko vile watu wengi walitaka, kuliko vile iletavyo maana ya kile kinachohitajika kutunza jamii huria – kiasi cha kufikia kubomoa uhuru.

Jamii huria zaidi huweka kanuni kujaribu kuzuia matatizo haya. Chaguzi ni sehemu muhimu ya hilo. Lakini ni dhaifu katika kuwadhibiti wanasiasa na maafisa. Huja mara chache na mara nyingi zikitawaliwa na vyama vikubwa, hivyo kufanya mabadiliko kuwa taratibu. Vidhibiti vikubwa zaidi vinahitajika.

*Makubaliano ya kikatiba*

Njia ya kawaida ya kudhibiti mchakato wa kisiasa ni kuwa na katiba inayokubaliwa na kila mmoja, au na watu wengi sana, na ambayo huweka kanuni zinazoongoza namna uchaguzi unafanywa na maamuzi ya kisiasa yanavyofanywa. Ikiwa kila mtu anapaswa kukubali zipi ziwe ndiyo kanuni, inakuwa vigumu kwa serikali kuleta kanuni zilizobuniwa kwa manufaa yao – kwa mfano kwa kupiga marufuku wagombea wa upinzani au kwa kuweka kodi zisizo na uwiano kwa wapigakura wa upinzani.

Mchakato wa kisiasa unaweza kudhibitiwa zaidi kupitia mgawanyo wa madaraka. Badala ya mtu mmoja au taasisi moja kuwa na nguvu zote za utengenezaji sheria, wazo liwe kugawanya mamlaka miongoni mwa taasisi tofauti, ambayo kila moja inaweza kuzuia, kurekebisha au kudhibiti kile wengine wanaweza kufanya. Kwa sababu hiyo ndiyo maana wakati mwingine huitwa mfumo wa kuchunguzana na kuwianishana *(checks and balances).*

Ikiwa taasisi moja, kama vile *politburo*, au baraza la wawakilishi, lina mamlaka yote, wengi kisiasa na makundi maslahi yatajaribu kulidaka kwa maslahi yao wenyewe.

Lakini ikiwa katiba inagawanya madaraka baina ya sehemu mbili tofauti za serikali, inafanya mamlaka kuwa vigumu kudakwa na makundi maslahi. Ikiwa sehemu hizo mbili zinachaguliwa kwa namna tofauti, itakuwa ngumu hata zaidi kwa kundi maslahi hilo hilo kutawala zote. Ikiwa sehemu yoyote inaweza kukwamisha au kurekebisha maamuzi yaliyofanywa kwenye sehemu mojawapo, bado inafanya ulipanaji fadhila na unyonyaji wa walio wachache kuwa mgumu zaidi.

Kama msingi wa mfumo huu wa kutathminishana na kuwianishana, katiba nyingi za nchi zilizo huru zaidi pia huteua rais kama mwakilishi wa watu wote, ambaye (hutumainiwa) anaweza kuwa juu ya mtafutano wa kisiasa na kuzuia sheria inayowaumiza walio wachache. Msingi mwingine zaidi dhidi ya unyonyaji ni Mahakam huru. Hii ni muhimu kwa jamii huria. Majaji wanapaswa kutokuwa na upande kisiasa, na wanatakiwa kuwa na uwezo wa kupinga sheria zinazokiuka katiba na kuwanyonya walio wachache – na waweze kufanya hivyo pasipo hofu ya kisasi cha wanasiasa.

Katiba mara nyingine huweka vizuizi kwenye shughuli za serikali, kama vile bajeti zenye uwiano – zikisisitiza kuwa bajeti zake zinapaswa kusawazika katika kipindi fulani (tuseme miaka mitau hadi mitano), na kuweka ukomo wa ukopaji kwa mwka na jumla ya deni la taifa. Nyingine hata hudhibiti kiwango cha pato la taifa ambalo serikali inaweza kutumia, ili kuzuia kawaida hii ya matumizi kuongezeka. Zaidi ya hayo, kunaweza kuweka ukomo wa mihula ili kwamba wanasiasa wasisalie madarakani kwa muda mrefu na kumalizia na vitu vinavyozuia wakala za serikali kuendelea kuwepo hata baada ya uhitaji wake kuisha.

*Viwango vya wingi*

Njia zaidi ya kulinda wachache ni kupitia mfumo wa kupiga kura wa kufikia kiasi fulani cha wingi. Uhuru utakuwa hatarini sana ikiwa kwa mfano, mamlaka zilizopo madarakani zinawez kubadili kanuni za kikatiba kwa idadi ndogo tu ya wingi wa kura kaitka bunge. Hivyo jamii huria huweka vikwazo vya juu zaidi – kma vile theluthi mbili ya kura katika sehemu zote za bunge, pamoja na wingi mkubwa kwenye kura ya watu wote au kwenye majimbo. Kwenye masuala ambako ni rahisi kuwanyonya walio wachache kwa namna mbaya sana, maamuzi yanapaswa kuhitaji idadi kubwa sana ya watu.

Kwa mfano, ni rahisi kuunda kodi ambazo zinaweza kuweka mzigo mkubwa sana kwenye makundi fulani. Baadhi ya watetezi wa jamii huria hivyo hutaka kanuni za kodi – siyo kiwango gani cha kodi, bali nani analipa kodi gani – kunapaswa kuamuliwa kwa pamoja ili kwamba walio wachache walindwe, hata ikiwa walio wengi wanazidi.

*Umma ulioshikiliwa*

Kwenye uchumi wa soko, uko huru kupeleka biashara yake kwingine ikiwa unahisi mfanyabiashara anakulaghai au anakupa thamani ndogo ya fedha yako. Lakini ikiwa serikali yako inakulaghai au kukunyonya, hakuna kwingine kwa kwenda. Unaweza pengine kuhama nchi – lakini kutokana na lugha na vikwazo vingine, hii huwa siyo mbadala wa watu wengi. Hili ni kiungo cha ubabe – kinachofanya iwe muhimu kuhakikisha majukumu na matendo ya serikali na kila sehemu yake yamebainishwa vilivyo na yamewekwa mikononi mwa wale tu wanaohitajika kulinda na kukuza uhuru wa watu.

# 4 USAWA NA KUKOSEKANA USAWA

## Usawa katika Jamii huru

Watu wengi hudhania ya kwamba jamii huru zinapaswa kuwa tofauti sana. Pia huruhusu watu kuchuma na kulimbikiza mali nyingi mno. Jambo hili (linaloendesha mjadala) lazima litapelekea utofauti mkubwa sana wa kiuchumi.

Hata hivyo, hoja hii si sahihi. Kama tulivyoona, tofauti ya kipato baina ya nchi huru na zisizokuwa huru ni karibu sawa. Kama kwa chochote, basi nchi zilizo huru zaidi, kwa kiasi zinafanana zaidi.

Zaidi ya hayo, Jamii zisizo huru zina aina nyingine ya ukosekanifu wa usawa usiokuwa wa kifedha ambao Jamii nyingi huru hazina. Kila raia wa jamii huru anaweza kutamani kuongeza mali na pato lake kwa kubadili ajira kwenda kwenye inayolipa zaidi, au kujihusisha na shughuli za kibiashara zinazoweza kuwafaidisha. Jambo hili ni nadra kuwezekana kwenye jamii zisizo huru. Ajira za serikali zinaweza kupatikana tu kwa wale wanaokiunga mkono chama tawala, au kwa rafiki na washirika wa watawala. Sheria na upendeleo unaweza kuwazuia wanawake na makabila madogo au makundi fulani mengine kufanya kazi kwenye baadhi ya nafasi. Watu wa rangi fulani au tabaka fulani la kijamii wanaweza kusalia

kwenye kazi dhaifu zisizo na fursa zaidi. Wahamiaji wanaweza kuzuiwa kuanzisha na kumiliki biashara na hata kuwa akaunti ya benki.

Hata miongoni mwa wanaopata kazi, ukosefu wa usawa unaendelea kuwepo. Mjini Moscow kwa mfano, enzi za Usovieti, maduka ya GUM yaliyokuwepo *Red Square* yaliwahudumia watalii wenye pesa za kigeni na vigogo wa chama cha kikomunisti. Vigogo wa chama pekee ndiyo wangeweza kuendeshwa na magari ya kifahari ya Zil - huku magari mengine yakisimamishwa ili kuwarahisishia wao kupita – au kuburudika kwa likizo ndefu kwenye chemchemi *(spa)* za kiafya. Majumba ya starehe za mwisho wa wiki yaligawiwa na wenye mamlaka ambao walipendelea rafiki zao kwa majumba mazuri zaidi.

Huu wote ni ukosefu wa Usawa ambao hakuna namna ya kuuepuka: mara nyingi wahanga wake huwa hawana haki ya kushinikiza au kupigia kura mabadiliko ya kisheria. Kwa utofauti, wakazi wa jamii huru angalau wanaweza kupata fursa ya kuwa na kazi nzuri au kuanzisha biashara na kupata mali na kipato. Wanaweza wasifanikiwe wote, lakini hakuna anayewazuia.

## Aina za Usawa

Usawa katika jamii huru si kuwapa watu wote mali au kipato au kiwango cha maisha kinachofanana. Ni kuhakikisha watu wote wanatendewa sawa sawa.

Hii hujidhihirisha yenyewe kwa namna nne muhimu. Raia wa jamii huru wana *usawa wa kimaadili:* kila mmoja ana haki sawa ya kujichagulia mambo yake mwenyewe na kuheshimiwa na wengine. Kuna *usawa mbele ya*

*sheria:* sheria inawalinda na kuwatendea sawa, pasipo kujali rangi zao, dini, jinsia, mali au nafasi za kifamilia. Wana *usawa wa kisiasa:* wote wanaweza kupiga kura au kuogembea nafasi za umma. Pia wana *usawa wa fursa:* hakuna vikwazo vilivyotengenezwa kuzuia kufanya kazi, kusoma au namna yoyote ya kujiendeleza

*Usawa wa kimaadili*

Katika jamii huru, watu wote hutazamwa sawa katika kuthaminiwa na kuheshimiwa. Wana haki sawa za kufanya maamuzi kuhusu maisha yao, ila tu wakizingatia kutosababisha madhara kwa wengine.

Mtazamo huu umejengwa kwenye imani kuhusu asili yetu biandamu, asili ambayo sote tunayo. Sote tunataka kufanya maamuzi yetu wenyewe, bila kujali makabila yetu, dini au jinsia; sote tuataka wengine waheshimu haki yetu ya kufanya hivyo. Kanuni katika jamii huru ni "fanya kama ambavyo ungetaka ufanyiwe".

Hii haimaanishi kuwa watu wana maadili sawa katika matendo yao. Wanaovamia na kupora wengine hawatendi sawa kimaadili. Wengi hata hudharau maadili yaliyokubaliwa kijamii na ya kujamiiana.lakini bado maisha yao yanabaki kuwa na thamani. Kuvunja kwao sheria na kukosa maadili kunafungulia adhabu au karipio linalolingana na kosa lao. Lakini haiwafanyi kutendewa unyama na ukatili uliopitiliza.

*Usawa mbele ya sheria*

Sheria katika jamii huru hulinda na kuadhibu watu kwa usawa. Watenda makosa hawapendelewi na polisi, mahakama au magereza kwa sababu ya mambo

mengine ambayo hayahusiani na kosa, kama vile utajiri wao, kujuana, matabaka yao, jinsia, dini au kabila. Raia hawezi kulazimika kukamatwa au kufanyiwa ukatili kwa kuwa tu kuna mtu kwenye mamlaka asiyewapenda. Kila mmoja ana usawa kupata haki ikiwa amedhuriwa au amenyang'anywa na wengine bila kujali ni akina nani au kiasi gani washtakiwa hao wanaheshimika na jamii.

Katika nembo iliyopo juu ya majengo ya mahakama ya dunia, sanamu ya alama ya haki huonyeshwa kama mzani ukiwa umeshikiliwa mkono mmoja na mwingine ukishikilia upanga. Lakini kitu cha msingi hasa ni kwamba sanamu hiyo imefunikwa macho. Katika jamii huru, haki huwa kipofu katika kila kitu isipokuwa mambo kadhaa muhimu kwa kila kesi.

*Usawa wa kisiasa*

Aina nyingine ya usawa inayochipuka kutoka katika asili ya watu kama binadamu ni usawa wa kisiasa. Maslahi na maoni ya kila mmoja yana thamani ya kuzingatiwa. Hivyo, kila mmoja katika jamii huru ana haki ya kupiga kura kwenye chaguzi au kura za maoni, na hakuna mwenye kura zaidi ya moja. Hii huhakikisha kuwa masalahi ya kila mmoja yanazingatiwa na wagombea uongozi na wale wanaochaguliwa.

Kuna vikwazo vichache sana. Kawaida haturuhusu watoto kupiga kura, kwa kuamini kuwa hawajakomaa bado kiasi cha kuwasilisha maoni ya kuzingatiwa juu ya namna wengine wanavyopaswa kuongozwa. Vilevile, watu wenye matatizo ya akili wanaweza kuzuiwa kupiga kura, japo ulemavu wao unapaswa kushughulikiwa kwa namna tofauti ili kuepusha watawala kuwaondoa wapinzani wao kwenye kinyang'anyiro kwa kutumuia vigezo hivi.

Kuna utofauti wa mtazamo ikiwa wafungwa waruhusiwe kupiga kura au la. Katika baadhi ya nchi wafungwa magerezani wanapoteza haki yao ya kupiga kura kwa hoja kwamba mtu aliyevunja sheria hapaswi kuhusika katika uundaji wa sheria. Katika nchi nyingine, wale tu ambao wamefungwa kwa makosa makubwa ndiyo hawaruhusiwi kushiriki. Hata hivyo, katika nchi nyingine wafungwa huonekana wana haki ya kupiga kura kwa sababu ya asili ya utu ambayo sote kama binadamu tunayo.

Kanuni ya usawa wa kisiasa inamaanisha kuwa wanawake wana haki ya kupiga kura kama walivyo wanaume, japokuwa hata katika jamii ambazo ni kwa kiasi fulani ni huru, haki hii imetambuliwa si zaidi ya karne moja iliyopita.

New Zealand ilikuwa ya kwanza kuwapa haki ya kupiga kura wanawake watu wazima mwaka 1893. Kasha Australia nayo ikafanya vivyo hivyo mwaka 1902, japo vizuizi kwa wanawake wenye asili ya kiaborijini *(Aborigine)* viliendelea hadi kufikia mwaka 1962. Nchi nyingi za Ulaya zimeanza kuruhusu wanawake kupiga kura baada tu ya Vita Kuu ya Kwanza ya Dunia, japo Ufaransa ilichelewa hata kufikia mwaka 1944 na Uswisi hadi mwaka 1971.

Vikwazo vyovyote dhidi ya haki ya kupiga kura vinapaswa kuzuiwa kabisa. Ni rahisi sana kwa mamlaka za nchi zisizozo huru kuwazuia wapinzani wao haki ya kupiga kura kwa kuwafunga gerezani au kutangaza kuwa hawana utashi wa kutosha kuongoza au kutoa visingizio vingine vingi. Hayo ni matumizi mabaya ya madaraka yao.

Kwa kadri inavyofaa, kila kura ya mtu inapaswa kuwa na uzito sawa. Kwa mfano, kunapaswa kuwa na kiwango cha wapiga kura ambacho angalau kinalingana katika kila jimbo wanakochaguliwa wawakilishi. Jimbo likiwa kubwa sana, maana yake kura ya kila mmoja inakosa zaidi

nguvu ya maamuzi. Sababu pekee ya kuwa na majimbo yanayotofautiana ukubwa ni za kijiografia ambazo haziwezi kubadilishwa. Mipaka ya majimbo iamuliwe na vyombo huru ili asiwepo wa kuchezea mipaka kwa manufaa ya makundi yaliyopo madarakani

Pamoja na haki ya kupiga kura, kila mmoja ana haki ya kugombea na kushika mamlaka katika ofisi ya umma. Hakuna viti maalumu kwenye mabaraza ya kutunga sheria kwa ajili tu ya watu wa jinsia, rangi au dini fulani.

Mfumo wa upigaji kura unapaswa kulinda usawa huu, kuhakikisha, kwa mfano, kila mmoja anaweza kugombea pasipo hofu ya kutishwa – hasa na mamlaka za kisiasa zilizoko madarakani.
Hiyo inamaanisha wanapaswa kuwa huru kupiga kampeni na kuzungumza, kutangaza mtazamo wao na kuonyesha mapungufu ya wagombea wengine na hata mapungufu ya kisheria na katiba. Chaguzi zinapaswa kuwa ushindani wa mawazo, na hakuwezi kuwa na chaguzi huru ikiwa mawazo na uhuru wa kuzungumza unagandamizwa. Katika baadhi ya nchizisizo huru, ni kosa la jinai kuikosoa serikali; katika nchi zilizo huru, ukosoaji huo ni sehemu ya kawaida kabisa ya kila siku kwenye mjadala wa kisiasa.

*Usawa wa fursa*

Usawa wa fursa maana yake watu hawapaswi kukumbana na vikwazo vya makusudi katika kuyafikia malengo yao, katika elimu, kazi au sehemu yoyote ile ya maisha. Rangi zao zisiwanyime nafasi katika shule au timu ya michezo, kwa mfano. Mfungamano wa kisiasa au jinsia yao isiwanyime nafasi ya kazi. Wala umasikini wao au tabaka lao kijamii lisiwazuie kuoa mtu wa mazingira tofauti na ya kwao.

Hii hata hivyo haimaanishi kuwa shule au waajiri wanalazimika kumchukua yoyote yule bila kujali ubora wa sifa zao. Shule zinaweza kuruhusu kudahili wale tu wanafaulu mitihani, na mwajiri anaweza kuhitaji udhamini na uzoefu wa kazi. Mwanamke huru halazimiki kuolewa na mwanaume kisa tu, mwanaume huyo amempenda. Usawa wa fursa maana yake ni kwambahakuna vikwazo visivyo vya lazima vinavyowekwa mbele ya mtu, na kwamba hakuna anayelazimishwa kufanya asichotaka kufanya. Kwa mfano, ndoa za kupangwa ni kawaida sana kwenye baadhi ya tamaduni na zinakubalika kabisa hata kwenye jamiii huru ikiwa tu wahusika wenyewe wamekubaliana. Hata hivyo watu hawawezi kulazimishwa kuoana kinyume na mapenzi yao, hata ikiwa wazazi wao watataka hivyo. Katika jamii huru, mtu mwenye umri wa kutosha kuoa anatazamwa kuwa mkomavu kiasi cha kuweza kujichagulia mwenyewe. Kama ilivyo kwa mikataba mingine, ndoa si halali ikiwa yeyote amelazimishwa kuingia

Japokuwa watu hawapaswi kukumbana na vikwazo vyovyote vya kijamii katika maamuzi yao ya maisha, bado kuna mambo ya asili yanayokosesha usawa. Mtu aliyezaliwa akiwa hasikii haitegemewi akaweza kuja kuwa mtunzi au mwimbaji wa okestra (japo baadaye Beethoven aliweza). ni vigumu mtu asiyekuwa na miguu kutamani kuja kupanda milima. Na watoto hupata mwanzo tofauti kulingana na hali za familia zao: wazazi wa mmoja wanaweza kumnunulia vitabu na kumsaidia kazi za shule, wakati wazazi wa mwingine wanaweza kuwapuuza.

Swali: Watu masikini hawako huru kununua magari ya kifahari, ndiyo?

Ni kweli. Katika jamii huru kila mmoja yuko huru kununua vitu vya kifahari, hata japokuwa ni wachache tu wanaweza kumudu. Ni suala la uwezo, na siyo uhru, watu masikini zaidi wanakosa uwezo wa kununua magari ya kifahari; lakini hakuna mtu au mamlaka inayowazuia. Yeyote anaweza kutaka kununua vitu vya kifahari, kwa kufanya kazi kwa bidii ili kupata fedha, kwa kuweka akiba au hata kwa kuazima. Kumbuka pia kuwa hata familia masikini zaidi kwenye nchi tajiri zaidi na huru zaidi duniani wanafurahia vitu kama vile mfumo wa kupasha joto nyumani, mwangaza, nishati na maji ya bomba vitu ambavyo miongo michache iliyopita vilikuwa ni mambo ya kifahari. Kinyume chake,k atika jamii zisizo huru, watu hawawezi kutamani kuwa na vitu kama nyumba kubwa zaidi au shamba lenye rutuba zaidi isipokuwa mamlaka zimewapa vitu hivyo.

Baadhi ya watu wa Magharibi wanasema kuwa, japokuwa watoto wanapata mwanzo tofauti katika maisha, shule zilenge kuwafikisha sehemu moja wakati wanafikia utu uzima na kuingia kwenye mfumo wa kazi. Pia, shule ziwekeze rasimali nyingi kwenye elimu ya kuwasaidia wasiojiweza na kuwasawazisha wenye akili zaidi badala ya kuwasukuma hadi wafikie kiwango chao cha juu kabisa cha uwezo. Hata hivyo, kiuhalisia hatuwezi kufidia kwa tofauti za kiasili – na njia pekee ya kufidia tofauti za kijamii itakuwa jinamizi la serikali kuchukua watoto kutoka kwa wazazi wao wakati wa kuzaliwa na kuwelea kwa namna inayofanana.

*Ubaguzi chanya*

Baadhi ya nchi zimejaribu kufidia tofauti za kiasili, kuvunja ubaguzi kwa kutumia programu za ubaguzi chanya. Njia

hii inahusisha tu kuwafikia walio wa makundi madogo ya kijamii ambao hawangeweza kuwaza kuwa baadhi ya fursa ziko mikononi mwao – watoto wenye akili ila masikini, kwa mfano, ambao wasingewaza kuomba udahili kwenye vyuo bora zaidi – na kuwatia moyo wajaribu. Mbinu hii ya kuwafikia na kuwatia moyo haipingiki kwa sababu kilichofanyika ni kuwaongezea wigo wa machaguo watu hawa.

Lakini pia ubaguzi chanya unaweza kuchukua sura ya kutoa upendeleo kwa watu wa makundi madogo, kama vile kuweka idadi ya kufikiwa katika shule na ajira ili kuwalazimu kuchukua watu wengi zaidi la watu wa jamii ndogo. Mpaka kufikia hapo, hii inaweza kufanya kazi: inasemwa kuwa ubaguzi chanya nchini Marekani katika miaka ya 1960 na kuendelea ilitoa nafasi kwa watu weusi kuonyesha uwezo wao darasani na mahali pa kazi hivyo kuvunja ubaguzi wa watu weupe dhidi yao. Lakini ubaguzi chanya hauendani na jamii huru. Wakati unaweza kusaidia kuondoa ubaguzi na kuchochea uhuru, ubaguzi chanya hupendelea makundi fulani badala ya kuwatendea wote kwa namna sawa.

Baadhi ya watu huunga mkono kupendelea na kuweka kikomo cha chini cha idadi ya watu kutoka jamii ndogo ili kufidia hujuma walizotendewa kipindi cha nyuma. Lakini yaliyopita yamepita: ubaguzi chanya kwa kuwapendelea watu fulani leo hausahihishi madhila waliyofanyiwa watu wa jamii hizo hapo zamani. Na sera ya aina hii inaweza kuwa ya ukandamizaji kwa watu walio wengi kwani watahitaji kufikia viwango vya juu zaidi ili kuweza kupata fursa za shule na ajira zilezile wanazopata watu wa jamii ndogo. Watu kutoka jamii ndogo wanaweza kuja kuwa kama tabaka jipya linalopendelewa, na pia kunaweza kuweko mapambano ya kuipinga sera na hata jamii ndogo

kutoka kwa jamii yenye watu wengi.

*Ubaguzi hasi*

Si mara zote ubaguzi hulenga kusaidia makundi madogo. Mara nyingi ubaguzi huwa pale makundi makubwa kijamii wakijipendelea haki, marupurupu na upendeleo ambavyo havipatikani kwa makundi madogo. Malaysia na Afrika Kusini ni mifano dhahiri, lakini pia ulimwengu umesheheni visa vingi ambapo sheria inawabagua watu wa makundi madogo kwa sababu tu ya rangi zao, dini, lugha na upendeleo wa kijinsia au mitazamo ya kisiasa.

Ubaguzi huu pia hauna nafasi katika jamii huru: katika jamii huru, watu wako sawa mbele ya sheria na hakuna kundi linaloweza kujipendelea marupurupu maalumu. Mara nyingi aina hii ya ubaguzi imeachilia kuwa kitu cha moja kwa moja ambacho watu wa makundi madogo hunyanyasiwa. Wakiwa hawana haki wanazofurahia makundi makubwa, watu wa jamii ndogo hawana njia za kujiimarisha. Wanaweza kuonekana kama watu wa tabaka la chini, au hata ambao hawajafikia viwangu vya kuwa baindamu. Ubinadamu wao unapoondolewa, hakuna kiziuzi cha namna wanavyoweza kufedhuliwa na kutendewa vibaya.

## Usawa wa matokeo

Mara nyingi watu wakiongelea usawa,hawamaanishi haki ya kutendewa kutendewa kwa namna sawa chini ya kanuni za usawa wa kimaadili, usawa mbele ya sheria, usawa wa kisiasa na usawa wa fursa. Wanamaanisha katika thawabu wanazopata watu kama vile mali, kipato na ubora wa maisha. Na wengi wanahimiza kufanyaika aina fulani ya mgawanyo wa mali ili kurudisha kutoka kwa matajiri

kwenda kwa masikini ili kusawazisha thawabu hizo.

*Takwimu za utofauti wa kipato*

Watu wanaotetea usawa wa Matokeo mara nyingi huelezea kupitia kielezo cha mgawo kinachoitwa Gini, ambacho kilipewa jina kutokana na mtakwimu na mwanasosholojia Muitaliano; Corrado Gini. Hiki ni kielezo cha ukosefu wa usawa kwa vipimo kama vile vya kipato. Mgawo wa kipimo 0 maana yake hapo kuna usawa timilifu, na ikiwa 1 maana yake hapo hakuna usawa kabisa (ni kama pale ambapo mtu mmoja pekee ndiye mwenye kipato chote)

Taasisi nyingi kama vile Benki ya Dunia na Shirika la Ujasusi la Marekani zimejaribu kupima kiwango cha mgawo wa kipato (Gini) katika nchi tofauti na kuzipanga kwa safu kulingana na kukosekana kwa usawa. Safu hizo zinaonyesha kuwa nchi zilizoendelea zaidi zina mgawo wa kuanzia 0.25 mpaka 0.5 – kumaanisha zina kiwango cha juu cha usawa. Kiwango cha juu za zaidi cha kukosekana kwa usawa kinaonekana katika nchi za kiafrika, zikiongozwa na Afrika Kusini ambayo ina mgawo wa takribani 0.7

Tunapaswa kusalia na wasiwasi na vipimo kama hivyo, na hata zaidi juu ya mapendekezo kuwa nchi zenye mgawo usio sawia zaidi zilazimishwe kusawazisha. Kwanza, nchi chache tu ndizo zina takwimu za kutegemeka kuhusu vipato, hivyo kufanya kielezo cha Gini kutokuwa cha kutegemeka (ndiyo yaweza kuwa sababu ya taasisi nyingi zinazotumia kielezo hicho kuchakata takwimu, hufikia hitimisho tofauti). Pili, tofauti kubwa ya kipato inaweza kuelezea utofauti katika muelekeo wa jamii ambao ni chanya. Inaweza kuwa ukuaji wa kasi wa teknolojia mpya, ustawi katika miji ambao unakuwa haujafika bado maeneo ya vijijini. Isingeleta maana yoyote kuondoa ustawi huu

kwa kupunguza kipato cha wafanyakazi wa teknolojia ya mawasiliano wa mjini kwenda kwa wakulima wadogo wadogo vijijini. Badala yake, turahisishe watu masikini kushiriki ustawi huu kwa kuondoa vikwazo (kama vile vya kusafiri kwa uhuru) ambavyo vinawazuia kwa sasa kushiriki ustawi huo.

Tatizo jingine la takwimu ni kuwa zinalinganisha vipato ghafi, na kupuuza kodi ambazo watu hulipa na mafao ya serikali (ustawi, pensheni, huduma ya afya ya bure na mengine mengi) wanayopokea. Chukua mfano mdogo wa kipimo kutoka Uingereza, kipato ghafi asilimia 10 wa juu ni takribani mara 30 ya asilimia 10 walio chini, ambapo inaonekana ni kukosekana usawa kwa kiwango cha juu sana. Lakini, baada ya watu kuwa wamelipa kodi zao na wamepokea mafao yao ya serikali, tofauti ni takribani mara sita tu. Bado watu wanaweza kutumia takwimu ya kwanza ghafi ili kuhalalisha mgawanyo zaidi wa kipato, lakini hayo ni matumizi mabaya ya takwimu.

*Usawa wa kipato au utajiri?*

Wazo la kwamba watu wote wafurahie thawabu sawa ya uwepo wao kwenye jamii huitwa 'uswazishaji'. Lakini inaweza kuwa ngumu kupata maana halisi ya neon hilo, kwa sehemu ni kutokana na kuwa lenyewe lina mkanganyiko wake.

Wasawazishaji wanaweza wasieleweke ikiwa wanahitaji usawa wa kipato – au wa utajiri. Ikiwa wanamaanisha usawa wa kipato, wanapaswa kukubali kuwa tofauti kubwa ya utajiri bado itatokea kwa hakika. Mtu mmoja anaweza kuweka akiba na kuwekeza kipato chake kwa hekima na akaongeza mtaji na mali, wakati mwingine mwenye kipato kinachofanana anaweza kuchezea kamari

au kutumia kwa starehe. Baada ya muda mfupi tu, vipato vyao vitakuwa tofauti sana.

Vilevile, kama kazi zote zingelipa sawa, kungekuwa na uhitaji mkubwa sana wa kazi nyepesi na nzuri na ukosefu mkubwa wa watu walio tayari kufanya kazi zilizo ngumu na zisizo nzuri. Kwa nini mtu kujitaabisha kufanya kazi kwa bidii ikiwa anapata sawa na aliye mvivu?

Kuna zaidi ya kipato cha fedha katika ajira. Kuna hiki ambacho wachumi wanakiita kipato cha kisaikolojia – kuwa na wafanyakazi wenza wanaokubalika kwa mfano, au kufanya kazi katika sehemu nzuri ya nchi au sehemu bora ya jiji yenye huduma muhimu. Haya ni baadhi ya mambo yanayothaminiwa na wanaoyafurahia, lakini si vitu vinavyoweza kuwekwa kwenye usawa.

Kama kwa upande mmoja, wasawazishaji wanamaanisha kwamba utajiri unapaswa kusawazishwa, bado kunaweza kuweko tofauti kubwa za vipato, kutegemea ujuzi wa mtu na kipaji chake, na uhitaji wa waajiri. Na ikiwa baadhi ya watu waliweka akiba na kuongeza katika utajiri wao, huku wengine wakitumia na kupunguza, milki yao ya mali itapishana ndani ya muda mfupi. Hivyo, nini cha kufanya? Wilfred Pickles, mwendeshaji wa chemsha bongo maarufu ya redio huko Uingereza miaka ya 1950, *Have a Go,* alianza kwa kuwauliza washindani maswali kuwahusu wao na malengo yao. Mmoja wao akasema 'Malengo yangu ni kupata pesa zote duniani na kuzigawanya sawia kwa kila mtu.' Alipigiwa makofi kwa kusema hivyo. Lakini akaharibu pale aliposema 'nitakapomaliza gawio langu, tutarudia kufanya hivyo tena.' Katika dunia inayobadilika ni vigumu kusawazisha utajiri.

Hivyo, matokeo sawa, iwe ni ya kipato au utajiri, si ya asili wala si thabiti. Kusawazisha chochote kati ya hivyo na kuvifanya visalie sawa, itahitaji kuharibu sana uhuru na mali za watu. Itahusisha kuchukua mali kwa nguvu kutoka kwa baadhi ya watu na kuwapa wengine – na kuendelea kufanya hivyo tena na tena ili kuweka vitu karibu na sawa.

Baadhi ya utajiri ni ngumu kuuvunja vunja na kuugawanya: kiwanda tata, kinachofanya kazi na kuzalisha mali kinaweza kuvunjwa vunjwa kwa visehemu vyake kama matofali na vipuri vya mashine, lakini katika hali hiyo maana yake hakitaweza tena kuzalisha chochote. Pia hakiwezi kuuzwa ili pesa igawanywe – kwani katika ulimwengu wa usawa wa mali, hakuna atakayekuwa na rasilimali za kutosha kukinunua.

Sera hizo za kugawanya utajiri zitakuwa za kibabe na hazitakuwa na ufanisi. Zitawanyima watu matunda ya kazi yao na kuondoa motisha yote ya kufanya kazi na kutunza akiba. Zitaharibu utajiri badala tu ya kuugawanya. Na pia itahitaji nguvu kubwa sana ya kisiasa kutekeleza – nguvu ambayo haiendeani na jamii huru.

*Taratibu za ugawanyaji*

Tatizo lingine ni kuamua nani hasa anapaswa kuwa sehemu ya mchakato wa ugawanyaji. Mara nyingi wasawazishaji kwenye nchi tajiri huwalenga watu kwenye nchi zao wenyewe, au kwenye nchi nyingine zilizo katika kundi kama la kwao. Hii ni kwa sababu kushirikiana kiapto na utajiri na watu wote wa ulimwengu kutamaanisha (hata ikiwa ingewezekana) kushuka sana kwa kiwango cha maisha ya watu katika nchi tajiri. Hii si aina ya sera inayotarajiwa kukubalika kwa amani.

Wasawazishaji katika nchi masikini, wao huwa na mtazamo wa ulimwengu mzima kuhusu usawa: kushirikiana utajiri wan chi tajiri, wakitoa sababu kuwa itapelekea mabadilko makubwa sana kwa wakazi wan chi masikini. Lakini hii ni ndoto isiyofikika, kwani nchi tajiri kamwe hazitakubaliana nayo.

Wala ugawanyaji huo hautahakikishia masikini utajiri wa kudumu. Utajiri siyo mchezo wa pata-potea. Hakuna dimbwi la utajiri mahali fulani kiasi kwamba mtu anaweza kuwa tajiri ikiwa tu mwingine amefanyika masikini zaidi. Utajiri hujengwa kwa ubunifu, biashara na kujenga mtaji. Kuharibu vijenzi vya mtaji vya walionacho hakusaidii vyovyote wale wasio nacho. Sera ianyofaa zaidi ni kukabiliana na vinavyoondoa motisha, kama vile vita na wizi, ambavyo hukatisha tamaa watu katika nchi masikini kukusanya mtaji wao wenyewe.

Maswali haya kuhusu nini kitakachogawanywa, kutoka kwa nani kwenda kwa nani, yanaonyesha wazi kuwa hakuwezi kufikiwa makubaliano ya namna sera ya ugawanyaji itakavyokuwa. Wakati huo huo, ili ugawanyaji ufanye kazi, lazima kuwepo mpango kabambe, ambao kila mmoja amekubaliana nao. Kusipokuwepo makubaliano, namna pekee ya kufanikisha ugawanyaji ni matumizi ya nguvu.

Kulazimisha kufikia usawa wa mali/utajiri utaua kabisa msingi wa mtu kuhangaikia kitu bora zaidi. Kwa kuwa kila maslahi ya utajiri ambayo mtu atapata kwa ubunifu, biashara au juhdi ya kazi utachukuliwa, kwa nini basi mtu ajitaabishe kufanikiwa? Pia kutakuwa na hasara kubwa zaidi kwa binadamu zaidi ya hii. Kwa kuishupazia shingo biashara na ubunifu, usawazishaji utafunga milango ya uendelevu wa maisha ya mali kwa ulimwengu wote.

## Usawa na haki

*Maana mbili za haki*

Wengi wanaounga mkono kuwagwanywa utajiri na kipato wanatoa sababu kuwa ni haki kwamba baadhi ya watu ni matajiri kuliko wengine – na wachache wanaweza kuwa mtajiri sana kuliko walio masikini zaidi. Kukosekana haki huku kwa haki kijamii kumezungukwa na ukweli kwamba utajiri wa watu hauakisi thamani yao kwa jamii.

Hoja hii hata hivyo, inaliteka nyara neon 'haki', ambalo sote tunakubaliana kuwa ni kitu chema na tunachokitamani, na kilicho stahili ya kila mmoja wetu kama binadamu – na wanalipa maana mpya iliyo tofauti kabisa, ambayo ni ya usawa au bila upendeleo

Maana halisi ya haki ni kuhusu tunayoyatenda kuliko tunayoyatarajia kutoka kwa wengine. Ikiwa mtu amekiuka mkataba au ameiba, tunasema hajatenda haki, kwa sababu tabia hiyo imekatazwa chini ya kanuni ya kutodhuriana na chini ya taratibu zetu za kisheria na kimaadili. Kwa maneno mengine, maana hii ya haki, *(commutative justice)* inayotegemea namna tunavyoendana na kanuni, ni ya namna binadamu wanavyofanya. Inafanya kazi pale tu watu wanapofanya mambo kwa kukusudia. Ikiwa mtu ameambukizwa mafua au kupata ulemavu, ni balaa tu, na wala si ukosefu wa haki, kwani hakuna ambaye ametenda ndivyo sivyo.

Matumizi ya pili ya neno 'haki', mara nyingine huitwa 'haki ya mgawanyo' (*distributive justice)*, si kuhusu mwenendo baina ya watu, bali nimgawanyo wa mali baina yao. Hata hivyo, kwenye jamii huru, mgawanyo wa mali na kipato unaoibuka ni matokeo ya shughuli za hiyari za kiuchumi

ambapo kila mmoja anafuata taratibu za kisheria na maadili. Haiwezi kuwa si haki kwa kuwa tu kuna mtu ametenda ndivyo sivyo. Hakuna aliyepangilia Matokeo hayo, ni uhalisia tu wa maisha.

*'Thamani kwa jamii'*

Matumizi ya neno 'haki ya kijamii' yanafanya kosa kwamba jamii ni aina ya mtu anayeamua mfumo wa mali na kipato. Lakini 'jamii' haina utashi wake yenyewe: ila tu watu ndiyo wanaoweza kufanya maamuzi na kuyatendea kazi. Na watu hutofautiana sana juu ya masuala ya sera za jamii na uchumi. Sababu mojawapo kwa nini wazo ya 'haki ya kijamii' linavutia wengi ni kwa sababu linakanganya kuhusu nini hasa matokeo yanapaswa kuwa na ndiyo huelezea kutofautiana huku.

Tunapojaribu kutazama namna mgawanyo wa thawabu kufuata 'haki ya kijamii' utakavyoonekana, ugumu wa kufukia muafaka kuuhusu unaonekana dhahiri. Watu wengi wanakubali kwamba usawa timilifu wa kipato siyo lengo sahihi, kwa sababu watu watapata manufaa sawa pasipo kujali namna walivyochagua kuwa wavivu na wazuiaji. Kwa uwazi, thawabu apatayo mtu inapaswa kuzingatia juhudi au mafanikio. Mtazamo wa jumla hivyo ni kwamba, badala ya usawa timilifu, thawabu zigawiwe kwa kuzingatia thamani ya watu kwa jamii.

Lakini tena, ni nani wa kuamua kuhusu thamani ya mtu kwa jamii? Jamii si mtu, na haina viwango vyake yenyewe. Watu hawawezi kuwekeza thamani kwenye kitu ikiwa chenyewe hakina maadili/viwango vyake. Ni watu pekee ndiyo wana viwango/maadili, na maadili hayo mara nyingi ni tofauti na yenye kukinzana. Kundi moja la watu linaweza kuthamini utendaji wa mwanamasumbwi, lingine kwa

mpiga fidla, ni vigumu kusema yupi analeta thamani kubwa zaidi kwa jamii kwa sababu vinavyowaburudisha watu tofauti haviwezi kulinganishwa. Tunawezaje kuamua thamani kwa jamii ya muuguzi, mchinja nyama, mchimba makaa, hakimu, mzamiaji, mkaguzi wa kodi, mgunduzi wa dawa yenye kuokoa maisha au profesa wa hisabati?

*Mgawanyo kwa stahili*

Pendekezo lingine kutoka kwa wasawazishaji ni kuwa thawabu zigawiwe kulingana na 'stahili'. Lakini tena, hakuna njia isiyo ya upendeleo ya kuamua 'stahili' za watu tofauti na namna gani wapate. Watu tofauti wanaweza kuwa na mtazamo tofauti sana juu ya namna sifa za ubora zinavyoonekana.

Tena, kuna mambo halisia yanayohusika wakati wa kuamua kiasi gani cha stahili kinapaswa kuhusika. Je, stahili za mtu aliyewekeza miaka mingi ya mahangaiko na hakufanikiwa zitolewe wakati yule anayeleta thamani kwa mamilioni ya watu aadhibiwe kwa sababu tu ni matokeo ya ajali ya bahati? Hatutaki kuchochea mahangaiko matupu yasiyo matunda; ukuaji wa uchumi unahusu kuongeza thamani ya tunachokizalisha na kupunguza kujitoa muhanga kwetu kunakoambatana nako. Kutoa thawabu kwa watu kwa ajili ya kujitoa mhanga kwao kutachochea tu watu kujitoa mhanga na si kwa ajili ya kuhudumia wengine. Hakuna uchumi unaweza kuendeshwa kwa kanuni za aina hiyo.

Thawabu zitolewazo na soko haziakisi stahili za maadili na za mtu binafsi za wazalishaji, wala siyo muda na juhudi walizotumia kupeleka bidhaa na huduma zao sokoni. Haijalishi ikiwa bidhaa zao zilihitaji miaka ya mahangaiko au uwekezaji au matokeo yake yalikuwa tu ajali ya bahati.

Badala yake, thawabu ya soko huakisi kufurahia bidhaa na huduma ambazo watu huzitoa kwa wengine. Wateja huwalipa wazalishaji kwa bidhaa na huduma walizozalisha kwa sababu wanazithamini bidhaa hizo. Na kiuhalisia, thawabu itolewayo na soko inategemea thamani ambazo watu huziwasilisha kwa watu wengine kwenye jamii. Pia huakisi uhaba na vipaji cya wazalishaji, idadi ya wateja wanaohitaji huduma na uharaka au umuhimu ambao wanunuzi huuona katika kuwa na bidhaa husika.

*Mgawanyo kulingana na uhitaji*

Pendekezo lingine la wasawazishaji ni kwamba, rasimali zigawanywe kutokana na 'uhitaji'. Lakini tena, ni nani wa kuamua 'uhitaji' huo ni upi? Hakuna mstari wazi unaotenganisha wahitaji na wasio wahitaji. Hali za watu zinatofautiana sana; wana mali na vipato tofauti, na hivyo vinaweza kubadilika ghafla. Pia wanaishi katika nyumba nadhifu au mbaya sana, wana uwezo tofauti kimwili na kiakili, na wanafanya kazi na watu tofauti katika kazi tofauti. Manufaa haya ambayo mtu anayapata, kama vile kuwa na kazi inayokupendeza na kuwa na wafanyakazi wenza walio na urafiki ni vigumu kuyawekea takwimu.

Ikiwa watu ni wahitaji au la, hivyo, ni suala la maamuzi, na watu tofauti hutathmini mambo kwa namna tofauti. Mgawanyo kwa kigezo cha uhitaji ungefaa tu ikiwa chombo fulani cha kisiasa kingepewa mamlaka ya kuamua 'uhitaji' na kuufanyia kazi. Lakini watu kwneye jamii huru wanaweza wasikubali kutoa mamlaka kiasi hicho kwa yeyote. Itakuwa ni kutawaliwa katika kila kitu kwenye maisha ya watu. Hawatakuwa huru tena. Watakuwa watumwa kwa mamlaka hiyo.

Wala uwepo wa hitaji haupelekei ulazima kwa wengine kulitimiza. Mtu mwenye tatizo la figo anaweza kuwa na uhitaji wa figo nyingine. Lakini haifanyi kuwa lazima kwa yeyote yule mwingine kujitolea figo yake. Ndugu wa karibu wanaweza kusikia msukumo kimaadili na kifamilia wa kujitolea, au hata watu wa mbali wanaweza kusukumwa na huruma. Lakini bado inabakia kuwa chaguo lao. Tunaweza kutia moyo na kusifia vitendo kama hivyo, lakini jamii huru haiwezi kulazimisha watu kujitolea mhanga kuwasaidia wengine.

Uchumi huria hugawanya vitu, si kwa ulazima wowote, bali kwa thamani ambayo wanunuzi huambatanisha kwenye vitu na huduma tofauti ambavyo soko la uchumi linazalisha. Kama watu wanapendelea samaki wa asili kuliko wa kufugwa, kwa mfano, au viatu kuliko sandal, hivyo hicho ndicho huzalishwa. Na hugawanya rasilimali kupitia thamani amabyo watu wanaidhihirisha kupitia hisani wanazotoa kwa wengine. Maamuzi hayo yameachiwa watu binafsi: wazo la kuwa ni dola tu ndiyo inaweza kufahamu juu ya nini kinapaswa kuungwa mkono limekataliwa katika jamii huru.

## Uharibifu zaidi wa usawazishaji

Matokeo ya kiuharibifu ya mkazo wa usawazishaji kwenye wazo la 'haki ya kijamii' ni kwamba linaificha wazo na uhalisi wa haki ya kikanuni *(commutative justice)*. Kanuni za msingi zinazoifanya jamii kuwa huru – kama vile usawa mbele ya sheria – zinafifishwa na kupunguzwa thamani na neno hilo jipya. Kwa mgawanyo upya, hakuwezi kuwepo usawa katika namna watu wanavyotendewa: badala ya kuwatendea watu kwa namna sawa, tutahitajika kuchukua viwango tofauti kutoka kwa kila mchangiaji na kutoa kiwango tofauti kwa kila mpokeaji.

*Tamaa ya mali bado ipo*

Wakati haki halisi ipo ili kutatua migogoro, 'haki ya kijamii' huanzisha migogoro. Pale serikali inapojaribu tu kugawanya kipato kwa msingi wa stahili, au uhitaji, au thamni kwa jamii, itajikuta inashinikizwa na makundi tofauti yote yakitaka thawabu zao kuongezwa. Kwa kuwa hakuna njia halisi ya kuzigawanya, mgogoro huu wa kisiasa utachochoea maamuzi ya kibabe. Ubabe huo utaamua mambo ambayo hayaendani na jamii huru.

Na watu watajaribu kutafuta njia nje ya mfumo ili kujinufaisha wao na fmailia zao. Hii ndiyo iliyoshuhudiwa kwenye Jamhuri ya Kisovieti, ambako wengi wao walikuwa wakijihusisha na aina fulani ya shughuli zisizo halali ili kuboresha maisha yao. Usawa wa mali wa kulazimisha huishia tu kuwabadilisha watu ambao ni watiifu kuwa taifa la wahalifu.

*Jukumu la matajiri*

Utofauti wa kipato na utajiri pia una manufaa. Tama ya watu kupata zaidi na pengine kuwa matajiri ni motisha yenye nguvu. Inawachochea watu kutafuta kazi bora zaidi na pia kuwekeza, kuzalisha na kusambaza bidhaa zilizo bora zaidi ambazo zitaboresha maisha ya watu wengine. Watu matajiri wana jukumu muhimu kama wafanyao majaribio ya bidhaa hizi mpya.

Bidhaa nyingi mpya huingia kwenye soko kama vitu vya fahari – kabla hazijajiweka kuwa bidhaa za wengi, hutengenezwa kdigo na kwa gharama kubwa. Hivyo huletwa na kujaribiwa kwa watu wenye utajiri zaidi. Mwitikio wa watu hao ndiyo huwezesha wazalishaji kutambua kiwango cha uhitaji wa bidhaa na panapohitaji

maboresho. Inawapa nafasi kuachana na bidhaa zenye kasoro kabla hawajawekeza katika uzalishaji mkubwa zaidi an kuboresha ubora wa bidhaa kabla hazijaingia kwenye soko kubwa zaidi. Kwa namna hii, uzoefu wa matajiri ambao ni wateja wa mwanzo kabisa, unafaidisha kila mtu.

Watu wenye mali na vipato vikubwa wana umuhimu mwingine katika majukumu ya kijamii. Wana rasilimali za kujaribu utoaji wa bidhaa na huduma mpya ambavyo huongeza machaguo na hunufaisha mchakato wa uborshaji. Wanaweza kudhamini sanaa, elimu na shughuli za utafiti wanazoamini serikali inapuuzia. Na pia wana nguvu ya kifedha kutoa changamoto kwa malka dhalimu kwa kuchochea mawazo mapya ya kisiasa ambayo maafisa wa serikali wanaweza kuona yanawatishia. Haya yote ni mambo ya kuzingatia ikiwa tutataka kutunza jamii huru.

*Uharibifu wa mtaji*

Si kila mtu yuko vizuri katika kusimamia rasilimali za uzalishaji. Wale wanaojiendeleza kama wajariliamali wanapaswa kuwa: ikiwa wanataka kupata faida katika miradi yao, wanapaswa kujua usimamizi wa hatari zilizopo na kukusanya rasilimali za uzalishaji ili kuzalisha bidhaa bora na nafuu zaidi. Ila ugawanyaji utaondoa rasilimali kutoka kwa wazoefu hawa na kuzipleka kwa wengine. Hii itamaanisha upotevu wa mtaji na uzalishaji wa mtaji. Mtaji ndiyo hufanya uchumi uzalishe, ikiwa kuan uzalishaji wa chini zaidi, na rasilimali nyingi zaidi zikiwa tu zinatumika, ustawi wa muda mrefu wa jamii husika laizma utaanguka.

Kutokuwepo kwa usawa hupelekea kuimarika kwa uchumi. Mapato makubwa yaliyotengenezwa na wazalishaji

waliofanikiwa, kuwavuta watu na rasilimali mahalia ambako thamani kubwa zaidi inaweza kuvunwa, mbali na zisizozalisha sana au zenye thamani ndogo. Hivyo, watu na rasilimali vitavutwa ambako kutajenga zaidi vipato vyao vya baadaye. Ni hatua endelevu, inayobadilika na kukua. Kukosekana usawa ambako wengi wanachukia ndiko kunakovutia watu na rasilimali kwenye matumizi yenye manufaa zaidi, hivyo kuinua ustawi kila mahali. Ikiwa tutagawanya vipato kwa ajili ya usawa, tunazuia kazi ya mvuto, na tunapoteza thamani ya baadaye, uzalishaji na ukuaji ambao ungeweza kutokezwa. Kwa watu wengi ambao wanautegema uchumi unaokua, wao ndiyo wangeathirika zaidi. Tuanwezaje kuita hicho 'haki ya kijamii?'

*Kodi na ustawi*

Usawa timilifu wa mali na kipato unaweza kuwa lengo la kufikirika, lakini serikali nyingi bado zimejaribu kusogelea karibu kwa kodi za viwango vya juu kwa watu matajiri zaidi. Hata hivyo, kodi hizi zinaweza kuwa na madhara sana. Kwa kupunguza thawabu kutoka kwa biashara na juhudi, shughuli hizi muhimu hukatishwa tama – pamoja na ajira na maboresho inayoyaleta.

Mbaya zaidi, kodi hizo huwekwa kwenye akiba na mitaji. Kodi kwenye akiba huwaacha watu wakiwa na kidogo zaidi cha kuwekeza kwenye miradi ya biashara ambayo ingekuza ustawi wa jamii nzima. Kodi kwenye mitaji maana yake rasilimali kidogo zaidi zitakwenda kwenye ujengaji wa rasilimali za uzalishaji, hivyo kupunguza ustawi wa jamii yote.

Katika jamii huru, biashara na mbadilishano huwa ni hiyari. Wazalishaji hutengeneza fedha kwa kuzalisha tu

bidhaa ba huduma ambazo watu wengine wanazihitaji na wako tayari kuzilipia. Watu wanaokuwa watajiri hawamnyang'anyi mtu. Wala hawana hatia ya kutotenda kwa haki. Hatutakubali mnyang'anyi awaibie kwa msingi kuwa hilo litapunguza kukosekana kwa usawa wa mali: hivyo kwa nini turuhusu serikali zifanye hivyo?

# 5 BIASHARA HURIA

## Uchumi wa soko huria

Mfumo wa uchumi katika jamii huria ni uchumi wa soko huria. Hufanya kazi kupitia mbadilishano wa hiari wa bidhaa na huduma baina ya watu – wakati mwingine moja kwa moja lakini kawaida kupitia fedha. Watu wapo huria kuchagua Kama, vipi, lini, wapi na ambaye wanafanya kazi, wanatumia, wanawekeza, wanahifadhi na kufanya biashara. Hakuna anayelazimishwa katika hizi shughuli.

### *Kanuni za kukuza ushirikiano*

Uchumi wa soko huria si bure -kwa-wote ambapo watu wanaweza kufanya nini wanataka, bila kujali matokeo kwa wengine.Kanuni ya kutokuwa na madhara bado ipo. Na kunamfumo wa sheria, ambayo inashughulikia upatikanaji, umiliki na kubadilishana kwa mali, haki za watu juu ya kazi zao wenyewe, na utekelezaji wa mikataba. Sheria hizi hujumuisha si tu tabia ya watu binafsi, lakini vikundi kama vile ushirikiano, makampunina misaada. Jukumu la serikali ni kudumisha sheria ambazo zinalinda mali za watu na uhuria na kutekeleza mikataba yao.Jukumu hilo lina ukomo, hata hivyo. Sheria hazipo pale kuelekeza biashara, ila kuirahisisha. Wao ni kama kikapu chenye moto.Na ni muhimu kwamba nguvu ya uchumi wa soko haujalainishwa na sheria nyingi na kanuni. Lakinisheria

ya msingi ya mali, kubadilishana na mkataba unaruhusu watukushirikiana, hata hivyo hao kuchagua, kwa manufaa ya kuheshimiana, juu ya msingi wa uaminifu, kujiamini na usalama. Hiyo huhamasisha ushirikiano mkubwa wa kiuchumi na kuzidisha faida nyingi ambayo yanatokana nayo.

*Faida za kubadilishana kwa hiyari*

Ni rahisi kufikiria kwamba wauzaji tu ndio hufaidika na biashara. Baada yayote, wao kuishia na fedha zaidi kutokana na mpango huo, wakati mnunuzi huishia na vichache. Hiyo inafanya baadhi ya watu wanadhani kwamba wauzaji wana tamaa na nia yao ni faida yao wenyewe, si kwa watu wengine.

Hili ni kosa. Je, baada ya yote, nini lengo la fedha? Katikanyakati ambazo fedha zilihusisha dhahabu na fedha, angalau ilikuwa na baadhi ya matumizi kama chuma ambayo inaweza kufanywa kuwa vito na mapambo.Lakini fedha iliyotengenezwa kutokana na karatasi na madini ina matumizi machache. Jambo la muhimu ambalo unaweza kufanya ni kwa kubadilishana kwa bidhaa na huduma nyingine.

Kwa maneno mengine, fedha ni njia ya kubadilishana. Mnunuzi hubadilishana kwa bidhaa au huduma; kisha muuzajihubadilisha kwa bidhaa mbalimbali na huduma kutoka kwa mtu mwingine. Wote hufikiriakufaidika kutokana na mpango huo. Wasingekubaliana na hilo kama ingekua vinginevyo.

*Jinsi gani biashara inajenga thamani*

Hakuna mtu ambaye hubadilishana kwa thamani ya

chini, jinsi gani wote watafaidika? Sababu ni thamani kwamba,kama uzuri ,upo katika jicho la anaeona.Si ubora wa kisayansi wa vitu, kama uzito au ukubwa. Ni kile ambacho kila mtuanadhani juu ya hicho kitu. Watu waishio nchi zenye mvua huona thamani ndogo juu ya kikombe cha maji; lakini wale walio katika jangwa ili huzingatia hiyo thamani. Mtindo mpya wa nguo unaweza kuwa na lazima kwa kijana, wakati wazazi wao hufikiri ni ujinga.

Ni kwa sababu binadamu hutofautiana jinsi wanavyoiona thamani ya kitu wanayoweza kupata kutokana na kubadilishana. Mteja anaenunua kuku kutoka kwa mfanyabiashara sokoni huthamini kuku zaidi yafedha aliyotumia kubadilishana. Lakini mfanyabiashara huthamini pesa zaidi kulikokuku. Wakati mfanyabiashara anatumia fedha kununua vitu vingine - mkate, kusema – kitu hicho hicho hutokea. Mfanyabiashara huthamini mkate zaidi ya fedha ambayo mwokaji anahitaji. Wote watatu wamepata, na ndio maana walikubali kubadilishana haya.

Kiuhalisia, kadiri ya utofauti wa thamani wanaouweka juu ya kuku, fedha na mkate, ndivyo wanavyopata faida ya kubadilishana kwao. Wanachohitaji ni kukubaliana juu ya sheria ambayowatafanyia biashara - sheria ya mali, uaminifu na mkataba ambao utatengeneza mfumo wa uchumi wa soko huria. Mbali na hilo, wenzi katika kila mpango wana nia binafsi: kila mmoja hufanya kubadilishana yao kwa faida yake mwenyewe, si kwa faida ya mtu mwingine.

Hata hivyo kwa kufuata kanuni hizi, kila mtu huwafaidisha wengine bila kukusudia - kama vile kuongozwa na ‘ mkono usioonekana ‘, kama Adam Smith alivyoweka.Ingawa

motisha ni maslahi binafsi , wao kwa hiari hushirikianana kila mmoja.

Kwa njia ya fedha, kila mmoja wetu sasa anaweza kufanya biashara -na kushirikiana - sio tu na wengine katika soko sawalakini pamoja na mamilioni ya wengine katika nchi nyingine ambazo kamwe hatutazitembelea, ambaolugha hatuwezi kusema na ambao tamaduni na siasa sisi hatuwezi kuzikubali. Katika shughuli hizi za kila siku, kila upande unafaidika. Watu hushirikiana. Thamani huundwa. Binadamu wamefanywa bora zaidi. Ubinadamu hufanikiwa.

*Maskini hufaidika zaidi*

Hivyo asili na manufaa ni mfumo huu wakubadilishana bure ulioenea kila mahali. Inaweza kuwepo kwa njia haramu, au ni kulanguziliwa, katikanchi ambazo hukataa masoko huria kama suala la itikadi. Nchi nyingi (ikiwa ni pamoja kadhaa katika Asia) ambazo huwapa wananchi wao uhuriakidogo katika mambo ya kibinafsi na kijamii, hata hivyo huwapa uhuria wa kiuchumi.

Hakika, biashara ni jambo muhimu katikamiaka ya mwanzo ya ulimwengu wa Kiislamu na kuenea kwake baadaye. Ufunguzi wa njia za biashara duniani ulitengeneza utajiri mkubwa na mwamko huko Ulaya, ambayo kwa upande mwingine ilizalisha ustawi wa sanaa, utamaduni na kujifunza. Amerika ilifanikiwa kupitia muunganiko wa kibiashara na Ulaya, na kisha China.

Lakini si matajiri tu ambao huinuliwa zaidi na wimbi hili la kupanda kwa mafanikio ya binadamu. Ambapo uhuria wa kiuchumi umeenea, hali ya maisha ya maskini imeongezeka zaidi. Kama

Mchumi wa kimarekani Milton Friedman alivyosema, maji ya bomba ndani ya nyumba yalikuwa kama anasa katika falme ya Roma; lakini seneta wa Kirumi hakuwa na haja nayo kwa sababu alikuwa na watumishi wa kuleta hayo maji. Maskini wa falme ya Roma waliishi katika mazingira machafu; lakini maskiniwa Roma ya kisasa sasa wanachukua anasa ya maji moto na baridi ya bombakwa nafasi.

Athari hii inaweza kuonekana dhahiri katika ufunguzi wa biashara za kimataifa na kuenea kwa kanuni za masoko katika nchikama vile China na India. Katika miongo mitatu tu, labda watu bilioni au zaidi wamekuzwa kutoka katika umaskini uliokithiri kama matokeo. Mamilioni zaidi sasa wanaweza kutamani kuwa tabaka la kati na kufurahia anasa kama simu za viganjani, luninga na vyombo vya usafiri - na kwa kweli kufanya kazi katika maeneo ya baridi, kavu, ofisi za starehe na viwanda badala ya hali zote za hewa juu ya nchi.

## Jinsi ya kuwa tajiri

Wazalishaji wanapaswa kuwahudumia wateja

Katika jamii huria, wateja na uchaguzi. Hawalazimishwi kununuakutoka kwa wazalishaji fulani, kama vile ukiritimba unaoendeshwa na serikali.Watoaji wanaweza kujaribu kula njama kuongeza bei,lakini ni vigumu kufanya hizo njama zidumu, kwa kuwa yeyote kati yao anawezakudanganya kwa kupunguza bei zao ili kuvutia wateja zaidi. Wakati huo huo, watoa huduma wengine wapo huriakuingia katika soko na kushindanana makampuni ambayo yanajaribu kuongeza bei.

Katika ushindani wa dhati wa uchumi wa soko huria, hata hivyo,wazalishaji hawana uwezo wa kunyonya wateja wao. Isipokuwa wanazalisha kile wateja wanachotaka, na ubora wanaoutaka nakwa bei ambayo ni ya kuvutia, wapo karibuni kupoteza biashara. Watu hawajafungwa kwa nguvu za makampuni.Kinyume chake, wazalishaji wanaishi tu na kukabiliana na mabadiliko yamahitaji ya umma.

Kampuni inaweza kuwa kubwa, lakini bado inakabiliwa na ushindani.Kampuni kubwa pengine hutengeneza bidhaa nyingi tofauti na inashirikikatika biashara nyingi tofauti. Lakini si tu inakumbana na ushindani kutoka kwa makampuni mengine makubwa. Pia inakabiliwa na ushindani kutoka kwa kampuni ndogo ambazo zinaweza kushindana kwa sehemu fulani ya biashara. Makampuni madogo yenye matumizi ya kawaida wanaweza kuwa na uwezokuzalisha baadhi ya bidhaa za kampuni kubwa kwaubora zaidi au kwa bei nafuu. Makampuni mapya na ya kibunifu yanaweza kuzalisha bidhaa mpya ambazozitatoa bidhaa moja au zaidi ya kampuni kubwa ya kizamani.

Ni hadithi, kwa hiyo, huo ubepari unapelekea makampunikuwa makubwa, na hatimaye ukiritimba, kadri makampuni yanavyojiingiza kwenye uchumi mdogo. Udogo una gharama zake pia: mashirika makubwa ni vigumu sana kusimama na polepole juu ya miguu yao .Inaelekezwa kuangaliamagazeti yoyote ya Magharibi, tuseme, miaka hamsini iliyopita. Makampuni machache yaliyokua yakitangaza biashara bado yapo. Wote wamepitwa na washindani walioanza taratibu lakini walikuwa na ubunifu zaidi au gharama nafuu.

## Hakuna kushikilia nguvu ya kiuchumi

Hivyo, hakuna haja ya makampuni kushikilia nguvu ya kiuchumi, wala kwa watu ambao huendesha hizo biashara. Watu wanawezakuwa tajiri katika uchumi huria, lakini ni pale tu wanapoendelea kuutumikia umma kwa muda mrefu na kuvutia wateja. Hakika, 'kutoka kwenye mikono ya shati mpaka mikono ya shati katika vizazi vitatu' ni jambo la kawaida katika jamii zenye uhuria: watu kuanzisha makampuni na kutengeneza fedha kwa ajili ya familia zao, lakini wajukuu wao watakapokuja kwenye biashara, makampuni mengine yatakua yameanza kuwapita kiushindani.

Huu ni mfumo mzuri zaidi kuliko pale wasomi wanapodhibiti upatikanaji wanguvu za kisiasa na kiuchumi, na kuhakikisha kwamba wao nafamilia zaowameshikilia nguvu hiyo. Katika uchumi huria, mtu yeyote mwenye kipaji na malengo anaweza kutamani kujenga mali - zinazotolewa kwamba waokuwatumikia wengine. Nafasi ya kuwa tajiri haijawekwa mipaka kwa marafiki, familia au chama cha wale waliopo madarakani, wala kwa wale walio katika mbari au vikundi vya kidini. Hakika, baadhi ya watu wengi waliofaulu katika jamii huria ni wahamiaji, wanaokuja na uzoefu tofauti na mawazo na kuzalisha bidhaa mpya au huduma ambazo watu wana nia ya kununua.

Ambapo kuna serikali yenye nguvu ambayo inaweza kusimamia fadhila kwa marafiki zake, hata hivyo, wafanyabiashara hujaribu kuitumiakwa faida yao wenyewe. Wao wanaweza kutafuta kanuni ambayo inaweka nje washindani, au hata ukiritimba kamili. Ingawa wanaweza kujaribu kuhalalisha hiikwa kusema

kwamba italinda umma kutokana nabidhaa hafifu, nia yao halisi ni kuhodhi soko. Lakinihii itawapa nguvu ya udhibiti ambayo ni kinyume najamii huria. Serikali haipaswi kuwa na uwezo wa kukingama na masoko na kujenga ukiritimba; badala yake, wajibu wao wanapaswa kupanua uhuria na ushindani.

**Swali: Je, ushindani, faida na matangazo si ufujaji?**

Hapana. Faida ndiyo inayopelekea watu kufanya, kutafuta fursa na kujenga bidhaa na huduma ambazo watu wengine wana hiari kabisa ya kuchagua kununua. Faida pia inaonyeshakuwa rasilimali zinatumika kuzalisha bidhaa au huduma ambazojamii inathamini zaidi ya rasilimali ghafi zenyewe.

Matangazo ni muhimu kwa sababu huwaambia watu kuhusu bidhaa mpya na kuboresha bidhaa zilizopo. Ushindani huwapa watu uchaguzi kati ya bidhaa mbalimbali, kusukuma wauzaji kubuni na kutoa huduma bora kwa gharama ya chini .Bila ushindani, watumiaji watakuwa dhaifu. Ingewabidi wao kuchukua kile ambacho mkiritimba ameridhia kutoa – au kuacha.

## Ujasiriamali

Mafanikio katika uchumi bure si juu ya kufanya kazi kwa bidii tu– ingawa hiyo husaidia mara nyingi. Unapaswa kusambaza bidhaa na huduma ambazo watu wenginewanataka na wako tayari kununua. Hiyo inaweza kuhusisha kuchukua uthubutu -kubahatisha watu watahitaji bidhaa gani mpya - na kuandaamlolongo wa uzalishaji ambayo inaweza kuhusisha wauzaji wengine wengi, wafanyakazina wasambazaji. Kwa kulinganisha ni watu wachache walio tayari kufanya uthubutu na kuwajiibika; lakini matarajio ya uhitaji yenye mafanikio na shirika la mifumo ya uzalishaji, mitandao na juhudini

mchango halisi ya wafanyabiashara hawa. Wao huchukua tahadhari kubwa, naiwapo umma hufanya kweli kununua bidhaa zao, hulipwa vizuri.

Hiyo kwa upande mwingine huleta tija na uvumbuzi. Inapelekea watu katika kutengeneza bidhaa mpya na bora zaidi na taratibu kwa matumaini kwamba wao pia watapata utajiri ambao wajasiriamali wa zamani walipata. Na huo uboreshaji wa mara kwa mara na uvumbuzi huwafaidisha wateja na jamii nzima. Uvumbuzi ambao huwapa watu kazi au kuboreshamaisha yao, huongeza mafanikio na kueneza utajiri kuliko mpango wa ustawi wa serikali.

Wateja hufaidika na bidhaa na huduma ambazo kamwe wasingeweza kupata au kuzalisha wao wenyewe. Huchukua mpango wa utafitina utaalamu, kwa mfano, kuendeleza na kusambaza dawa madhubuti. Watu wana uwezekano wa kukosa kemikali, utaalamu wa utengenezaji na kibaiolojia zinahitajika - lakini makampuni ya kitaalamu ya madawa wanavyo.Hata wafamasia wa mitaani wanaweza kuwa na maarifa ya kitaalamuya matumizi, ufanisi na madhara ya madawa kama mia tanoau zaidi katika hisa zao. Wateja hawangeweza kupata hayomaarifa ya kitaalamu - kwa hakika labda kama wao pia walikuwa wataalamu wa vyakula, vinywaji, nguo, viatu na vitu vingine vyote wanavyohitaji katika maisha yao ya kila siku.

Wajasiriamali huweza kujilimbikizia utajiri. Lakini hawafanyi hivyo kwa gharama ya watu wengine. Fedha wanayopata huja kutokana na malipo ya hiari ya wateja wao. Wao hupata utajiritu kwa kuwasaidia wengine, na si kwa kuwatoza kodi au kuwanyonya watu. Na wanatunza mali zao kadri wanavyoendelea kutumikia umma. Kuendelea kupata kipato, wanapaswa kuelewa

wateja wao na matarajio ya mahitaji yao. Hivyo siku zote wao hutafuta bidhaa ambazo hazijakamilishwa na kuzikamilisha. Ni utaratibu wa mara kwa mara wa kujaribu kuwaridhishawateja.

## Faida na ukisiaji

Matarajio ya faida, huchochea wazalishaji - wakubwa na wadogo – kwa kuchukua tahadhari, kuvumbua, kuandaa na kufanya kazi kwa kuwatumikia watu wengine.

Wakosoaji wengi wa uchumi huria huumbua wazo la ‘ faida ‘ -lakini kwa kweli sisi sote ni watafutaji wa faida. Tunajitoa mhanga kwenye baadhi ya mambo ili kupata kitu ambacho ni cha thamani zaidi. Kwa mfano, tunatumia muda na juhudi za kufanya usafi ili kuwa na nyumba nadhifu na maridadi. Sisi tunathamini nyumba safi kuliko juhudi za kusafisha: tofauti ni faida yetu. Na si faida ya kifedha, lakini kwa njia nyingine ni tu kama mjasiriamali anaponunua vifaa nakuzalisha kitu ambacho anauza kwa gharama zaidi kuliko gharama za utengenezaji. Hata sisi tunaposhiriki katika jamii au miradi ya uhisani -kuhudumia bodi ya shule, sema - tunafanya hivyo kwa ajili ya miisho yetu wenyewe, hata kama miisho hiyo inaweza kuwa tunataka kuona watoto wetu wote wameelimika. Hiyo pia ni (isiyo ya kifedha) faida kwetu. Lakini nifaida ya kifedha tu ambayo wakosoaji wanaiona na kuichukia. Hii haina mantiki na haiendani na utaratibu.

Hiyo ni kweli pia wakati ulanguzi unapokosolewa. Katika hali halisi, ulanguzi haujawekewa mipaka katika masoko ya biashara. Sisi wote ni walanguzi. Wakulima hupanda mbegu kwa matumaini ya kuongeza soko la mazao. Tunakwenda shule na kupata sifa ambazo sisi tunatumaini zitatufanya tuajiriwe. Hii ni mipango ya kukisia.

Katika dunia ya kifedha, ulanguzi ni muhimu sana. Meli zisingeweza kusafiri kama makampuni ya bima na wafadhili hawapo tayarikubashiri na kuchukua tahadhari juu ya usalama. Uzalishaji wa kisasa hutegemea mikataba mikubwa na ya muda mrefu- Kama vile mikataba ya usambazaji, au mikataba ya kujenga na kudumishakiwanda. Wazalishaji binafsi hawawezi kuchukua tahadhari kwa ujumla. Hivyo hualika wengine kununua hisa katika biashara zao.Hiyo ni aina nyingine ya ulanguzi. Katika masoko ya hisa, walanguzi hununua na kuuza kwa matumaini ya kutengeneza faida, lakini kufanya hivyo inahitajikuwa na uelewa wa kitaalam wa makampuni wanayofanya biashara, namatarajio yao ya baadaye. Utaalamu huo huleta habari muhimu sokoni, na husaidia bei kufikia kiwango chake haraka zaidi kuliko wasingekuwa nao, na kufanya soko zima kuwa na muitikio zaidi na ufanisi.

Kutengeneza faida Ni si sawa na kuwa na tamaa .Watu hujipatia faida wenyewe kwa maslahi binafsi, lakini si sawa na tamaa. Kipimo cha maslahi binafsi ni muhimu kama sote tunataka kuishi, kuepuka kuumia na kuboresha miili yetu. Lakini tamaa ni dhana ya maadili inayoonyesha kwamba mtu ni mbinafsi kupita kiasi, kwa hasara ya wengine. Katika jamii huria, wazalishaji unaweza kukidhi maslahi yao binafsi kwa kuwasaidia wengine tu.

## *Biashara na mahusiano*

Muhimu ni kwamba biashara sio maisha yote. Hata mfanyabiashara mwenye juhudi sana katika jamii huria ana familia na mahitaji mengine kama michezo au burudani, au makundi na vyama vyenye shauku. Mmoja anahitaji tu kuangalia nchi za kibeparikama vile Italia, ambapo mahusiano ya kifamilia ni makubwa sana, kwa

kutambuakwamba familia na uchumi wa soko hukaa pamoja kwa urahisi.

Kuwa katika biashara haihalalishi kutojali wengine,na kwa hakika haihalalishi kuwaumiza wengine –hiyo inatawaliwa na sheria-isiyo na madhara. Na kati ya mahusiano yenye tija ni yale ya wafanyabiashara wenzako mahali pa kazi. Uchumi wa soko huria hukuza mahusiano ya kijamii kwa njia nyingi pia. Inawapa watu utajiri na muda wa kujishughulisha na maslahi mengine kama vile ya kidini au jamii na sababu za kiuhisani.

## Jinsi masoko yanavyofanya kazi

Mfumo wa mawasiliano ya mbali wa bei

Masoko mengi hufanya kazi kupitia hela. Inaweza kuwa kubadilishana moja kwa moja – kubadili mali kwa mali – au bila hiyo; lakini fedhahuleta urahisi. Muuzaji anaweza kubadilishana bidhaa au huduma kwa ajili ya hela, kisha kununua karibu kwa ajili ya thamani iliyo bora kabla ya kubadilishana bidhaa na huduma. Ina maana kwamba vinyozi wenye njaa hawana haja yakutafuta waokaji ambao wanaohitaji kunyolewa ili kufanya nao biashara.

Kawaida bei hutolewa katika fedha. Bei si kiwango cha thamani, kwa sababu thamani ipo katika mawazo ya walewatu wanaohusika na watu mbalimbali huthamini kitu kimoja kwa njia tofauti. Lakini bei hudhihirisha kitu fulani juu ya mahitaji ya watu kwa ajili ya bidhaa na kuhusu uhaba wake. Wanaakisi kiwango ambacho watu wapo tayari kubadilishana kwa jambo moja kwa jingine.

Kama kiashiria cha uhaba, ni vigumu bei kushindana. Pia huonyesha wapi kuna uhitaji mkubwa. Bei kubwa

hushawishi wauzaji kutosheleza mahitaji. Wakiona bei kubwa, wazalishaji huingia sokoni ili kupata faida kubwa,na kuelekeza rasilimali kama vile vibarua na mtaji ili kutosheleza mahitaji. Bei ya chini, vile vile, zinaonyesha kuwa mahitaji ni hafifu na kwamba rasilimali zinatumika vizuri mahali pengine.

Kwa njia hii, bei ina jukumu muhimu katika uchumi huria, kusaidia kupeleka rasilimali mahali ambapo uhitaji ni mkubwa na kupunguza ambapo kuna ziada. Wanasaidia kupunguza ufujaji: kupata faida kubwa zaidi, wasambazaji wanahitaji kutafuta pembejeo za gharama nafuu.Hiyo husaidia kuhifadhi rasilimali nakuhakikisha kwamba zinatumika kuleta tija kadri iwezekanavyo.

Athari hii huenea kutoka soko mpaka soko katikauchumi wote, na kweli katika dunia nzima. Kwa mfano, tuseme kwamba matumizi mapya ya bati yamegundulika. Wazalishaji wataanza kuhitaji bati zaidi. Watakuwa tayari kulipa zaidi ya gharama waliyokua wanalipa hapo awali. Bei ya juu itashawishi makampuni ya madinikuzalisha bati zaidi, na wauzaji wa jumla kusambaza. Lakini kwa usawa, watumiaji wengine wa bati wataanza kutafuta mbadala, badala ya kulipabei ya juu. Watahitaji vitu mbadala zaidi, na bei yake itapanda. Hiyo itapelekea watu kutengeneza vitu mbadala kwa wingi, na kuhamasisha watumiaji kutafuta vitu mbadala vya mibadala hiyo.

Kwa njia hii, bei ya kusambaza habari kuhusu uhaba katika mfumo mzima wa uchumi. Mchumi FA Hayek aliiita ni ‘mawasiliano makubwa ya simu’ ya soko, mara kwa mara akifafanua wapi ziada na uhaba huwepona kuwaambia watu wapi ni bora kuweka juhudi na rasilimali zao.

## Masoko hayawezi kuwa timilifu

Kama utasoma kitabu cha kiada cha uchumi, unaweza kupata hisia kwamba masoko ya hutegemea 'ushindani timilifu' baina ya idadi kubwa ya wauzaji wanaofanana na kuuza bidhaa za kufanana kwa wateja wanaofanana. Hawafanyi hivyo. Hizi ni dhahania za kinadharia tu.Katika hali halisi, masoko hufanya kazi - na inaweza tu kufanya kazi - kwa sababu watuna bidhaa ni tofauti.

Kama kila mtu angekuwa na thamani inayofanana, hakuna mtu angefanya biashara ya kitu chochote kile. Pande zote mbili zingethamini bidhaa sawa sawa, hivyo kusingekuwa na umuhimu wa kubadilishana. Mabadilishano hutokea tu kwa sababu sisi hatukubaliani juu ya thamani. Na tena, kama kila msambazaji angetoa bidhaa zinazofananakwa bei ya kufanana, kusingekua na kitu cha kuchagua kwa wateja baina yao. Hakuna msambazaji ambae angepita katika ushindani na kupata faida kubwa.

Lakini faida kubwa ndiyo inayowasukuma wajasiriamali kupita katika ushindani. Wanafanya hivyo kwa kufanya bidhaa zao kuwa za bei nafuu – sema, kwa mtiririko wa uzalishaji. Lakini muhimu zaidi, wanafanya hivyo kwa kutengeneza bidhaa bora zao wenyewe. Wanavumbua na kutofautisha biashara zao. Wanawapa wateja vitu vipya na bora kuliko bidhaa zilizopita. Na huonyesha hayo mabadiliko kwa matumaini kwamba wanunuaji watapendelea bidhaa zao kuliko za wengine.

Hii inafanya masoko huria kuwaelimumwendo - si elimutuamo, iliyogandishwa na isiyosogea kama ugavi wa vitabu vya kiada na grafu ya mahitaji. Wasambazaji huvumbua mara kwa mara ili kuzalisha bidhaa za kuvutia zaidi, na wateja mara kwa mara wanatafuta maboresho.

## Mipango mikuu isiyowezekana

Jitihada za serikali kuendesha uchumi na kuzalisha bidhaa wanazotaka watu haziwezi kuendana na elimumwendo ya mfumo huu wa soko.

Kuna shinikizo chache juu ya ukiritimba wa serikali kufanya uvumbuzi.Wala watendaji wa serikali hawawezi kujua nini wanachama wa umma wanataka na kuthamini. Wapate kufanya kura za maoni mara kwa mara, lakini hiyo imeondolewa kutoka kwenye ushindani wa soko wa mara kwa mara, ambapo uchaguzi wa mnunuaji unawapa wazalishaji taarifa za dakika-kwa-dakika kuhusu mahitaji yao.

Ili kufanikiwa, wajasiriamali wanatakiwa kuelewa wateja wao. Hawawezi kusubiri kwa miaka ili kupata maoni yao kuhusu bidhaa, kama serikali ifanyavyo katika uchaguzi. Wanahitaji kuweka tahadhari kwa kile mteja anachotaka, na juu ya gharama na upatikanaji wa vifaa na pembejeo. Wakala – kwa mfano,anahitaji kujua nini kinatokea katika soko la mali za mtaa – wanunuzi wapi wanapenda aina Fulani za nyumba, kwa mfano – si tu kutoka mwezi hadi mwezi, ila siku kwa siku na hata saa kwa saa. Hakuna mamlaka kuu inayoweza kukusanya taarifa hizi zinazobadilika kwa haraka, usitie shaka fanyia kazi kabla haijabadilika tena.

Baadhi ya watu wanadhani kwamba kwa sababu uchumi huria haujapangwa kutoka katikati, ni lazima itakuwa ya ovyoovyo na isiyo na mantiki. Kwa kweli, masoko yana utaratibu sana. Kwa kufuata kanuni walizokubaliana za mali na kubadilishana, watu wana uwezo wa kufanya biashara na kushirikiana, na wanatarajia matendo ya

wengine, kwa uhakika mkubwa. Masoko ni ya kimantikii zaidi. Wanatumia utaalamu wa ndani na maarifa ya mamilioni ya watu, ambao wote wanafanya mipango yao wenyewe nakurekebisha na mipango ya mabadiliko ya wengine. Mipango mingi zaidi inaendelea katika uchumi huria kuliko katika serikali kuu inayodhibitiwa - hutokea kufanyika katika ngazi ya watu binafsi badala ya ngazi ya serikali.

**Swali: Je, masoko huria yameshindwa kulinda mazingira?**

Hapana. Masoko hayajashindwa. Hakuna soko katika bidhaa zinazotunza mazingira. Masoko hufanya vizuri pale ambapo kuna uhaba na pale ambapo mashirika yasiyolipa wametengwa, na sio wakati vitu vipo vingi au pale mashirika yasiolipa hayajatengwa.

Watu wanaanza kuona, hata hivyo, kwamba kunaweza kuwa na masoko ya bidhaa-mazingira pia. Badala ya kuruhusu samaki-bahari kuvunwa mpaka kupotea, kwa mfano, idadi ya nchi sasa inaweka kikomo na kutoa ruhusa kuvuna sehemu tu ya mavuno hayo. Vibali vinauzika, na soko la haraka linaibuka, linakuza ufanisi wakati huo huo linahodhi akiba.

Na kadri watu wanavyokua tajiri, shukrani kwa uchumi wa soko huria, wanaweza kumudu kujali mazingira yao. China inakabiliwa na uchafuzi mkubwa wa mazingira kutokana na viwanda yake, lakini huko watu wanathamini ukuaji wa kiuchumi zaidi ya hewa safi. Kadri wanavyokua tajiri, kama nchi yoyote tajiri kabla yao, viwango vitabadilika na wao watakuwa na uwezo wakumudu usafi wa michakato ya viwandani inayochafua kwa kiasi kidogo.

## Makampuni yanayofadhiliwa na serikali

Mataifa machache leo yanaamini kwamba wanaweza kumiliki kwa ufanisi na kusimamiauzalishaji wa taifa

lao. Uchumi wa mataifa mengi duniani ni uchumi 'mchanganyiko' ambapo serikali inamiliki baadhi ya viwanda na kujaribu kusimamia na kuongoza pato la wengine kupitia mipango, kanuni, ruzuku, kodi na hisa za serikali.

Karne ya ishirini iliona nchi nyingi zikitaifisha sekta ya viwanda ambayo ilikuwa inasemekana kuwa ni kwa ajili ya mkakati muhimu, na nchi nyingi zinaendelea kumiliki na kudhibitiviwanda hivi - ambayo inaweza kuwa ni pamoja na mawasiliano ya simu, usafiri, benki, huduma, madini na mengineyo.

Kwa bahati mbaya, umiliki wa viwandahivyo husababisha ukiritimba wa serikali. Ukiritimba huo ni mkubwa mno kwa mtu yeyote kusimamia kwa ufanisi. Lakini haijalishi kama ukiritimba ni wa umma au ni binafsi; itafura na kuwa na uvivu na kutoa huduma mbovu katika gharama kubwa.

Umuhimu wa kimkakati wa viwanda hivi bado hauna sababukwa nini serikali inazimiliki. Benki za nchi tajirini benki binafsi: na kwa kweli, kuzibadilisha na kuwa katika ukiritimba zitaharibu benki na biashara na familia zinazowategemea. Makampuni ya kibiashara, yanayofanya kazi kama wasambazaji kwa serikali au yanayoshughulika moja kwa moja na wateja, sasa yanatoa mawasiliano mengi ya simu duniani, usafiri na huduma. Nchi nyingi zimebinafsisha makampuni yao yanayomilikiwa na serikali, wakijua kwamba huduma hizi muhimu zinaweza kutolewa ipasavyo na makampuni yenye ushindani ambayo yataleta usimamizi binafsi wa kitaalamu na mtaji binafsi.

Serikali imejifunza, hata hivyo, kwamba wanaweza kudhibitiviwanda bila ya wao kuvimiliki. Wanaweza kununua hisakatika kampuni muhimu (na kampuni binafsi), nakutumia haki zao kama wanahisa kudhibiti kile ambacho kampuni inafanya na nani anayeteuliwa kwenye bodi. Wakati mwingine wanajipa wenyewe 'hisa za dhahabu' ambazo zinawapa wao usemi wa mwisho juu ya masuala ya muhimu.

Ule muingiliano unaosambaa unaweza kukataliwa na jamii. Inapelekea umiliki wa serikali na utaifishaji, inayoruhusu serikali kufanya maamuzi ya viwanda bila kununua. Wamiliki – ikiwa ni pamoja na watu wa kawaida ambao wanaweza kuwekeza akiba zao na pensheni katika makampuni yenye dhamana ya hisa zao - zinaibiwa mali zao. Na fursa za rushwa ni kubwa – washirika wa karibu wanaweza kuzawadiwa nafasi za bodi zinazoleta faida, viwanda vinaweza kuwekwa kwenye maeneo yenye upendeleo, na pato linaweza kutumika kufaidisha wafuasi.

Serikali pia inaweza kudhibiti makampuni binafsi kupitia kanuni. Kanuni zinaweza kupunguza au kutoa mwongozo jinsi gani makampuni yajiendeshe, watengeneze nini, watoze kiasi gani,kiasi gani wawalipe wafanyakazi wao – na vinginevyo. Aina hii ya udhibiti wa serikali wa rasilimali binafsi ni wa kawaida sana, hata katika nchi wanazojiita huria – lakini ni kinyume kabisa na kanuni za umiliki binafsi ambayo ni msingi muhimu wa jamii huria.

## Biashara ya kimataifa

*Biashara dhidi ya ulindaji*

Faida zinazotokana na biashara huru kati ya watu binafsi wa nchi hiyo zinatokea wakati watu wanafanya biashara

katika mipaka ya kimataifa. Biashara inaruhusu mataifa kuwa na utaalam zaidi katika kile wanachoweza kufanya kwa ubora zaidi, na kutuma ziada zao kwa nchi ambazo ni bora katika mambo mengine. Idadi kubwa ya maua yaliyokatwa duniani, kwa mfano, yalianzia Kenya, ambapo udongo nahali ya hewa ni nzuri kwa ajili ya kukuza maua; wakati Chile, Australia na Ufaransa hujulikana kama wazalishaji wanaoongoza katika mvinyo kwa sababu ya ardhi yao na hali ya hewa na utaalamu wao waliojijengea. India, pamoja na nguvu-kazi yake nafuu lakini yenye elimu nzuri, imekuwa nchi muhimu kwa huduma za habari na mawasiliano na uzalishaji. Biashara ya kimataifa inaruhusu watu kuwa utaalam na kujengamitaji kama vile zana na vifaa vya kufanya uzalishaji wao kuwa wa gharama nafuu zaidi.

Na kwa sababu maadili ya watu katika nchi mbalimbali hutofautiana kwa undani zaidi kuliko maadili ya watu katikanchi moja, fursa za manufaa kwa pande zotekwa njia ya biashara ni kubwa zaidi. Katika zama za kati, kwa mfano, wasafiri kutoka Ulaya walilipa bei kubwa kwa ajili ya bidhaakama vile chai ambayo ilikua inaota kwa urahisi na kwa wingi huko India na China, aukwa ajili ya viungo ambavyo vilikua nafuu katika Mashariki ya Kati. Leo, watu wanaruka pande zote duniani kutembelea usanifu wa majengo ya Venice au utamaduni wa Thailand, wakishangaa jinsi tofauti ulivyo na nchi zao za nyumbani.

Jamii huru ipo wazi kwa bidhaa kutoka nchi zote. Inatambuafaida ya biashara, na jinsi gani biashara husaidiakueneza mafanikio. Mbadala ni ulinzi, ambaponchi hufanya jaribio la kulinda wauzaji wao wenyewe kwa kuweka pembeni uagizaji wa bidhaa kutoka nchi nyingine. Hii inatoa ahueni kwa wauzaji wa ndani.

Lakini ina maana kwamba walaji wa ndani wananyimwa bidhaa nafuu na huduma kutoka nje ya nchi. Wanalipabei ya juu ili kulinda wazalishaji wa ndani, wana uchaguzi mdogo na wanatakiwa kuendana na bidhaa maskini.

Ulindaji ni kufuja

Nchi inapozalisha kitu nyumbani ambacho kingeweza kuzalishwa kwa ubora zaidi au nafuu nje ya nchi, ni ufujaji wa rasilimali (ikiwa ni pamoja narasilimali za kimazingira). Adam Smith alisema kuwa kwa njia ya hewa chafu, zabibu inaweza kulimwa katika baridi, sehemu za mvua za Scotland - lakini kwa gharama mara thelathini ya kuzilima katika mwanga wa jua asili wa Ufaransa. Kwa nini upoteze rasilimali – muda wako, fedha na juhudi - kujaribu kufanya kitu mwenyewe wakatimtu mwingine anakifanya kwa ubora na bei nafuu zaidi?

Bila kushangaza, wazalishaji fanisiwatapewa nchi nyingine ili kujaribu kuweka bidhaa zao pembeni kwa njia ya makatazo, upendeleona ushuru. Wanaweza pia kulipiza kisasi kwa kuongeza vikwazo vyaomwenyewe. Vita hivyo vya biashara havimfaidishi mtu. Ni bora zaidi – hasakwa wakazi maskini wa nchi zote mbili, ambao wanafaidika kutoka kwa bidhaa za nje za bei nafuu - kama mipaka yote ni itaondolewa na watu kuruhusiwa kufanya biashara kama wao watakavyochagua.

Hali kadhalika kwa uhamiaji. Katika jamii huriaserikali inaweza isiweke vikwazo juu ya watu wanaohama kati ya nchi na nchi. Wahamiaji huleta nguvu na mawazo mapya ambayo yanafaidisha nchi wanayohamia. Mawimbi ya uhamiaji katika Ulaya naAmerika ya Kaskazini, kwa mfano, yametengeneza mafanikio makubwa sana. Kuachaudhibiti ambao umekuwepo mahali kwa miongo

kadhaa haiwezi kuwa rahisi, na inaweza kusababisha matatizo makubwa ya muda mfupi, lakini ni lazima ibaki kuwa lengo kuu kwa waumini wa jamii huru.

Biashara huru kwa vitendo

Nchi zenye utawala wa biashara ulio wazi unakua kwa kasi na kuwa na mafanikio zaidi kuliko wasio nao. Fikiria miji midogo ya kibiashara kama vile Hong Kong na Singapore – hakuna mji mmoja kati yaowenye rasilimali nyingi za asili ili kuwasaidia. Katika miaka ya 1960, walikuwa maskini kamanchi nyingi za Afrika na Caribbean ambazo zilikuwa na rasilimali nyingi. Leo, tunashukuru biashara na huria wa uhuru wa kiuchumi, wao ni tajiri maradufu.

Kuenea kwa biashara kumepunguza umaskini kwa kiasi kikubwa. Baadhi ya watu wanahofu kwamba kuruhusu katika bidhaa kutoka nje, na hasa uwekezaji wa nje, itasababisha unyonyaji wa wakazi - kama vile ‘maduka ya peremende’ kuzalisha viatu au nguo.Ukweli ni kwamba hakuna mtu yeyote anaelazimishwa kufanya kazi katika viwanda; lakini watu wengi hupendelea sana kufanya kazi katika viwanda kwa ajili ya mshahara ya mara kwa mara kwa ili kuwaunga mkono wafanyakazi walio chini ya jua kali bila uhakika na ujira mdogo. Katika nchi kama vile Vietnam, ambapo uwekezaji wa nje umefika, wafanyakazi hao wa viwanda wanaweza sasa kutamanikumiliki motokaa, televisheni na anasa nyingine ambazo wao hawajawahi kuota kabla.

Karibu bidhaa zote za kisasa leo - kama vile simu za mkonoau kompyuta - inahusisha rasilimali, ujuzi nautaalamu zilizokusanywa kutoka duniani kote. Wabunifu wanaweza kuwa wanaishi California, lakini watengenezaji wanaweza kuwa wanasimamiwa na watu

kutoka Hong Kong na kufanywa na wengine katika China. Vyuma na vifaa vingine vilivyotumika katika bidhaa hiyo vinaweza kuwa vimechimbwa kutoka Asia, Australia au Amerika ya Kusini. Bidhaa inaweza kusafirishwa na shirika la meli kutoka Ugiriki au mashirika ya ndege yanayotokea Uholanzi. Na watumiaji, bila shaka, kutoka duniani kote.

Kadri watu wanavyofanya biashara na nchi nyingine, huelewa vizuri, au angalau kuwapa heshima yao. Wafanyabiashara hawawezi kujiona bora zaidi kuliko mataifa au jamii nyingine. Kujifaidisha wenyewe, inabidi wafanye kwa amani biashara na wengine kama wasambazaji au washirika au wateja. Biashara ya kimataifa inazalisha ufahamu na amani, ambayo ina faida zake pana. Si jambo la kushangaza kuwa jamii nyingi huru na wazi ni zile ambazo zina biashara huria na wazi.

# 6 MALI NA HAKI

Katika sura ya 4 tumeona kuwa 'haki' ina maana bayana sana – namna gani watu watendeane, badala ya namna gani thawabu za matendo yao kugawanywa baina yao. Lakini kanuni zinazoongoza namna watu wanavyotendeana ni tata. Kuzitunza na kusimamia utekelezaji wake kunahitaji maadili fulani na taasisi za kijamii – vitu kama umiliki mali, utawala wa sheria na kuheshimu haki za watu wengine.

## Mali binafsi

*Maana ya mali*

Uwezo wa watu kumiliki mali ni muhimu katika utendaji kazi wa jamii huru. Umiliki mali humaanisha kuwa unaweza kushika na kuongoza kitu fulani, na – muhimu – ni kwamba una mamlaka ya kutowahusisha wengine katika hiyo. Unaweza kuifurahia, kuikodisha, kuiuza, kuigawa au hata kuiharibu, lakini watu wengine hawawezi kuichukua kutoka kwako pasipo ruhusa yako. Mali yako haiwezi kuchukuliwa kihalali kutoka kwako.

Watu binafsi wanaweza kumiliki mali, vivyo hivyo makundi kama vile wanandoa, washirika wa kibiashara na makampuni, na serikali na vyombo vya umma.

Mali siyo mara zote huwa kitu fulani kinachoshikika na kisichohamishika kama ardhi au jingo. Inaweza kuwa kitu kinachohamishika, kama vile wanyama wa shambani, gari au kipande cha nguo. Kinaweza kuwa kitu kisichoshikika pia. Inaweza kuwa zao la akili kama vile alama ya kibiashara au hatimiliki juu ya kitu ulichoandika au kurekodi, au leseni ya ugunduzi/ubunifu wa kitu. Inaweza kuhusisha hisa katika kampuni, deni unalomdai mtu au akiba yako. Inaweza kuwa mkataba wa kukodi ardhi ya mtu kwa kipindi fulani au haki ya kituo cha redio kutumia masafa fulani. Mali, hivyo, siyo tu kitu fulani kisichohamishika na kinachoshikika.

Mali inaweza kutengenezwa pia. Gari au vazi huundwa kwa kutumia sehemu muunganiko na kutokea mali mpya. Mnyama wa shambani huzalishwa na kukuzwa akawa mkubwa. Watu huandika vitabu vipya, huunda vifurushi vipya vya akiba. Teknolojia ya kidijitali imeruhusu uundwaji wa namba nyingi za chaneli za simu za mkononi – aina mpya kabisa ya miliki.

Kwa umuhimu, mali yako pia inajumuisha haki juu ya mwili wako na haki ya kufurahia matunda ya kazi yako mwenyewe. Katika jamii huru, huwezi kukamatwa na kufungwa bila sababu ya maana. Huwezi kulazimishwa kisheria kufanya kazi kwa ajili ya mtu mwingine. Wala watu wengine hawaruhusiwi kuiba ulichokiunda kwa ujuzi wako, kipaji chako, maarifa na juhudi zako.

*Mali na maendeleo*

Umiliki binafsi wa mali ni mkongwe kama binadamu wenyewe, japo haujakuwa ukiheshimiwa siku zote. Katika milki ya zamani ya Sparta, wazo la umiliki binafsi wa mali lilipuuzwa. Miaka ya hivi karibuni, nchi kama Urusi na

China zimejaribu umiliki wa kijamaa wa mashamba na viwanda. Lakini ilikuwa kwa kukubali hatua kwa hatua umiliki binafsi wa mali, na kulinda hilo ndiko kukapelekea kuibuka na kukua kwa biashara ya kisasa – na kuleta ongezeko kubwa la utajiri miongoni mwa mataifa yanayofanya biashara.

Ni rahisi kuona ni kwa nini hivyo. Mwanaikolojia Garrett Hardin aliandika kuhusu 'balaa ya mali ya pamoja'. Pale watu wanapomiliki rasilimali, wanasukumwa zaidi kuitunza na kuiboresha kuliko wasipokuwa wamiliki. Ardhi inayomilikiwa binafsi hulimwa kwa namna bora zaidi kuliko ikilimwa kijamaa. Ngazi za majengo yanayotumiwa pamoja na sehemu za pamoja za majengo huwa chafu na zilizochakaa, japo vyumba vya watu binafsi huwa vimetunzwa vyema. Watu hawaoni sababu ya kwa nini watumie pesa na juhudi kubwa katika kitu wasichokimiliki, kwa kuwa watu wengine watapata faida pasipo kuifanyia kazi.

Ulindaji wa mali na kuheshimu umiliki wa mali huruhusu watu kujenga mtaji wa uzalishaji. Wakulima wanatazamiwa zaidi kupanda mbegu, kulima mazao na kununua matrekta ikiwa ni wamiliki wa mavuno yatokanayo na juhudi hizo. Wajasiriamali wanaweza kujitolea kuwekeza kwenye viwanda, vifaa na mitandao ya uzalishaji ikiwa wa maamuzi yao wenyewe namna gani mali zao zitatumika na kuwa wengine hawana haki ya kuzichukua. Ikiwa hakimiliki zinalindwa na kuheshimiwa, watu watajenga mtaji wa uzalishaji na uzalishaji utaongezeka na kusaidia jamii nzima. Lakini ikiwa mali zinaweza kuibwa na kuharibiwa na wengine, au ikiwa mtu mwingine anaweza kuchukua mazao inayozalisha, hakuna msukumo kwa watu kuwekeza ujuzi wao, muda, fedha, jitihada na utaalamu kwenye uzalishaji – na jamii nzima huathirika.

*Hakimiliki na haki nyingine*

Haki na uhuru ambao watu wanafurahia katika jamii huru vimejengwa katika umiliki mali. Pasipo umiliki binafsi wa mali hakuwezi kuwepo haki na uhuru.

Chukulia kwa mfano haki ya kuzungumza kwa uhuru, kushirikiana na wengine, na kushiriki katika mchakato wa kisiasa. Kusingekuwepo mali binafsi – ikiwa baadhi ya serikali zinamiliki rasilimali zote – wagombea wangewezaje kufanya kampeni za uchaguzi? Ili kufikisha ujumbe wao, watahitaji kukodi kumbi za mikutano, kuchapisha vipeperushi na kutangaza maoni yao. Lakini ikiwa serikali inamiliki kumbi zote, viwanda vya uchapishaji na karatasi, na ikiwa inamiliki vituo vyote vya matangazo, ingeweza kuzuia kabisa yeyote kupiga kampeni. (Hasa ikiwa mgombea ni mpinzani wa sera za serikali, nafasi ya jambo kama hili kutokea ni kubwa zaidi). Mbaya zaidi ikiwa watu hawamiliki mali zao wenyewe, kusingekuwa na kuizuia serikali kuwanyamazisha wapinzani wao kwa kuwakamata au kuwaua. (Ni ya kushtusha, lakini mifano ya haya ni ya kawaida sana.)

Pasipo umiliki mali, hakuna haki. Isipokuwa una haki juu ya mwili wako mwenyewe, nguvukazi yako na miliki zako, vinaweza kuchukuliwa kutoka kwako pasipo fidia. Ikiwa hauna haki kwa mwili wako, waweza kukamatwa hovyo tu, kufungwa na kuuawa; ikiwa hauna haki juu ya nguvukazi yako, waweza kutumikishwa; ikiwa hauna haki juu ya miliki zako, waweza kuporwa. Hakutakuwa na ulinzi dhidi ya dhuluma.

*Manufaa ya kimaadili ya mali*

Mali na ulindaji wa haki za mali, humpa mtu kinga muhimu dhidi ya nguvu ya dola na uonevu wa wengine.

Kumiliki mali huwapa watu uwezo wa kujilinda wenyewe na kufanya maamuzi yao wenyewe, kutengeneza mipango yao wenyewe, kusaka wanavyopendelea wenyewe na kuelezea maoni yao bila kuwa wahanga wa matakwa ya wengine ama serikali au watu binafsi.

Mali na kanuni za biashara zinazokua kutoka humo huruhusu watu kushirikiana kwa amani na kwa manufaa ya wote. Inawawezesha kuishi na kila mmoja na kushirikiana rasilimali za asili na matunda ya kazi yao kulingana na kanuni walizokubaliana pasipo migogoro, vurugu na uonevu.

Mali hazichochei tu ushirikiano wa amani; bali pia hufanya ushirikiano kuwa muhimu kwa yeyote anayetaka kuboresha hali yake. Watu hawawezi tu kuchukua wanachokitaka kwa lazima. Mali huweza kuhamishwa – kuuzwa, kukodishwa, kumilikiwa kwa pamoja, kupangishwa au kutolewa – ila tu kwa matakwa ya mmiliki. Jamii huru zaidi zina mfumo imara zaidi wa kulinda haki hii muhimu, kanuni kama vile za kulipa madeni na kuheshimu mikataba. Watu huru huona hii kuwa njia adilifu zaidi ya kuhamisha rasilimali kuliko kuchukuliwa kwa lazima au kuibwa kwa ubadhirifu.

*Hisa katika jamii*

Siyo wale wanaomiliki mali pekee wanaonufaika na yote haya. Kwa kuchochea uwekezaji, ukuzaji mitaji na biashara, jamii yote hufaidika. Kwa mfano, wakazi wa mijini wasio na ardhi yao wenyewe hupata chakula, shukrani kwa msukumo walionao wakulima wa kukuza mazao yao wenyewe na kuuza kwa hiyari kwa wateja. Hiyo ni shukrani kwa haki za umiliki ardhi na mazao kwa wakulima. Matokeo huwa kinyume chake kwa namna

ya kushtusha katika nchi ambako haki ya umiliki mali haikulindwa – kwa mfano, katika nchi ya Zimbabwe chini ya Robert Mugabe, ambako watu walitiwa moyo kuchukua ardhi iliyoendelezwa na wakulima kama ya kwao. Kadri wakulima (wengi wakiwa wazungu) walivyoondoka, matokeo haikuwa kuongezeka kwa ustawi, bali kushuka: pasipo kanuni bayana za umiliki wa ardhi, uzalishaji huanguka na wakazi wa mijini wanajikuta wakihangaika kwa uhaba wa chakula.

Katika jamii huru, ulindaji wa haki za mali za watu ni jukumu muhimu la serikali. Husaidia watu kujilinda dhidi ya uonevu wa wahalifu na wakwasi wachache wenye nguvu. Umilikaji binafsi wa mali unampa kila mmoja nafasi katika jamii na kujali umuhimu wa ushirikiano wa amani. Kila mmoja anafaidika kutokana na haki ya umiliki mali ambayo huchochea rasilimali zinazomilikiwa kuendeshwa vizuri, na kuruhusu mtaji wa uzalishaji kujengeka na kuwa endelevu. Umiliki mali katika jamii huru si maalumu kwa ajili ya wachache. Ni wazi kwa ajili ya kila mtu na kwa faida ya wote.

## Kanuni za haki

*Kuitafuta haki*

Haki ni kanuni ambazo hutumika kutoa thawabu na adhabu. Zimejengwa katika namna ya kawaida ya watu wanavyojisikia kuhusu kitu watu wanastahili kama matokeo ya matendo yao. Ikiwa mtu kwa makusudi anawadhuru wengine, watu wengi hukubaliana kuwa anapaswa kumfidia mwathirika au kupata adhabu kwa kosa lake.

Kanuni za haki si vitu tunajitungia tu wenyewe. Ni

sehemu ya asili yetu kabisa. Baadhi ya watu huamini kuwa sheria hii ya asili tumepewa na Muumba wetu na imefunuliwa kwetu kupitia dini zetu. Wengine, kama mchumi mwanafalsafa mwenye tuzo ya Nobeli, F.A. Hayek, huchukua mtazamo wa kimageuzi, kwa kudai kuwa kanuni za haki zimekua pamoja nasi kwa sababu hutusaidia kuishi kwa amani kama viumbe wa kijamii. Vyovyote vile, huwa tunajisikia hisia za haki kiasili ambazo hutusaidia kujenga ushirikiano na jamii inayofanya kazi vyema. Ikiwa tusingekuwa na hisia hizo na kutojisikia ukosekanifu wa haki – ikiwa hatungechukua hatua pale watu wanapoporwa au kuuawa, tusingeweza kuishi kwa kitambo kirefu.

Hivyo, bunge na mahakama za jamii huru haviwezi kulazimisha ipi ni haki. Kanuni zozote wanazoweza kuzifikiria haziwezi kufanya kazi vema zaidi ya zile ambazo ni sehemu ya asili yetu. Wanachoweza kutumainia zaidi ni kugundua kanuni za haki ni zipi.

Mtu anaweza kuona hii katika utendaji kazi wa sheria ya kawaida au mfumo wa sheria wa sehemu fulani. Migogoro baina ya watu – migogoro ya mipaka baina ya majirani kwa mfano, hupelekwa mahakamani. Mahakani itapaswa kuamua uamuzi upi utakuwa wa haki, kutegemea na hali ya kila kesi. Mgogoro mwingine wa ardhi unaweza kuwa unafanana kwa namna moja ila si nyingine, na mahakama inapaswa kujaribu tena kutafuta uamuzi wa haki. Mahakimu hawafikii tu uamuzi. Hutumia kanuni zilizokubalika kwa muda mrefu katika masuala mapya. Na kupitia mchakato mrefu wa kujaribu kama huu, huibuka uelewano juu ya tabia ipi kati ya majirani ichukuliwe kuwa ya sawia na ipi siyo.

*Haki si sheria, maadili wala usawa*

Sifa ya msingi ya kanuni za haki katika jamii huru ni kuwa zifanye kazi sawasawa kwa kila mmoja. Watu tofauti katika suala la aina moja watendewe kwa namna iyo hiyo. Sheria na haki siyo mara zote ni kitu kimoja. Kwa mfano, sheria zinaweza kutowatendea watu kwa usawa mara zote. Zinaweza kuwa zimeundwa na wataalamu ambao wamelenga kuwalinda marafiki na kuwadhuru maadui zao. Hizi ni sheria zisizo za haki.

Pia haki na maadili si kitu kimoja. Wengi huwezi kuitazama ngono kabla ya ndoa kuwa si maadili kabisa. Lakini hiyo haiifanyi kutokuwa haki. Hakuna mwingine anadhurika na matenda ya makubaliano kama hayo; kwa hivyo, chini ya kanuni ya kutodhuru wengine, si haki kuwaadhibu wale wayafanyao. Tena sheria zinazowaadhibu si za haki. Ikiwa sheria inaweza kuwaadhibu watu kwa sababu tu wanaona tabia yao kuwa ya kuchukiza, hakutakuwa na uhuru umesalia kwa yeyote kati yetu.

Usawa pia si sawa na haki. Ukweli kuwa kuna watu ni matajiri na wenine masikini haifanyi jamii kutokuwa ya haki. Jamii isiyo na uwiano wa usawa inaweza kuwa na haki sawa na ile ambayo ina uwiano wa usawa. Ikiwa tu watu wanapata mali zao kihalali pasipo uonevu, wanatenda kwa haki kabisa.

Baadhi ya wakosoaji wa mali umiliki binafsi wa mali husema mali zimeanzia katika wizi tu. Hii si kweli. Watu wa kwanza kudai kumiliki pori lililokuwa halitumiki au kutakiwa na mtu hawakumdhuru yeyote. Ikiwa wamenufaika kwa kuilima au kwa kuvumbua madini ya thamani, hiyo ilikuwa bahati yao: hakuna aliyeathiriwa na kufanywa masikini, hivyo hakuna uonevu uliofanywa.

Vivyo hivyo kwa mjasiriamali anayewekeza kwenye bidhaa au mchakato mpya na kuwa tajiri kwa kuwauzia wanunuzi waliohitaji, hakuna aliyedhurika: badala yake dunia nzima imenufaika kwa uvumbuzi husika.

*Utekelezaji wa haki*

Lengo kuu la jamii huru ni kupunguza matumizi ya nguvu. Lakini haki hupaswa kusimamiwa kwa namna fulani. Ikiwa watu watawadhuru wengine, tunatarajia waadhibiwe, ama kwa faini au kifungo. Hii itamaanisha matumizi ya nguvu dhidi ya mhalifu. Ili haki kutawala, kiasi fulani cha matumizi ya nguvu hakikwepeki.

Jamii huru hutatua mtanziko huu kwa kutoa mamlaka juu ya nguvu za dola kwa mamlaka za kijamii. Wao pekee ndiyo huweza kutumia nguvu, na ni kwa ajili tu ya kusimamia haki na kuwalinda wananchi dhidi ya maadui wa ndani na nje. Matumizi ya nguvu na watu wengine ni marufuku.

Ikiwa serikali pekee ndiyo ina mamlaka ya kutumia nguvu, inapaswa kubanwa sana. Serikali zimeundwa na wanadamu, na hakuna mwanadamu anaweza kuaminiwa kumiliki nguvu pasipo udhibiti. Vishawishi vya kuitumia kwa manufaa binafsi ni vikubwa mno.

Vivyo hivyo, mfumo wa haki wa jamii huru huwa na kanuni kali zinazodhibiti utumizi wa nguvu za dola na mamlaka. Kwa mfano, kunapaswa kuwepo kanuni imara juu ya nguvu za watawala za kupeleleza na kukamata, namna kesi zinavyoendeshwa na namna adhabu zinavyotolewa. Hizi kanuni ni za mchakato wa namna maamuzi yanavyotolewa, na si kitu gani kinachoamulia. Kanuni hizi zinapaswa kufuatwa ikiwa mchakato wa kisheria utatazamwa kuwa wa usawa na haki.

*Vitisho kwa haki*

Mfumo huu unahitaji kuwa imara ikiwa tunataka watu wasishitakiwe kwa uonevu wa nguvu za dola. Huweza kuvurugwa kirahisi, hata na watu wanaodhani wanafanya kwa manufaa ya haki. Majaji kwa mfano, wakati mwingine hudhani kazi yao ni kutengeneza matokeo ya usawa badala ya kufuata kanuni za mchakato. Lakini matendo hayo ya kihakimu huinua maoni binafsi juu ya haki. Pia huweza kufanya matokeo ya mchakato wa kimahakama kutotabirika: kosa hilo moja linaweza kupewa adhabu tofauti kutegemeana na jaji. Na huwapa walioko mamlakani nguvu kubwa zaidi ya ushawishi juu ya matokeo ya mchakato wa kimahakama, ikiwa wataweza kuwahonga au kuwatisha majaji, wanaweza kubadili adhabu za watu. Lakini ikiwa kuna kanuni za mchakato ambazo lazima zifuatwe katika kila kesi, ushawishi huo unazuiwa. Hii ni ulinzi muhimu kwa wanaokwenda Mahakamani.

Njia nyingine inayodumaza usimamizi wa haki ni wazo la ‘haki ya kijamii’. Kutengeneza mfumo wa ugawaji sawa zaidi wa ugawanyaji wa utajiri na kipato unakinzana na kanuni za umiliki mali na haki. Ili kuwa na mgawanyo sawa, mali itapaswa kuchukuliwa kutoka kwa baadhi ya watu na kupewa wengine. Kanuni za umiliki, ambazo huwapa watu haki ya kumiliki mali na kuiachia wanavyotaka itapaswa kuchanwa. Kwa mara nyingine tena, tunapowapa watawala mamlaka kubwa kama hiyo, hakuna aliye salama. Biashara zitafeli pia; kwa nini mtu ajitie katika hatari na bidii ya kumiliki mali ikiwa mamlaka zaweza kuipokonya?

Kanuni mahsusi zinazopaswa kutumika kwenye umiliki mali haziko dhahiri hata hivyo. Je, umiliki wangu wa kipande cha ardhi unanipa haki ya kuchimba madini

yaliyomo chini yake? Je, inanipa fursa ya kuzuia watu kuruka kwa ndege juu yake? Naweza kuzuia kiwanda cha jirani kuchafua hewa yangu kwa moshi wao? Hivyo vyote bado kuamuliwa. Na katika jamii huru vinaendelea kuwa katika hali hiyo, kwa kujaribiwa na kuboreshwa katika mahakama na majaji wasio na hisia kali ambao hujaribu tu kujielekeza katika kutambua zipi hasa ni kanuni za haki.

*Haki ya asili*

Katika jamii huru, utungaji na usimamizi sheria wote lazima ufuate kanuni za haki – kanuni ambazo zimejenga mizizi ndani sana katika ubinadamu wetu ambazo huitwa haki ya asili.

Kwanza, sheria lazima zijulikane, ziwe wazi na za kutegemeka. Ikiwa sheria ni za siri na zinabadilika kila mara, mtu hawezi kufahamu ikiwa anazivunja, hivyo hawezi kujizuia kushtakiwa.

Sheria pia zinapaswa kutabirika. Watu waweze kujua mahali sheria zinapofanya kazi na zisipohusika, na yapi yatakuwa matokeo ya kuzivunja. Hata katika jamii zinazochukuliwa kuwa huru, sheria mara nyingi huwekwa kwa ajili ya lengo moja – kama vile kupambana na ugaidi au uhalifu wa kupangiliwa – na kisha kutumika kwa lengo lingine kabisa. Wananchi wanaweza kujikuta wakikumbana na adhabu kali kwa makosa ambayo kiukweli yalikuwa madogo sana.

Pili, sheria haziwezi kuwa kwa ajili ya mambo ya kale. Zinaweza tu kuwa kwa ajili ya matendo yajayo. Kinyume chake, watu wanaweza kujikuta wakishtakiwa kwa mambo ambayo yalikuwa halali wakati wakiyatenda. Kwa

mara nyingine tena, jamii zinazochukuliwa kuwa huru zimefeli hapa napo. Kwa mfano, mwaka sheria ya mwaka 2008 ya Uingereza inayozuia aina fulani ya ukwepaji kodi ilirekebisha sheria ya awali kwa namna ambayo ilipelekea deni la kodi kwa watu 3,000 ambao hawakuwa wakikiuka sheria kwa wakati huo.

Kanuni ya tatu ya haki ni kuwa, sheria haipaswi kulazimisha watu kufanya mambo yasiyowezekana, kwa kuwa hilo litafanya iwe vigumu kwa watu kujizuia kuvunja sheria. Hata nchi zinazochukuliwa kuwa huru bado zinashindwa katika hili, hasa pale sheria zinapokinzana: hivyo sheria za moto hutaka mmiliki wa jingo kuweka njia ya kukwepea moto katika jingo wakati sheria za mipango hukataza majengo kubadilishwa – hivyo kwa namna yoyote ile mmiliki anavunja sheria. Cha kusumbua zaidi ni kuwa, serikali zisizo za haki zinaweza kutumia sheria zisizotekelezeka kwa ajili ya kuwanyanyasa wapinzani wake.

Kanuni nyingine ya msingi ya haki ya asili ni kuchukuliwa kuwa huna hatia. Hakuna yeyote anapaswa kutendewa kama mhalifu mpaka itakavyothibika hivyo, hata katika kesi zinawakabili kuonekana zimewabana mno. Hii inamaanisha ni muhimu kwa mamlaka kuthibitisha makosa yao, na si kwa wao kuthibitisha kutokuwa kwao na hatia. Hii hufanya iwe vigumu kwa serikali kuwanyanyasa maadui wake kwa mashtaka ya kusingizia: mashtaka yote yanapaswa kuthibitika mahakamani kabla ya watu kuadhibiwa.

Kanuni ya mwisho ya msingi ni kuwa, majaji na mahakama wawe huru na mamlaka za kisiasa. Kunapaswa kuwepo mgawanyo wa mamlaka baina ya watengenezaji na watafsiri wa sheria. Majaji wasiwe tu mawkala wa

wanasiasa: mitazamo yao ya kisiasa isichochee namna wanavyoendesha kesi. Ikiwa majaji wako karibu sana na wanasiasa kiasi cha kuwa rahisi kuwashawishi na kutishwa nao, basi mfumo wa mahakama unakuja kuhudumia maslahi ya wanasiasa badala ya haki halisi. Jamii huru zaidi huwa na chombo huru cha kuteua majaji au kuwateua kwa maisha yao yote ili kupunguza ushawishi wanaoweza kuwa nao wanasiasa juu yao.

## Utawala sheria

*Maana ya utawala wa sheria*

Hakuna kinachotofautisha jamii huru na isiyo huru kwa uwazi zaidi kama utawala wa sheria. Hili ni wazo kuwa ria wanapaswa kutawaliwa kwa kanuni za wazi na jumla za sheria badala ya mapendeleo ya kubadilika ya wafalme na wanasiasa. Wabunge hawawezi kujifanyia vyovyote wanavyojisikia. Sheria zao zinapaswa kufanya kazi kwa kila mmoja, ikiwemo na wao.

Malengo ya sheria ni kuwalinda watu dhidi ya utumizi wa nguvu ya hiyari. Ikiwa tunazipa serikali umiliki wa nguvu zote, tunapaswa kuhakikisha inatumika tu kwa ajili ya masuala yaliyolengwa, kukiwa na uwajibikaji na kwa manufaa ya watu wote katika jamii, si wapendelewa wachache.

Utawala wa sheria huhakikisha kuwa walioko mamlakani wanakumbana na adhabu zile zile kwa uhalifu na makosa kama wengine. Idadi ya kushtusha ya nchi huwapa watawala walio madarakani na wastaafu kinga dhidi ya kushtakiwa – na matokeo yake wengi kati ya viongozi hao wamekwepa mkono wa sheria. Japo kuna hoja ya kuwalinda viongozi wa umma – na mwingine yeyote – dhidi

ya mashtaka yasiyo na msingi wowote (au yaliyochochewa kisiasa), hakuna hoja ya kumpa yeyote kinga dhidi ya haki kwa uhalali.

Utawala wa sheria hivyo, huegemea katika kanuni za jumla na za kudumu badala ya maamuzi yanayobadilika badilika ya watawala. Hutuhakikishia haki ya asili kupitia kanuni kama usawa mbele ya sheria, mchakato sahihi wa sheria, uhuru wa mahakama, haki isiyopendelea, kutoshikiliwa kwa muda mrefu bila mashtaka, kutosumbuliwa na mamlaka (kwa mfano kwa kushitakiwa kila mara kwa jambo hilo hilo – kinachoitwa kwa hatarini mara mbili), kuchukuliwa huna hatia (mpaka itakapothibitika vinginevyo) na uhakika, uimara na utekelezekaji wa sheria. Na muhimu, watu wanaotengeneza sheria wanabanwa nazo kama walivyo wengine. Jamii haiwezi kuwa huru ikiwa baadhi ya watu, hata wawe juu vipi, hawawajibiki kwa matendo yao.

*Kuulinda utawala wa sheria*

Nchi zina namna tofauti ya kuzuia utawala wa sheria usiharibiwe na walioko mamlakani. Hii hujumuisha katiba zilizoandikwa, mchakato wa kimahakama ulijengwa kwenye sheria zilizoko tayari na za kawaida, na kuhakikisha haki ya asili.

Katiba zilizoandikwa hutoa nguvu kwa utawala wa sheria. Lakini ni rahisi sana kuunda katika wakato taifa jipya linaanza, wakati wananchi wanaanza kuwa pamoja kwa mara ya kwanza kuliko katika nchi iliyokua tayari, ambako watawala tayari wamewekeza maslahi yao na wameshika hatamu za utawala na wako katika nafasi ya kuchngesha katiba  mpya kwa maslahi yao wenyewe.

Utawala wa sheria unaweza pia kusaidiwa na miaka uzoefu kadri kesi tofauti zinavyokwenda mahakamani. Watu wanaweza kupinga maamuzi ya wabunge na maafisa na kupima haki yake na uhalali wake mahakamani. Taratibu, kunajengeka alama zinazoonyesha mipaka ya nguvu za wenye mamlaka.

Njia ya tatu ya kusaidia utawala wa sheria ni kuchochea mjadala juu ya kanuni za haki na kanuni zinazotegemeza mapatano katika jamii. Ikiwa uhuru wa kuzungumza upo na yeyote yuko huru kujadili mawazo haya, itazidi kuwa vigumu kwa mamlaka kupindisha uelewa wao kwa manufaa yao wenyewe

Wazo moja la msingi linalotokana na mjadala wa utawala wa sheria ni kuwa, ikiwa watu wanakuwa wamekutana kwa mara ya kwanza kuamua namna gani waongozwe, hakuna ambaye angekubali kulazimishwa na wengine, isipokuw katika baadhi ya maeneo – kama vile adhabu kwa wizi au vurugu – ambazo wote wataona ni kwa ajili ya manufaa yao ya muda mrefu. Hivyo, tunaweza kuhitimisha kuwa jamii zote huria zinapaswa kujengwa katika kanuni za jumla zinazozuia matumizi ya nguvu na kuzuia makundi fulani kuwa na uwezo wa kuwanyonya wengine.

*Usimamizi wa haki*

Njia zozote zile zilizochaguliwa kuulinda utawala wa sheria, kuna mbinu mahsusi zinazoweza kusaidia.

Majaji wanapaswa kuwa wenyewe huru, na huru kisiasa. Vinginevyo, mfumo wa mahakama hautaheshimiwa na uonevu mkubwa utatokea kwa kisingizio cha kutenda haki. Katika nchi nyingi, majaji wanalipwa kidogo, hawawajibiki na wana usimamizi mbovu: hivyo hufanya maamuzi ya

kesi kwa misingi ya hongo badala ya sheria. Badala yake, majaji wanapaswa kulipwa vizuri na kuchunguzwa mara kwa mara ili kwamba rushwa ya namna hiyo isiwepo wala kuvumiliwa.

Mfumo wa utoaji haki unahitaji kutegemezwa na usimamizi mzuri wa mahakama. Katika nchi nyingi inaweza kuchukua miezi au hata miaka hata kwa jambo dogo kufika mahakamani kwa sababu ya urasimu mwingi uliotokana na maafisa kukosa msukumo wa kusimamia kesi. Mfumo wa kisheria uliojengwa kwenye marejeo huruhusu mapitio ya haraka ya kesi na maamuzi yaliyopita, hivyo kesi hazihitaji kuletwa upya mahakamani kwa kupoteza muda kwa sababu ya kukosa rekodi ya marejeo ya zamani.

Katika nchi nyingi, polisi pia ni sehemu ya tatizo badala ya suluhisho. Kwa sababu ya mamlaka yao ya kukamata na kuzuia, huweza kuwatendea watu kwa uonevu kwa manufaa yao wenyewe kupitia rushwa. Maafisa wanaotoza 'faini' ndogondogo kwa sababu ya makosa ya barabarani halisi au ya kutunga ni dalili ya hilo. Inakuwa sehemu ya utamaduni uliopo – lakini utamaduni wa hongo ukizoeleka, hakuna kanuni ya kuweza kupinga vitu hivyo vibaya. Polisi wanahitaji kufunzwa vyema na kusimamiwa, hasa na chombo huru chenye nguvu ya kupeleleza na kutendea kazi malalamiko dhidi yao.

Watumishi wa umma pia wanapaswa kuteuliwa kwa sifa zao badala ya upendeleo wa kisiasa. Wanapaswa kuwa wawajibikaji hasa. Kuchukua maamuzi kwa sababu za kisiasa au manufaa binafsi kunapaswa kuadhibiwa.

Chaguzi zinapaswa kuendeshwa kwa usawa na haki na utawala wa sheria unapaswa kudumishwa. Kunapaswa

kuwa na uhuru wa kuzungumza ili kwamba wagombea walio wapinzani wa watawala waweze kutoa maoni yao. Pia kunapaswa kuwepo upigaji kura ya siri na tume huru ya uchaguzi ili kuhakikisha chaguzi zinafanyika kwa uwazi.

*Haki na maendeleo ya kiuchumi*

Utawala wa sheria ni muhimu kiuchumi na kijamii. Kila mwaka, Benki ya Dunia hutoa orodha ya nchi kwa vigezo vya urahisi wa kufanya nazo biashara. Kuvutia biashara na uwekezaji kutoka nje na kurahisisha watu kufanya biashara ya ndani ni moja ya sababu muhimu kwa ukuaji wa uchumi na ustawi wa watu. Orodha hiyo hutazama uwazi wa kanuni za kodi, viwango vya rushwa miongoni mwa maafisa na namna ilivyo rahisi watu kuanzisha biashara, kusajili mali, kufanya biashara ya kuvuka mipaka na kushughulikia madeni yasiyolipika na kadhalika.

Singapore, ambayo ni nchi huru sana kwa vigezo vya kiuchumi (japo si huru sana kijamii), imeongoza orodha hiyo duniani kwa miaka saba, ikifuatiwa na nchi nyingine huru kiasi kama Hong Kong, New Zealand, Denmark, Uingereza na Marekani. Zinazowafuatia ni Jamhuri ya Korea, nchi nyingine iliyo huru kiuchumi lakini isiyo huru kijamii. Chini kabisa katika orodha hiyo ni nchi ambako haki na utawala wa sheria uko chini sana – kama vile Kongo, Venezuela, Zimbabwe, Iraq, Bolivia na Uzbekistan.

*Vitisho kwa utawala wa sheria*

Katika nchi nyingi, hasa nchi zinazoendelea, kuna mifumo mingi ya utoaji haki. Zaidi ya mifumo ya sheria na utoaji haki ya kimataifa, mara nyingi huwa kuna mifumo ya eneo fulani, ya kikabila au ya kidini, pamoja na sheria binafsi au za mikataba baina ya watu.

Rushwa iko zaidi katika mifumo ya kitaifa. Mifumo ya mahali pamoja, ya kidini na sheria binafsi mara nyingi huwa na mizizi katika haki ya asili, na hivyo kuwa na ukubalikaji mpana zaidi. Kinyume chake, mifumo ya kitaifa huwa imeanzishwa na wakoloni na wakaliaji wa nchi za wengine. Zinaweza kuwa hazijawahi kukubalika sana, lakini nguvu yake inasalia kwa mtu yeyote mbadhirifu kuitumia.

Watu katika serikali na mahakama za kitaifa hawaoni ubaya wowote kutumia nguvu ya dola. Jeshi, polisi na maafisa wa serikali huchukua hongo. Wanasiasa hutegemewa kupora mali ya serikali ili kunufaisha wa kwao au hata wao wenyewe. Kinachoonekana kuwa kibaya katika maisha binafsi kinapaswa kuonekana hivyo mbele za watu wengine pia.

Katika maeneo ambako usafiri na mawasiliano ni magumu na masuala ya eneo hilo ni muhimu na ya haraka zaidi , matumizi ya mifumo mchanganyiko yanaleta maana. Lakini malengo yawe kwa mifumo yote hii ya usimamizi wa haki yawe na mamlaka ruksa ya sheria za eneo husika, kueleweka na kufuata kanuni za sheria za kitaifa na utawala wa sheria usiopendelea.

## Haki za binadamu

*Kufafanua maana ya haki za binadamu*

Kutoka katika akisi hiyo ya haki kunaibuka suala la haki za binadamu. Hili ni wazo kuwa watu wanastahili huru kadhaa za msingi kwa kuwa wao ni binadamu – haki ambazo, kama sheria ya asili, huchochea utendaji kazi bora wa jamii, lakini ni haki zinazokubalika ulimwenguni kote (kila sehemu na kwa kila mtu) na hazinyang'anyiki

(haziwezi kutolewa kwa mtu au kunyimwa na wengine).

‘Haki’ hizi huenda ikafaa zaidi kuitwa uhuru wa wanadamu. Huhusisha uhuru kama vile wa kumiliki mali, kujiamulia mambo yako na kujimilikia mwili na nguvukazi yako, uhuru wa kutembea na kuhamia mahali utakapo na uhuru wa kuabudu. Matokeo yake ni kuidhibiti serikali namna inavyoweza kuwatendea watu.

Balaa ni kuwa ‘haki za binadamu’ huchanganywa na haki za kisheria ambazo hutolewa kulingana na mfumo wa kisiasa au wa kijamii au wa kitamaduni. Lakini sheria zinazowapa wafanyakazi likizo za malipo kwa mfano, siyo haki za binadamu kwani siyo za mahali pote. Hufanya kazi kwa wafanyakazi pekee na kwa nchi ambako fahari kama hiyo ipo. Na huweza kupokonywa – mfanyakazi anaweza kuacha kwenda likizo kwa mbadala wa fedha, pasipo kupoteza uhuru wowote. Vivyo hivyo, sheria za malipo sawa kwa wanaume na wanawake siyo haki ya binadamu kwa kuwa hazina msingi wa uhuru wa binadamu, badala yake ni shurutisho kwa waajiri.

Haki za makundi pia si haki za binadamu. Hazitendi kazi ulimwenguni kote. kutendewa kwa aina fulani maalumu kwa mfano, kwa wakazi wenyeji wa Amerika ni marupurupu ya kisheria tu: watu wengine hawayafaidi. Kitu hakiwezi kuwa haki ya ‘binadamu’ ikiwa kimelenga kwa watu wa kundi fulani tu na siyo binadamu wote.

*Uhuru, haki na majukumu*

Ni muhimu kuwa wazi kwa masuala kama haya. Kuchanganya haki na mazoea ya kijamii na marupurupu ya kisheria hutoa mamlaka yasiyostahili kwa sheria na hivyo hufifisha wazo zima la haki za binadamu. Wakati

baadhi ya mambo – malipo sawa, likizo za malipo au hata kutambulika fulani maalumu kwa baadhi ya makundi – kunaweza kuwa kunahitajika, ukweli ni kuwa si kila kitu kinachopendelewa ni haki ya kibinadamu.

Haki za binadamu hutuhakikishia uhuru wetu – haziweki matakwa ya lazima kwa yeyote mwingine. Uhuru wa kuongea kwa mfano, hautoi ulazima wa kufanya jambo fulani kwa mtu yeyote zaidi ya ulazima au wajibu wa kuiheshimu tu. Hakuna anayelazimika kukupa nafasi katika gazeti au kipindi cha redio ili kuweza kutangaza mawazo yako, wala kukusaidia kuhakikisha unazungumza kwa uhuru, au hata kusikiliza nini unachokisema.

Kinyume chake, tangazo ya Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu limeorodhesha haki ya kupata elimu bure. Lakini elimu bure si haki ya binadamu kwa sababu inamaanisha watu wengine wanalazimika kukulipia. Utoaji elimu una gharama – muda, jitihada, vifaa na pesa huhitajika. Katika jamii huru hasa, hakuna anayeweza kuwa na haki ya kufurahia elimu bure kwa sababu italazimika watu wengine kuilipia. (Inawezekana watu wengi wakasukumwa kuchangia gharama, lakini katika jamii huria hakuna anayelazimishwa kufanya hivyo)

Mara nyingi, watu huongelea kuhusu haki pasipo kuzitaja, au hata kuzitambua, kuwa wengine wanalazimika kufanya kitu fulani, kusukuma watu wazitekeleze na madhara makubwa ambayo lazima hiyo hutokeza.

Tena, hakuna haki ya ustawi katika jamii huru: hiyo itamaanisha baadhi ya watu wanalazimika kuwasaidia wengine, wakati ulazima pekee ni kwa wao kutodhuru wengine. Lakini hii haina maana kuwa watu masikini au wasiojiweza wanadhurika zaidi kwenye utamaduni wa

ustawi. Gharama ya kodi inaweza kukatisha watu tama ya kufanya kazi na biashara, na hivyo kufanya watu wa jamii nzima masikini zaidi, na manufaa ya ustawi kuweza kuchochea utegemezi. Vyombo vya ufadhili katika jamii huria vinaweza kuwategemeza walio na uhitaji zaidi ya vyombo vya mamlaka za kiserikali vinavyoweza kufanya.

# 7 JAMII HURIA

## Utaratibu bila shuruti

Jamii huru inaweza kujiongoza pasipo kuhitaji dola kubwa. Inaweza kuonekana ya kushangaza, lakini maisha ya mwanadamu yamejawa na mifano. Kama ilivyo katika uchunguzi wa mchumi wa Marekani, Daniel B. Klein, unaweza kudhani kiwanja cha kutelezea kwenye barafu, chenye watu mia au zaidi, kuanzia watoto mpaka wazee, wakiwa na viatu vya matairi lakini pasipo kofia ngumu (helmeti), kinga za magoti wala ujuzi wa kuteleza kwenye barafu, wote wakiteleza kwenye sakafu ngumu kwa kasi tofauti tofauti – kutakuwa na mfululizo wa ajali zinazongoja kutokea. Lakini kiuhalisia, watelezaji huweza kuteleza uwanjani huku wakiwakwepa wengine bila kuhitaji vidhibiti kasi rasmi, wala alama za kuonyesha uelekeo au taa za kuamuru kusimama. Haihitaji afisa mipango au tume ya mipango kuwaambia wapi na kwa kasi gani wateleze. Kila mmoja akiwa anajisimamia na kuzingatia wengine kwa ukawaida tu, wote wanaifikia nia ya kupata furaha huku wakiepuka kugongana.

Na cha kuvutia zaidi, lugha ya kibinadamu imepangiliwa sana na ni ya manufaa sana kwetu, japo haijawahi kubuniwa kwa mipango ya mamlaka yoyote. Kanuni za sarufi zinazofanya lugha ifanye kazi zimekuwa kiasili kwa karne nyingi, kwa sababu zinatusaidia kuelewana.

Tunafuata kanuni hizi japo ni ngumu na zenye kutatiza kiasi cha kupata tabu kuziandika. Hakuna tume ya serikali ingeweza kutengeneza kanuni kama hizo zilivyo tata, ngumu na zenye kufaa. Zimejengeka kwa kitambo miongoni mwetu.

Sehemu nyingi za jamii ya watu hufanya kazi kwa namna hii. Bila kuhitaji kuambiwa namna ya kuenenda, tunajikuta tunaenenda kwa utaratibu, mazoea, kwa namna inayotabirika, kwa kufuata tu kanuni chache za msingi ambazo zimekua kama sehemu ya asili yetu. Kwa kuzifuata, tunatengeneza manufaa ya kutosha kwa kanuni za kijamii. Kanuni nyepesi zinazoturuhusu kufanya biashara kwa amani baina yetu, kwa mfano, zimetengeneza uchumi wa soko huria la kimataifa ambapo ulimwengu mzima unashirikiana.

*Jamii zinazoongozwa na kanuni*

Kanuni za baina ya watu katika jamii huru zinawapa watu uwanda zaidi kuliko wanayoweza kuwa nayo jamii wanayotawaliwa na serikali. Watu huru wanaweza kufanya mambo mengi ambayo hayajazuiliwa moja kwa moja, badala ya kutegemea ukomo wa yale ambayo serikali imeruhusu. Hii inamaanisha jamii huru zinaweza kuwa mnyambuliko zaidi na zenye uwezo wa kubadilika kulingana na mazingira na mahitaji badala ya kulazimika kusubiri maagizo.

Kanuni hizi – kama vile kanuni ya umiliki na mali katika uchumi wa soko – huambatanisha aina ya hekima iliyovumbuliwa kadri miaka ilivyoendelea, kuhusu kipi kinafanya kazi na kipi hakifanyi. Zinajirekebisha na kubadilika kadri mazingira na mahitaji yanavyobadilika, zikiakisi kujifunza kutokana na makosa kwa miaka

mingi na mamilioni ya maingiliano ya watu. Hujumuisha kanuni za kitabia za namna ya kuwatendea watu wengine, kanuni za kisheria zinazojaribu kuelezea sheria ya asili iliyoandikwa, na sheria ya kawaida ambayo imejengeka kwa majaribio mengi.

Jamii hii huria inayoongozwa na kanuni, siyo tu ni bunifu na yenye kubadilika kulingana na mazingira; lakini pia inaweza kuwa changamani kuliko ile inayoongozwa na serikali kuu. Kama ilivyo lugha, inaweza kuwa changamani sana kiasi kwa mba hakuna anayeweza kuelezea kanuni zake zote – lakini bado ikafanya kazi vizuri sana. Jamii inayotegemea maagizo ya mamlaka fulani lazima ina ukomo fulani, katika ukubwa na asili, kulingana na vile ambavyo wachache walioko mamlakani wanaweza kuvifikiria. Lakini jamii ambayo inategemea kanuni zilizojengeka kama matokeo ya mamilioni ya miingiliano wa watu kwa maelfu ya miaka hujumuisha hekima pana na yenye kina zaidi. Jamii zinazoongozwa na mamlaka kuu hutegemea hekima yenye ukomo ya wachache; jamii inayoongozwa na kanuni hujumuisha hekima za maelfu ya watu.

Hivyo, mara nyingi kosa linalofanywa na mamlaka za kiserikali ni kuwa, wanaweza kupangilia jamii au uchumi kwa namna nzuri zaidi na yenye maana zaidi kuliko kanuni za kila siku za muingiliano wa kijamiii na kiuchumi. kwa kupuuza na kubadili kanuni zilizopo kwenye jamii hii changamani, hufanya mambo kuwa mabaya zaidi.

*Ujuzi na mamlaka iliyosambaa*

Hekima ya asili ya jamii hiari, inayoongozwa kwa kanuni, haipatikani katika jamii nyingine zenye kusimamiwa. Hekima hiyo hushikwa na mamilioni ya watu kadri

wanavyoendelea na maisha yao ya kila siku. Kwa kuwa mamlaka yamesambaa, watu hao huweza kufanya majaribio yao madogo katika maisha yao wenyewe. Wanaweza kuchukua hatari zao na bahati zao wenyewe pasipo kuleta madhara kwa watu wengine. Lakini inapotokea uthubutu wao wa hatari ukafanikiwa, mafanikio yapo kwa ajili ya kila mmoja kuendeleza na kufaidika nao. Hii huchochea majaribio na mabadiliko kulingana na mazingira yanayobadilika, ikitoa jamii huria nafasi kubwa zaidi ya kufanikiwa katika ulimwengu wa mabadiliko. Mamlaka za kiserikali, kinyume na jamii huria, hufanya maamuzi kwa niaba ya kila mmoja, na hivyo kuhatarisha maisha na bahati ya kila mmoja. Hivyo hulazimika kuenenda bila mabadiliko sana – au wawe hatarini kufanya makosa makubwa sana. Na matokeo yake, jamii zisizo huru hubadilika taratibu zaidi na mara nyingi pasipo mafanikio.

Ni kweli kuwa jamii huria na uchumi huria haviwezi kuwa timilifu. Ni zao la matenda ya watu (japo siyo mpango wa mtu) na wanadamu hawako kamili. Hatuwezi kutabiri wakati ujao kwa mfano, na hivyo hufanya makosa katika majaribio yetu ya kuendana nao. Na taarifa ambazo kial mmoja wetu anazo si kamili na huwa za eneo tulilopo tu. Lakini katika ulimwengu wa maingiliano huru ya binadamu, taarifa hizi zisizo timilifu hupelekea jamii na uchumi ambao hubadilika inavyofaa kulingana na hali.

Katika jamii huru, watu hulazimika kujitafutia wenyewe namna ifaayo ya kuishi na wengine – ambao pia huwa katika kujaribu kuendana na matendo ya kila mmoja. Ni kama vile katika kituo che treni chenye shughuli nyingi wakati wa haraka ambapo kila mmoja anajaribu kufikia kati ya milango mingi ya kutokea, au kujaribu kuinga kupitia moja ya milango mingi na kujaribu kuifikia treni

yake hususa. Kila mmoja amejielekeza anakokwenda, japo safari yao inaweza isiwe kabisa ya moja kwa moja. Watalazimika kupita pita kati ya watu, ambao na wao wanajaribu kufanya kitu hicho hicho, wakibadili uelekeo kama wengine katika njia yao. Inaweza kuonekana kama vurugu, lakini kila mmoja hufika aendako pasipo mgogoro. Ikiwa mamlaka fulani ingelazimika kumwambia kila mmoja kati ya mamia au maelfu ya waliopo kwenye kituo wapi na muda gani wajongee, ingechukua masaa au siku kadhaa kila mtu kufika sehemu. Tatizo ni kubwa mno kutatuliwa kwa mfumo wa kati. Lakini jamii huria hulitatua kirahisi na kwa wakati huo huo.

## Uvumilivu

*Maana ya uvumilivu*

Kwa njia hii, watu katika jamii huru, kila mmoja anapaswa kuendana na matendo ya wengine. Hivyo ni muhimu kwamba watu wawe na uvumilivu kwa wenzao – ikiwa ni pamoja na matendo na mtindo wa maisha wasiokubaliana nao au unaowashtusha.

Katika jamii huru hatuwezi kumzuia mtu kufanya kitu kwa kuwa tu hatukipendi. Tunaweza tu kuingilia kati ikiwa matendo yake yanasababisha au yanaweza kupelekea madhara kwa wengine. John Stuart Mill alikuwa wazi kuwa hii ilimaanisha madhara ya kimwili. Kama 'madhara' yangejumuisha mambo kama mshtuko, fedheha kijamii au kudhalilishwa, basi kila kitu kingezuiliwa na kusingekuwa na uhuru kabisa. Kwa vyovyote vile, mwitikio wa nguvu wa waliotaka kuzuia taia fulani utafikia ule wa wale walionyimwa uhuru wa kufanya. Haijalishi wingi wala kiwango cha hisia ambazo kila upande utakuwa nazo, hakuna namna isiyo ya upendeleo ya kuamua kati yao. Na

kwa kuwa jamii huru hairuhusu migogoro kutatuliwa kwa nguvu, kila upande unahitaji tu kuvumulia mawazo, tabia na mitindo ya maisha ya wengine.

Hii hailingani na ilivyo kwenye kutojali maadili. Mzazi ambaye hakukemea tabia mbaya kwa mtoto hatakuwa akifanya kwa uvumilivu, atakuwa anapuuza elimu ya maadili ya mwanaye. Ikiwa watu wazima wanatabia tunazoona zinashtusha, tuna kila haki ya kusema hivyo na kujaribu kuwashawishi kuenenda vema – lakini si kuwalazimisha.

Pia uvumilivu si sawa na maadili ya uwiano – wazo la kwamba maadili ni sawia sehemu zote kwa kuwa watu hutofautiana kuhusu maadili na hakuna njia isiyo ya upendeleo ya kuamua baina yao. Tuna haki ya kuamini kuwa mfumo wetu wa maadili na wa kidini ni sawa zaidi ya wa wengine – lakini si kulazimisha mawazo yetu kwa mwingine yeyote.

*Uvumilivu, uanuai na chaguo*

Kuvumilia wengine inaweza kuwa vigumu wakati ambapo watu wanazidi kuwa tofauti. Urahisi wa usafiri wa kimataifa, kuanguka kwa vizuizi vya uhamiaji na uchumi wa kiutandawazi zaidi ni baadhi tu ya sababu za watu wa mataifa mbalimbali wako tofautitofauti kuliko walivyokuwa miongo michache iliyopita.

Baadhi ya watu hudai kuwa chaguo kubwa zaidi litapelekea makundi ya watu, tamaduni, mataifa, lugha na dini tofauti kutengana zaidi, kuwekeza wasiwasi unaoweza kudhuru uvumilivu. Kwa mfano, wazazi wanaweza kutaka watoto wao wakue na wenzao wa rangi inayofanana, na wanaweza kuwachagulia shule zao wenyewe na kupelekea nafasi

zaidi ya utengano kuliko ikiwa watoto wote wangekwenda shule moja iliyowekwa na serikali.

Kiuhalisia, shule zina nafasi ndogo zaidi ya kuwa jumuishi pale serikali inapotenga maeneo ya shule, kwani kawaida watoto huenda kwenye shule iliyo karibu nao zaidi. Na kwa kuwa ni kawaida kwa watu wenye asili inayofanana kuishi karibu karibu, walioko shuleni pia wataakisi ukosefu wa mchanganyiko huu. Lakini ikiwa wazazi wataweza kuchagua shule, wanaweza kuchagua shule za maeneo mengine, au nyingine ambazo huchagua kwa kigezo kingine wanachokithamini kuliko ukabila, kama vile taaluma, muziki na uwezo wa lugha.

Utengano wa kikabila ni wa kiasili kabisa, na watu huchagua rafiki zao na wenza wa kazi kutoka katika makundi yanayowiana. Ila kuna kila tofauti kati ya hilo na kutokuwa mvumilivu kwa jamii nyingine. Mgogoro mbaya zaidi wa kijamii huwa katika maeneo ambako baadhi ya makundi yamenyimwa haki na fursa kama wengine – kwa maneno mengine, pale ambapo kanuni msingi za jamii huru zinapovunjwa.

*Tishio la wenye msimamo mkali kwa uvumilivu*

Tishio kubwa zaidi kwa uvumilivu kwa wengine ni msimamo mkali wa kimaadili, kiitikadi na kidini. Wengi wenye misimamo mikali ya kidini, wanaweza kwa mfano, kuchukulia mapenzi ya jinsia moja au mahusiano ya kimapenzi kabla ya ndoa kuwa ya kuchukiza, ya aibu, ya kushtusha na yasiyofaa. Wanaweza kuchukulia vitu kama kufuru, kutengeneza sanamu za miungu, kukana maandiko ya kidini na kukataa kanuni za kimaadili za dini au kufuata dini nyingine kama dhambi kabisa. Hii pekee itaonekana kuwa sababu ya kutosha kwa tabia za aina hizo kupigwa marufuku kisheria na kuadhibiwa.

Lakini matendo ya mtu hata yawe ya kuchukiza au kushtusha kiasi gani kwa wengine, na hata yaonekane ni dhambi kiasi gani kwa misingi ya kidini, hakuna mwenye uwezo wa kuwazuia kwenye jamii huru, labda ikiwa inawadhuru wengine kimwili au inatishia kuwadhuru. Tena hii haizuii watu wa dini fulani kukosoa matendo haya au kuzungumza kinyume chake, au kuwatenga wayafanyayo kutoka kwenye jumuiya zao – ikiwa tu hilo halisababishi vitisho au madhara halisi kwa mtu. Lakini pia hairuhusu yeyote, ikiwemo serikali, kuwazuia, kuwadhibiti, kuwakamata, kuwafunga, kuwatesa, kuwajeruhi, kuwahamisha au kuwaua watu kwa msingi wa mtazamo huu na matendo haya.

Maandiko ya msingi ya dini nyingi ulimwenguni hukumbatia kuvumilia wengine, japo katika baadhi ya maeneo mamlaka zimeyatafsiri kivingine kwa maslahi yao binafsi. Dola za kigeni zilipotawala nchi fulani mara nyingi zilitawala na dini zao pia, wakibadili kanuni zake za maadili na kisheria ili kuwezesha tawala zao wenyewe. Baadhi ya serikali za kidikteta zimejaribu kuua kabisa dini, wakizichukulia kuwa ni shindani kwa itikadi na mamlaka yao. Lakini hili wala si jambo la kuzingatiwa katika jamii huru bila kujali msimamo mkali unaozungumziwa ni wa kidini au kiitikadi. Bado haitoi mamlaka ya kulazimisha wengine ambao matendo yao, maadili yao, dini na itikadi zao ni tofauti.

*Usahihi wa kisiasa*

Kuna kitisho kitatanishi kingine kwa uvumilivu: usahihi wa kisiasa. Hapa ndipo msukumo wa kijamii na kisiasa huwekwa kwa watu kukubali misimamo na maoni ya wasomi wanaotawala. Kwa ilivyozoeleka, wale wasiokubaliana nao huchukuliwa kama wana wazimu

au waovu. Hii hupelekea mawazo yao kupuuzwa badala ya kujadiliwa. Pia hujaribu kuonyesha kuwa maoni ya watawala ni thabiti kuliko vile yalivyo kiuhalisia.

Mchakato huu hutegemea mfumo wa kulazimisha kijanja, ambapo maoni tofauti hupakwa matope ili kwamba yasiweze kupata nafasi katika jamii. Kwa mfano, wanataaluma wanaohoji juu ya ushahidi wa mabadiliko ya tabia-nchi yanayosababishwa na shughuli za binadamu wanaweza kunyimwa fursa ya ajira au kupanda vyeo kwenye vyuo. Katika jamii huru, waajiri hawalazimiki kuajiri watu wanaotofautiana nao, wala vyombo vya habari havilazimiki kuripoti juu ya nadharia zenye utata. Lakini pale ambapo taasisi za elimu na vyombo vya habari vinapokuwa ni taasisi zinazomilikiwa na kuendeshwa na serikali, kutengwa huku kwa wachache wenye mawazo tofauti kunafikia kiwango cha ugandamizaji.

*Uvumulivu na utafutaji wa ukweli*

Uvumulivu katika jamii huru unakwenda mbali zaidi ya uvumilivu wa tofauti za kidini na kiitikadi. Kwa mfano, hujumuisha uhuru wa kujieleza – katika mazungumzo, maandishi, utangazaji au njia yoyote ile nyingine – ambayo huashiria kutokuwepo uthibiti.

Baadhi ya watu huweza kuona ulimwengu usio na udhibiti kuwa ni wa kutia shaka sana. Wengi watashtushwa sana na maneno, picha, mijadala na mawazo ambayo yanaweza kuibuka katika ulimwengu ulio huru sana. Lakini katika jamii huria hatuna haki ya kuzuia uhuru wa mawazo au kuzuia maoni ya watu hata ikiwa karibu wote hatukubaliani na kilichosemwa, au ikiwa tunaona kinakera au kuona si cha kimaadili.

Hata hivyo kuna udhibiti fulani kwenye uhuru wa kuongea ikiwa kitakachosemwa kitapelekea madhara kwa wengine, kama vile kupiga yowe la "moto" kwenye ukumbi. Tungemuadhibu mtu yeyote ambaye angepelekea hatari kwa wengine kwa namna kama hii. Kwa namna hiyohiyo, tunawalinda watoto wetu dhidi ya picha na maneno tunayoamini yatawaharibu. Tunaweza tusikubali matangazo ya wazi ya madawa kuwekwa, kwa mfano, kwenye mabango karibu na shule. Pia kunakuwa na umakini katika kuwapa watu taarifa – kama vile muhtasari wa filamu ili waisjikute wakikumbana na vitu ambavyo vinaweza kuwadhaisha.

Hii ni tofauti kabisa na udhibiti wa moja kwa maoja – kuzuia aina fulani za maneno, picha, mijadala na mawazo kutosikika kabisa. Hakuwezi kuwa na udhibiti wa aina hiyo kwenye jamii huria ya kweli, kwa sababu jamii huria imejengwa kwenye uwazi na chaguo. Watu wanapaswa kujua machaguo waliyonayo ikiwa watapaswa kuchagua kiuwiano na kujaribu mawazo mapya yanayoweza kuboresha maisha ya watu wote. Udhibiti huzuia machaguo na hivyo huzuia maendeleo.

Wala hatuwezi kuwaamini wadhibiti. Ukweli na mamlaka ni vitu viwili tofauti. Walioko mamlakani wana sababu zao wenyewe – kama vile kujilinda, kwa kuzuia usambazaji wa baadhi ya mawazo. Lakini hata ikiwa wadhibiti wamebeba maslahi ya umma mioyoni mwao, si kwamba wao ni timilifu. Hawana umuliki wa mwisho wa hekima, wala ujuzi maalumu wa kipi ni kweli na kipi si kweli. Ni mjadala tu, majadaliano na uzoefu vitabainisha hayo. Wadhibiti wanaweza kukandamiza ukweli kimakosa tu. Wanaweza kutokuwa na uhakika kuwa wanafinya mawazo ambayo hatimaye yatadhihirika kuwa sahihi. Mawazo mengine yanaweza kuwa makosa kwa kiwango kikubwa, lakini

yakawa na kiwango Fulani cha ukweli ndaniyake, ambapo ni mjadala tu unaweza kuyachambua. Ukweli wa baadhi ya mawazo hudhihirika baada ya muda Fulani kupita.

Njia ya kuhakikisha hatufinyi mawazo yanayoweza kuwa kweli na yenye kufaa ni kuyaruhusu yasemwe, kukiwa na uhakika kuwa uzuri na ubaya wake utadhihirika kupitia majadiliano. Hii inamaanisha kuwaruhusu watu kutetea mawazo yao, hata katika mambo ambayo wengi katika jamii wanaona uhakika wake tayari. Ukweli utaweza tu kuthibitishwa na ushindani kama huo. Ilikuwa kwa sababu hii kwamba Kanisa Katoliki kati ya mwaka 1587 mpaka 1983 lilikuwa likimteua 'wakili wa ibilisi' kujenga kesi dhidi ya mtu aliyependekezwa kwa ajili ya utakatifu. Ni muhimu kuweka wazi msukumo wetu wa kuhoji. Ikiwa tunaamini wengine wamekosea katika mawazo yao, mawazo hayo yachukuliwe na kupingwa, na si kunyamazishwa.

Kuanzia enzi za Socrates na kuendelea, historia imejaa mifano ya watu ambao wameshitakiwa kwa mtazamo wao. Mashtaka hayo mara nyingi yamepelekea wengi kunyamaza kimya, japokuwa mawazo yao hatimaye huthibitika. Kuhofia hasira ya Kanisa Katoliki, Nicholaus Copornicus hakuchapisha nadharia yake ya kimapinduzi iliyoelezea kuwa sayari huzunguka jua mpaka karibu na kifo chake mwaka 1543. Mwanafunzi wake Galileo Galilei alishitakiwa na kumalizia siku zake zilizosalia katika kifungo cha nyumbani.

Vitisho kam hivyo hugandamiza ukweli, majadiliano na maendeleo. Huidhuru jamii na wale wazushi wanaogandamizwa.

Ikiwa tunakubali tu mawazo yaliyopo pasipo mjadala wowote, mawazo hayo yamejengeka kwenye msingi dhaifu

sana usio salama. Kukubalika kwake si makini. Yanakuwa mambo ya mkumbo badala ya kweli zenye maana. Na pale mawazo mapya yanapofanikiwa kupata upenyo, inaweza kutokea kwa vurugu na mvurugano.

Inaweza kuwa na usumbufu pale watu wanaposema mambo ambayo kimsingi hatukubaliani nayo, wakielezea mawazo ambayo tunaamini si sahihi, wakifanya vitu tunavyoona ni vya kushtusha, au hata kupuuza imani za maadili na dini zetu. Lakini uvumilivu wetu kwa mambo kama haya unadhihirisha kujitolea kwetu kwa ajili ya uhuru na imani zetu kuwa tutafanya maendeleo zaidi na kuvumbua kweli mpya haraka zaidi, kwa kuruhusu mawazo tofauti kujadiliwa badala ya kugandamizwa.

*Makatazo*

Tutakuwa na hasira sana ikiwa vitu vingi tunavyovifurahia kwenye maisha yetu ya kila siku vitapigwa marufuku. Balaa ni kuwa vingi tayari vimepigwa marufuku.

Sheria ya kutosababisha madahara inasema hatuna haki ya kuzuia matendo isipokuwa yataleta madhara au yanaweza kuleta madhara kwa wengine. Lakini shughuli nyingi zimepigwa marufuku kwa madai kuwa zina madhara kwa wale wazifanyao. Hii ndiyo sababu kwa marufuku juu wa utumizi wa madawa ya kulevya, uvutaji sigara, unywaji pombe na kadhalika. Tatizo ni kuwa, sababu ya kuwaokoa watu wasijidhuru inaweza kusababisha karibu kila shughuli kuzuiwa. Ni rahisi kusema kuwa watu wanaweza kujiletea madhara kwa kunywa vinywaji vyenye sukari nyingi, kula vyakula vyenye mafuta sana, kufanya michezo ya hatari, kufanya ukahaba na mapenzi ya jinsia moja, kubadili dini na kuhoji mamlaka. Ikizingatiwa idadi ya watu wanaosema mambo haya, ikiwa kanuni hii

ikipotea, basi haitachukua muda mrefu kabla ya uhuru kuanza kugandamizwa.

Mazuio mara nyingi hupelekea madhara pia. Kwa kusukuma upatikanaji wa baadhi ya mahitaji kwa njia ya panya, hupelekea udhibiti wake kuwa mgumu zaidi na hata wahalifu hujitokeza na kuanza kusambaza bidhaa au huduma hizo. Marekani kwa mfano, bado inaathirika na uwepo wa magenge ya uhalifu ambayo nguvu yake imekua kutokana na marufuku kuwekwa miaka ya karne iliyopita, wakati usambazaji pombe ulipokuwa umepigwa marufuku. Kuendelezwa kwa marufuku ya kamari na ukahaba katika maeneo mengi ya Marekani kumepelekea muendelezo wa magenge hayo ya kihalifu ambayo yanafurahia kusambaza huduma ili kufidia uhitaji wa watu.

Mazuio pia hufanya iwe vigumu kwa watu kuelewa madhara ya tabia zao. Bado watu wanahitaji madawa ya kulevya, lakini ikiwa ni haramu, inakuwa vigumu kwao kupata taarifa za kiafya kuhusu madhara yake. Pia ni vigumu kwa watumiaji kujua ubora wa wanachokinunua. Inakuwa vigumu pia kwa waraibu wa madawa kutafuta msaada wa kitabibu au wa kijamii kwa sababu kwa kufanya hivyo ni kujidhihirishia uhalifu wao. Na watu wanajikuta wakijiweka katika hatari nyingine, kama vile kupata maambukizi ya VVU kutokana na sindano zisizo salama, kwa sababu uharamu wa madawa ya kulevya unawapa ugumu kuwapleka katika mahali salama. Matokeo yake ni kuwa madhara mengi yatokanayo na madawa hayo ni kwa sababu ya kupigwa kwakwe marufuku kisheria.

Marufuku kama hizi huwaharamisha watu ambao si wahalifu ambao hawaoni madhara ya kutumia madawa ya kujiburudisha, au kucheza kamari au kunywa pombe nyumbani na marafiki, ambapo hakuna kati ya hivyo

kinachosababisha madhara kwa watu wengine kabisa. Na wakiwa wameidharau sheria kwa makosa ya kipuuzi, wanaweza kujiweka katika hatari ya mambo makubwa yenye madhara zaidi.

Mazuio/marufuku ni kama huwa hazisaidii kabisa. Kuzuiwa kwa vileo nchini Marekani kulichochea unywaji wa kichini chini ambao hauwezi tena kudhibitiwa. Sheria kali za madawa na hukumu kubwa dhidi ya biashara ya madawa ulimwenguni hazijasaidia kukomesha biashara inayokadiriwa kuwa na thamani ya mabilioni ya dola.

**Swali: Hatuhitajiki kuwalinda watu dhidi yao wenyewe?**

Hapana. Unahitaji 'kulindwa' dhidi yako mwenyewe? Au unadhani unapaswa kufanya maamuzi yako namna gani unaishi maisha yako? Kuruhusu serikali kutuamulia nini ni kizuri au kibaya kwa jaili yetu haitoshi: tuko katika nafasi nzuri zaidi ya maafisa walioko mbali wanaotuamulia hatari zipi tunazikabili. Na ni hatari, serikali inaweza kuanza kwa kuzuia vitu ambavyo sote tunakubali kuwa vina madhara, lakini kanuni ikishakubalika, wanaweza kupiga marufuku kila kitu.

Je, tuzuiwe kuvuta kokeini, sigara, kunywa pombe, kula vyakula vyenye mafuta au kugida vinywaji nyenye sukari? Je, tulazimishwe na sheria kufanya mazoezi, kuacha michezo ya hatari na kuhudhuria kanisani? Je, tuzuiwe kusoma vitabu hatarishi au kuwakosoa watawala wetu? Jibu katika jamii huru ni *hapana.* Ikiwa watu wanakiuka maadili yetu au kufanya kitu hatari, tuwaambie hivyo. Lakini ikiwa tu hawamdhuru mwingine yeyote, hatuna haki ya kuwazuia.

Kujaribu kuondosha tabia ya kawaida ni kupoteza wakati. Na ni kuhatarisha uhuru kwa sababu kutahitajika usimamizi mkubwa sana ili kufanya kuleta matokeo.

Hii itaondosha rasilimali za usimamizi wa sheria kutoka kwenye kuchunguza na kuendesha mashtaka ya makosa yenye madhara kuelekea mambo haya. Pia itafungua milango kwa rushwa miongoni mwa polisi na mahakama; japokuwa kamari na kuraibu madawa kunaweza kuleta madhara kidogo au kutoleta madhara kabisa kwa wengine, adhabu zinaweza kuwa kubwa, hivyo kuwawezesha maafisa wa serikali kuchukua viwango vikubwa vya rushwa kutoka kwa wahusika.

*Tabia za umma na binafsi*

Kanuni za jamii huru zinaongoza tabia ya pamoja/umma – namna gani watu wanafanya kwa wengine. Lakini tabia binafsi – inayoleta matokeo kwa mtu anayehusika tu – inasalia katika maisha binafsi. Inakuwa jambo la kisheria ikiwa tu inaleta madhara kwa wengine.

Hata hivyo, kwenye jamii huru ni muhimu kuwa makini kutambua kuwa madhara au hatari ya madhara kutokea ni halisi. Je, watu waruhusiwe kuuza sumu? Ikichukuliwa kuwa sumu ina matumizi mengi mengine ambayo hayahusishi kuwadhuru binadamu, madhara makubwa zaidi yanaweza kusababishwa kwa upigaji marufuku uuzaji wa sumu kuliko kuruhusu. Pia kunaweza kuwa na rekodi ya wauzaji nawanunuzi wa sumu ili wajue kuwa kuna nafasi ya kujulikana, na si zaidi ya hapo.

Je, kunapaswa kuwa na kanuni dhidi ya ulevi wa hadharani? Au dhidi ya uendeshaji wa madaguro na nyumba za kamari? Ndiyo, ikiwa zinasababisha vurugu, ndiyo maana nchi nyingi zinachagua kuzipa kibali. Lakini kwa kiwango kikubwa, shughuli hizi huathiri wahusika tu. Watu wengine kukerwa kwa kuzifikiria, lakini ikiwa tutaruhusu shughuli hizi kupigwa marufuku kwa sababu

tu zinasababisha madhara binafsi kwa watu fulani, hakuna shughuli ya binadamu iliyo salama dhidi ya wanamaadili.

Je, watu warehusiwe kufanya biashara siku takatifu? Au waoe wake wengi? Ni kazi kwao wenyewe, wala haituhusu, haimdhuru mwingine yeyote. Sheria katika jamii huria zipo ili kulinda na kupanua uhuru wa watu, na si kulazimisha maadili ya watu fulani kwa wengine.

Hata hivyo, katika jamii huru, watu wanaruhusiwa kuweka sheria kwenye mali zao wenyewe, kwa kuzingatia tu kwamba kanuni ya kutodhuru wengine imezingatiwa. Katika nchi nyingi, baadhi ya maeneo ya umma (kama maduka makubwa) yanamilikiwa kibinafsi badala ya kutawaliwa na mamlaka za kisiasa. Hivyo, mwaka 2005, kituo cha manunuzi Bluewater kilichopo kusini mashariki mwa jiji la London kilipiga marufuku matusi, uvutaji sigara, kusambaza vipeperushi na kuvaa mavazi yanayozuia uso. Na mjiji Bournville, katikati mwa Uingereza – mji wa kiwanda uliojengwa na mtengenezaji choklet, George Cadbury ambao unaendeshwa na wadhamini binafsi ambao hushikilia kanuni zake – uuzaji wa wazi wa vileo ni marefuku. Kwa kuwa Bluewater na Bournville ni milki binafsi, wako ndani ya haki zao.

## Tatizo la uungwana

Watu wengi wana hofu ya wazo la kuwa jamii huru na uchumi huria huendeshwa kwa misingi ya manufaa binafsi ya wahusika. Wangependa badala yake, ulimwengu ambao unaongozwa na uungwana – kujali ustawi na maslahi ya wengine bila ubinafsi. Lakini hii hupelekea matatizo kuliko inavyoyatatua.

*Hakuna mwongozo wa kuwasaidia wengine*

Kivipi kwa kuanzia, tunaweza kujua kipi ni maslahi ya watu wengine? Hatuna uwezo wa kuona moja kwa moja akilini mwao au maadili yao. Ikiwa tungejaribu kufanya mambo kwa maslahi yao tungekuwa tukifanya makosa makubwa sana. Yeyote aliyewahi kupata zawadi isiyofaa zaidi ya sikukuu ya kuzaliwa anaweza kujua kiasi gani hata familia na marafiki wanaweza wasiwe na utambuzi mzuri wa kitu mtu anapendelea. Utamaduni wa utoaji unaonekana si msingi wa kujitosheleza wa kuendesha jamii nzima.

Ni vigumu pia kukosoa vitu wengine wanatupatia. Tunakubali zawadi kwa shukrani hata kutoka kwa watu tunaowachukia. Hii ina maana kuwa watu katika jamii ya kiungwana hawataweza kamwe kujua nini haswa watu wengine wanataka. Hiyo ni tofauti kabisa na uchumi uliojengwa kwenye misingi ya maslahi binafsi, ambapo wateja wasipopata wanachokitaka kutoka kwa muuzaji, wanasema hivyo na hutishia kupeleka biashara zao kwingine. Maslahi binafsi huwaelekeza wasambazaji kuwauzia watu vile vitu ambavyo wanavitaka hasa na kwa bei chee kadri iwezekanavyo.

*Uungwana huzalisha mgogoro*

Ikiwa kujaribu kuwasaidia wengine ndiyo msukumo wa michakato ya kibiashara, kungekuwa na mgogoro baina ya wauzaji na wanunuzi kama ambavyo iko leo katika ulimwengu wa maslahi binafsi. Wanunuzi wangetaka bei juu zaidi kuwanufaisha wauzaji, na wauzaji wangeuza kwa bei chee kabisa ili kuwanufaisha wanunuzi. Ni taswira ya kinachotokea leo.

Kwenye uchumi wa soko, watu wenye maslahi binafsi hugombana wenyewe, lakini huweza kutatua mgogoro wao kwa kujadiliana. Ikiwa msukumo pekee ni katika kunufaisha wengine, kusingekuwa na njia ya kutatua migogoro. Kila muungwana angesisitiza kumnufaisha mwingine. Na kwa kuwa hakuna anayetaka kunufaika, umuhimu wa mahitaji yao wenyewe usingewasaidia kukubaliana.

*Maslahi binafsi na gharama na faida*

Maslahi binafsi hutazama wauzaji na wateja pia – katika kuhakikisha manufaa ya muamala yanazidi gharama. Muuzaji muungwana ambaye amefanya kazi pasipo faida yoyote atatoa ishara ya kupotosha kwa kila mmoja – ishara kwamba muda na utaalamu wao ulikuwa hauna gharama. Wateja kwa kuchukulia ishara hii ya upotoshaji, ndani ya muda mfupi watawaelemea wasambazaji kwa mahitaji yao. Wauzaji hawatakuwa na namna ya kukataa kutoa huduma, hata ikiwa faida yake ni ndogo kutokana na kuzidiwa na gharama.

Mafundi ngozi kwa mfano, wangekuwa na misururu isiyokwisha ya watu wenye bidhaa za kufanyiwa marekebisho. Katika uchumi wa soko wa maslahi binafsi, wafanyabiashara hao wangewaambia wateja kuwa vifaa vyao havina thamani ya kurekebishwa tena, au wangetaja bei ya juu kiasi cha wateja kuamua kutojisumbua. Soko linaongoza uhitaji na huelekeza juhudi katika kile chenye thamani ya kweli.

Katika ulimwengu wa kiungwana, watu wangekuwa wakikimbilia kuwasaidia jirani zao kaatika kila aina ya kazi – kujenga nyumba kwa mfano. Lakini katika namna ya kujali gharama, ingekuwa vema kwa jirani huyo kwenda

sokoni na kuajiri fundi mwashi mjuzi badala ya kutegemea majirani zake wasio na ujuzi. Hasara ingefunikwa ikiwa majirani hao wangetumia vipaji vyao vema zaidi katika anina nyingine ya kazi. Soko huhamasisha watu kutumia muda na ujuzi wao katika vitu vilivyo na thamani zaidi.

**Swali: Je, tudhibiti bei ili masikini waweze kumudu vitu?**

Hapana. Bei ni ishara ya uhaba. Hutuambia wapi kuna ziada na wapi kuna nakisi. Huwaambia wazalishaji kiasi kikubwa zaidi cha bidhaa kinahitajika, na watumiaji wapunguze utumiaji au watafute mbadala. Udhibiti bei hufinya ishara hizi na uhitaji huzidi usambazaji na kutokeza nakisi. Hii hatimaye hupelekea mgawo wa bidhaa adimu kitu ambacho hakina ufanisi zaidi.

Mfano ni udhibiti wa kodi ya pango uliolenga kufanya makazi kuwa ya kumudu. Walichokifanya ni kufanya makazi kuwa hovyo zaidi na hata kuto[atikana, kwa sababu wamiliki waliamua kuwa kodi hizo hazina thamani ya uwekezaji kwao wakaamua kuondosha mali zao kwenye soko. Ikiwa kuna wasiomudu mahitaji, njia bora zaidi ya kuingilia kati si kuuingilia mfumo wa soko, bali kuwapa fedha – ama kupitia wafadhili au kupitia mipango ya bei ndogo iliyofadhiliwa kwa kodi. Wanweza kununua vitu hivyo katika soko hilihilo shindani na lenye ufanisi kama wengine.

*Maadili ya sokoni*

Ukweli kwamba uchumi wa soko huria umejengwa katika maslahi binafsi haumaanishi kuwa hauna maadili. Katika masoko, watu wanaweza tu kustawi kwa kushirikiana na wengine kusambaza vitu wanavyovihitaji. Tabia ya kujitenga huadhibiwa: kwa nini mtu afanye biashara na mwenye chuki dhidi ya wengine ikiwa kuna watu wengine walio tayari kufanya nae biashara?

Pia kuna kanuni zinazofanya masoko kufanya kazi pasipo shuruti. Lakini sheria fulani mahsusi haziwezi kufanya kazi katika kila aina ya jambo linaloibuka. Masoko hutegemea kuaminiana, na huwafaidia wenye sifa ya kuwa waaminifu na wenye kutegemeka. Hata japo msukumo wake ni maslahi binafsi, mfumo wa soko huchochea maadili ya kuthamini maslahi ya wote.

*Jukumu la shirika kwa jamii*

Watu wengi wanataka biashara kufanya kazi kwa maadili zaidi, na kuchochea wajibu wao kwa jamii. Makampuni mengi makubwa ya kimataifa huchapisha taarifa zao za mwaka wakielezea nini wanafanya kuwa raia wema.

Lakini ni watu pekee wanaweza kuwajibika au kutowajibika, kimaadili au la. Makundi hayana maadili yake yenyewe. Nchi, mji, kabila, watu wa rangi fulani, klabu au kampuni haiwezi kuwa yenye maadili au la – ni kila mmoja kati ya watu wanaoiunda. Kiukweli tutahitaji viongozi wa kibiashara kujenga utamaduni wa uadilifu katika mashirika yao. Lakini uadilifu na wajibu huonekana katika matendo – na matendo hufanywa na watu na si makundi.

Wajibu wa shirika kwa jamii ni jitihada za kupeleka gharama za program za kijami na ustawi kwenye biashara. Biashara hujaribu kuonyesha jinsi walivyowajibika kwa kudhamini shule zinazowazunguka, makundi ya kijamii na kadhalika. Inaweza kuleta mantiki nzuri kibiashara kwao kwa kufanya hivi: ikizingatiwa watahitaji kuajiri kutoka kwa shule zinazowazunguka, hivyo kujenga uhusiano mzuri nao utafanya mchakato wa kuwaajiri kuwa rahisi. Lakini hii inapaswa kuwa uamuzi wa kibiashara uliofanywa kwa hiyari na viongozi na wenye hisa, si kwa kulazimishwa kwa kisingizio cha maadili.

Ikiwa biashara zingekuwa shindani haswa, kusingekuwa na fedha za ziada kudhamini miradi ambayo haileti faida kibiashara. Ikiwa makampuni yana pesa za kutumia kwenye miradi kama hiyo, hii ni ishara kuwa mfumo wa soko haufanyi kazi (kwa mfano, sheria ya serikali inayozuia makampuni kushindana). Katika soko la ushindani halisi, makampuni hayo yangepoteza nafasi kwa wengine waliopuuza kudhamini miradi ya wenyeji na kupata faida ya ziada.

Pia si kwamba wafanyabiashara wako vizuri katika kuhakikisha pesa wanayodhamini inatumika ipasavyo. Wangeshauriwa vyema zaidi kujielekeza kwenye suala lao la msingi, kutengeneza faida kwa kutoa bidhaa na huduma ambazo watu wanazihitaji – ambavyo mwishowe vitazalisha utajiri utakaowawezesha kuwa wafadhili wanaojimudu.

# 8 UBINAFSISHAJI NA UTANDAWAZI

## Uhamiaji na teknolojia

Sehemu zilizokuwa za pembezoni mwa dunia sasa si za pembezoni tena. Televisheni, redio, mtandao wa intaneti na njia nyingine za mawasiliano zinaleta tamaduni nyingine, mtindo mwingine wa maisha, mbari nyingine, watu na mifumo mingine ya utawalam karibu nasi. Usafiri wa anga na usafiri wa kasi wan chi kavu unafanya kuwa rahisi kutembelea maeneo mengi zaidi moja kwa moja.

Hii imefanya kuwa vigumu zaidi kwa serikali kuficha maovu yake. Hakuna haja tena ya serikali kujenga uzio kuzunguka mipaka yake kwa tumaini kuwa itawaficha wananchi wake mapungufu yake. Shukrani kwa mawasiliano ya kila siku na maeneo mengine ya dunia kupitia mitandao ya kijamii au vituo vya televisheni vya kigeni kupitia satelaiti, wananchi hao huenda tayari wanafahamu kuhusu fursa adhimu mahali pengine.

Matokeo yake, nchi nyingi zimeachana na majaribio yao ya kujitenga na wengine duniani. Sasa wanafunguka kuruhusu watalii na wageni wengine. Miongo michache iliyopita, nchi kubwa kama Urusi, China, Vietnam, Burma (Myanmar) na nyinginezo zimekuwa wanachama wawazi zaidi wa jumuiya ya kimataifa. Leo, takribani moja ya tano

ya Waafghani wameishi ughaibuni kwa kipindi fulani cha maisha yao.

*Kubadilishana mawazo*

Siyo watu pekee wanaosafiri katika ulimwengu huu mpya – mawazo pia huambatana nao. Watalii huja na habari za ulimwengu tofauti, ambako watu wako huru kutenda, kufikiri na kuongea. Wenyeji huenda ughaibuni na kushangazwa kuwa hadithi za watalii hao ni za kweli. Ikiwa watu wanaweza kuona mitandaoni au kwenye televisheni, wanathibitisha walichokisikia kwa wanachokiona kwenye televisheni.

Biashara pia ina matokeo kama hayo. Pale nchi inapofungua mipaka kwa biashara za kimataifa, raia wake wanajikuta wakifanya biashara, wanakuwa marafiki na watu wa tamaduni tofauti, na kasha kujua mitindo yao ya maisha.

Hii huongeza msukumo kwa serikali kufunguka zaidi. Watu wanaojionea na kushuhudia uhuru moja kwa moja wanaelewa nguvu yake katika kuchochea maendeleo na kuendeleza ustawi. Wanahitaji sehemu ya maendeleo na ustawi huo kwa ajili yao pia. Teknolojia, biashara, uhamiaji, utalii na masoko ya kimataifa, vyote ni mabalozi wa jamii huria.

## Kukuza jamii huria

*Si ubepari wa kutokea juu*

Kuunda jamii huria ambako haijwahi kuwepo kabla si kazi rahisi. Serikali mpya na mashirika ya misaada ya kimataifa mara nyingi hutaka mabadiliko makubwa ya

maana, kama vile kubadili kabisa tabaka la utawala, au kubinafsisha viwanda vinavyoendeshwa na serikali.

Mara nyingi njia hii huwa ni balaa. Wakati utamaduni wa kutumia mamlaka kwa maslahi binafsi ungalipo bado, na pasipo uelewa wa wenyeji kuhusu masoko na ushindani, michakato mingi ya ubinafsishaji (kama Mexico mwishoni mwa miaka ya 1980) huwa tu ni uhamishaji wa makampuni ya serikali kwenda mikono ya marafiki wachache. Kwa wananchi, ubepari huu wa kirafiki hauonekani kuwa tofauti na mfumo wa kupendeleana kirafiki wa serikali uliokuwepo kabla. Na kwa kuwa kurekebisha mifumo ya kimahakama inaweza kuchukua iongo kadhaa, kupendeleana huko kunaweza kuendelea pasipo hatua yoyote ya mahakama dhidi yake. Hivyo, watu wanajikuta na mashaka na suluhisho linaloletwa na mfumo wa biashara huria kama walivyotatizika na mfumo wa uendeshaji chini ya serikali. Hivyo wengi wanajikuta wakishawishika kuwa wenye itikadi kali na wanamapinduzi pekee ndiyo wanaweza kutoa njia mbadala inayoweza kuwafaa watu wote badala ya la watawala wachache.

*Kuanzia chini huchochea uhuru*

Ubepari wa kuanzia juu hushindwa kwa sababu hujaribu kubadili mwonekano wa taasisi za kijamii pasipo kubadili misingi ya mitazamo, matendo na vichocheo vinavyoziwezesha.

Ubunifu na maendeleo ya jamii huru hukua kutoka katika mfumo wa kanuni za kisheria na kimaadili ambazo huonyesha namna watu wanaishi na kushirikiana kwa uhuru. Ikiwa tunaweza kuuanzisha mfumo kama huo wa kanuni za matendo, na kuwaacha huru kuendesha maisha yao ndani ya kanuni hizo, nishati ya asili na msukumo wa jamii yote utapelekea mabadiliko ya kimfumo.

Chukulia kwa mfano, kwamba tunafanya kuwa rahisi kwa watu kuanzisha biashara mpya, kumiliki na kuendesha biashara kwa kujiamini, kuwa na uhakika wa umiliki wa mali, kujenga mtaji wa uzalishaji na kufanya biashara kwa uhuru. Kwa kufanya hivi, tunatengeneza kanuni na vichocheo ambavyo kwa muda mfupi vitaleta ukuaji wa kiuchumi na kuchochea mabadiliko ya mfumo wa kijamii. Watu wataanzisha biashara ndogo, watajifunza namna biashara hufanywa, na kukua – wakipata faida sit u za kifedha, lakini pia kujiamini zaidi. Jamii inayojiamini zaidi itakuwa na uwezo zaidi wa kutatua matatizo makubwa zaidi ya kitaasisi kama vile kubadili mfumo wa utawala wa umma na taasisi za serikali.

Hivyo, hatupaswi kuanzia ngazi ya juu kujaribu kurekebisha taasisi zote za serikali. Tunapaswa kuanzia ngazi za chini kwa kufungulia vichocheo ambavyo vitapelekea mabadiliko ya mfumo wote wa kitaasisi.

## Haki za umiliki mali zikiwa kazini

*Haki za umiliki mali - Peru*

Mfano wa kuvutia wa mabadiliko ya haki za umiliki mali nchini Peru, kwa kiwango kikubwa zikiwa zimechochewa na mchumi Hernando de Soto mwanzoni mwa miaka ya 1990. De Soto alilalamika kuwa kwa sababu ya urasimu na rushwa nchini Peru, inaweza kuchukua mwaka mzima kusajili biashara mpya. Ilikuwa pia ngumu vivyo hivyo kumuliki mali. Matokeo yake ni kuwa, mamilioni ya wajasiriamali wadogo hawakuwa wakimiliki mashamba, biashara ndogo na nyumba zao kisheria. Hii ikafanya kuwa vigumu kwao kupata mikopo ya kupanua shughuli zao. Hawakuweza kuuza nyumba au biashara zao. Na

hawakuweza kutumia mahakama kutatua migogoro ya mali na biashara.

Kulikuwa na uchumi wa aina mbili katika nchi ya Peru, mmoja ukiendana na sheria na kufurahia manufaa yote ya uhalali na ulinzi wa kisheria, na mwingine ukijumuisha mamilioni ya wajasiriamali walionaswa kwenye lindi la umasikini kwa kuwa nyumba na biashara zao hazipo kisheria. Serikali ilipoteza mapato kwa sababu haikuweza kutathmini au kukusanya kodi kutoka kwa biashara hizi ndogo zisizokuwepo kisheria. Na bila kuwepo ulinzi wa kisheria, wajasiriamali hawa walijikuta katika nafasi ya kuhujumiwa kirahisi na wahalifu na wapiganaji wa kikomunisti, *Shining Path*.

Utatuzi ambao De Soto na wengine waliuleta ni kuondosha urasimu mwingi katika kusajili biashara mpya, na kuondoa leseni na vibali vingi ambavyo ilimpasa mtu kuwa navyo ili kuendesha biashara. Kulikuwa pia na marekebisho ya umilikaji ardhi ambapo kwa mara ya kwanza kabisa, zaidi ya familia milioni za Waperu zilipata vibali vya ardhi vinavyotambulika. Matokeo yake, ufanisi wa biashara ukaongezeka, kwa sababu wamiliki walipata uwezo wa kukopa ili kutanua biashara zao na kununua na kuuza mali. Kadri watu walivyopata mtaji na akiba, viwango vya makazi vikaimarika na wazazi wakaanza kutumia fedha zaidi katika kuwaelimisha watoto wao.

Mabadiliko hayakuja pasipo kukosolewa. Baadhi ya watu walilalamika kuwa utoaji vibali haukuwa wa usawa kwa sababu ilikuwa vigumu kuonyesha nani alimiliki nini. Na wengine wakalalamika kuwa utoaji vibali vya ardhi uliwanufaisha wamiliki wakubwa kuliko wadogo; kwamba vibali vilifanya ardhi ya wote ambayo masikini waliitegemea kuchukuliwa na wachache; au kwamba

mchakato huo ulivuruga makubaliano ya pango – ambayo japo si rasmi – yalifanya kazi vizuri. Wengine wakasema kuwa mabadiliko ya umiliki ardhi hayakuwa na thamani ya mageuzi iliyotegemewa, na kwamba kikwazo kikubwa zaidi cha maendeleo ya kiuchumi kilikuwa vikwazo ambavyo utamaduni wa watu umeweka kwenye matamanio yao.

Si rahisi kuanzisha mfumo wa soko unaofanya kazi vema mahali ambako haujawahi kuwako kabla. Ni rahisi kutengeneza supu ya samaki kutoka kwenye tangisamaki lakini si rahisi kutengeneza tangisamaki kutoka kwenye supu ya samaki. Hata hivyo, nchi nyingine zimejaribu kuiga mageuzi ya Peru, na De Soto mwenyewe amezishauri nyingi kati yake, kote, Amerika ya Kusini na Afrika.

*Kuunga mkono mageuzi*

Japokuwa uwepo wa haki za umiliki mali zinazofanya kazi vema ni muhimu, mageuzi mengine ya kuunga mkono pia yanahitajika. Kwa mfano, kunahitajika kuwepo soko la amana na amana ndogondogo linalofanya kazi vema, ambapo miongozo na urasimu mwingi vinaweza kuvitatiza kirahisi. (Mfano wa kuvutia wa amana ndogondogo ni Benki ya Grameen ya Bangladesh, ambayo hutoa mikopo midogo kwa biashara za vijijini – pamoja na mikopo ambayo wanawake wajasiriamali wasiokuwa na ardhi wanweza kuanzisha mfumo wa huduma ya simu ya kulipia kwa kutumia simu za mkononi.)

Kunahitajika kuwepo mfumo wa kisheria ulio fanisi na wa kuaminika, ili kwamba watu waweze kutatua migogoro yao kwa haraka na kwa kujiamini. Hatuhitaji kungoja mpaka watunga sheria wafikirie na kupitisha mageuzi fulani kwenye mfumo wa kisheria wa taifa. Sheria ya

pamoja, iliyojengwa kwa sauala moja moja, ni ya haraka zaidi na kunaweza kuwepo mfumo wa kisheria wa wenyeji uliopo tayari na chombo cha urejezi kinachokubaliana na mtazamo wa watu wa hapo kuhusu haki. Lakini tunapaswa kuweka kanuni msingi za biashara kufanyika, kama vile mifumo ya umiliki, dhima, haki ya wanahisa na mipangilio ya ufilisi.

Tunahitaji kupunguza miongozo inayozuia kuingia katika soko ili kwamba mawazo mapya yaweze kuibuka. Kwa mfano, watawala wa Nepal, nchi ilikuwa imejitenga sana na ulimwengu mwingine kabla ya miaka ya 1950, walikataa kabisa wazo la kuuza mfumo wao wa simu kwa madai kuwa watu watatishika watakapojua kuwa kampuni binafsi ndiyo inauendesha. Lakini walikubali wazo la vibali kwa makampuni mapya kuingia. Makampuni haya mapya yamefanikiwa sana kiasi kwamba sasa hivi Nepal ina mfumo wa simu wa kisasa unoonewa wivu. Kadri kunapokuwa na mifano zaidi ya biashara ndogo na waingiaji wapya sokoni, wakibuni ajira, kuongeza ustawi na kuboresha huduma kwa wateja, ndivyo inaongeza uwezekano wa watu zaidi kuelewa manufaa ambayo yanaweza kupatikana kwa uhru wa kubuni chanzo cha kipato na utajiri. Inapoungwa mkono zaidi, ndivyo watu wataacha kuhitaji njia mbadala zilizo gandamizi na kali.

*Mageuzi ya kilimo*

Mifano ya nguvu ya utendaji kazi wa haki za umiliki ni mageuzi ya kilimo katika Jamhuri ya Kisovieti ya Urusi, China na Vietnam. Serikali zao za kikomunisti zilijenga kilimo katika umiliki wa pamoja wa ardhi na wa miradi ya mashamba. Jumuiya zilikuwa na haki ya kutumia na kufanyia kazi ardhi na kuanzisha mfumo wa mgawo wa usawa. Ilikuwa ni balaa. Jumuiya zilkuwa nyingi mno,

zisizotawalika na zenye urasimu mwingi. Na kwa kuwa watu walipaswa kugawana matunda ya juhudi zao na wengine, walikuwa na kichocheo hafifu cha kufanya kazi kwa bidii na ufanisi zaidi.

Japo ilikuwa yenye kusitasita kuuacha mfumo huu wa kijamaa, China iliachana na mfumo huu wa kisovieti mwishoni mwa miaka ya 1970. Mfumo wa wajibu wa kila nyumba ukaingia, ambapo kila familia ilifanyia kazi kipande chao cha ardhi. Hii ikarejesha muunganiko kati ya jitihada na thawabu. Kilimo cha China kikakua. Uzalishaji wa mashamba mwanzoni mwa 1980 ukaongezeka kwa kasi, kukiwa na ongezeko la karibu asilimia 5 kwa mwaka kwenye mazao ya nafaka na asilimia 8 kwa kahawa na 14 kwa ufuta.

Lakini mafanikio haya ya mapema hayakudumu. Mfumo bado ulikuwa na kasoro. Ili kujaribu kusawazisha tofauti ya ubora wa ardhi, mamlaka ziligawia familia vipande vidogo tofauti vya ardhi badala ya kikubwa kimoja. Kwa kuwa jitihada za familia zilipaswa kutawanyika katika vipande vitano mpaka sita vya ardhi, ilikuwa vigumu kutumia mbinu bora zaidi za kilimo. Hata njia baina ya vipande vya mashamba vilichukua nafasi kubwa ya mashamba yaliyolimwa. Na mfumo wa ugawaji haukuzingatia utofauti wa uwezo wa uzalishaji wa kila familia.

Hivyo, ikaamuliwa kuacha mfumo wa umiliki wa ardhi pasipo kubadilishwa, isipokuwa kuanzisha mfumo wa matumizi ya haki – kuzipa familia haki za muda mrefu zaidi za kufanyia kazi mashamba yao, kupata mazao na kipato, na kuhamisha haki hizo kwenda kwa wengine.

Bado mfumo huu pia haukuwa sawa kwa mtazamo wa soko huria au haki ya umiliki. Mifumo ya manunuzi

na kupanga bei ya serikali iliminya uwezo wa wakulima kufanya maamuzi yao wenyewe na kufurahia matunda ya kazi yao wenyewe. Bila kuwepo soko halisi katika ardhi, bado kulikuwa uunganishwaji mdogo wa mashamba madogo. Lakini taratibu, kitu kinachofanana na soko katika utumizi wa ardhi kikaibuka.

Katika wilaya ya Meitan jimbo la Guizhou kwa mfano, wanakijiji na maafisa waliweka ukomo wa utumizi wa ardhi kwa miaka ishirini, hali iliyosaidia familia kufanya mipango ya muda mrefu. Wakulima walipewa uwezo wa kurithisha au kubadilisha muda wa umiliki na kuunganisha vipande vyao vya mashamba. Na kulikuwa na vichochea zaidi vya kutumia ardhi zisizolimwa. Matokeo yake, ardhi zaidi ikalimwa, na ubora wa ardhi ukaimarika kwa sababu familia zilijali zaidi na kuanza kutumia vifaa vya kisasa. Mwaka 1995, serikali ya kitaifa ikahimiza wengine kuiga mfano wa Meitan, na mfumo kama wa haki za umiliki mali katika ardhi ukaanza kuenea.

*Haki za maji*

Maji ni rasilimali nyingine adimu ambayo haki za umiliki mali zinaweza kuigawanya vyema zaidi ya serikali. Kwenye ukanda mkame wa magharibi wa Marekani, tishio la ukame lilikuwa kawaida, si kwa sababu ya uhaba wa amji, bali kwa sababu ya mfumo mkali wa kusimamia usambazaji wake. Kwa mfano, wale ambao walichimbua kwanza maji kutoka kwenye chemchemi, walikuwa na kipaumbele zaidi ya atakayekuja baadaye; lakini ili kuendelea kuwa na haki hiyo, walipaswa kuendelea kuchimba – hata ikiwa haja yao ya maji ilikuwa kidogo.

Mwanzoni mwa miaka ya 1990, majimbo kama Montana na Arizona yalianza kuruhusu watu kuuza haki zao za

maji. Wakati kungali miongozo mingi kuzuia soko hili, ilisaidia kuhakikisha maji yanaelekezwa katika matumizi ya mambo ya thamani zaidi. Kwa kuwa haki za rasilimali za maji zinaweza kununuliwa na kuuzwa, watumiaji wadogo (ambao wanaweza kutumia maji kidogo au yaliyobadilishwa kutumika upya) sasa wakawauzia haki za kuchimbua maji wale wenye uhitaji mkubwa zaidi. Hayo ni manufaa ya mfumo huu ambapo haki za maji sasa zimesambaa katika ukanda wote wa magharibi wa Marekani.

*Utaratibu wa ubinafsishaji*

Makampuni ya serikali mara nyingi ni ya kikiritimba, hayawapi wateja chaguo. Huweza na hutoza bei kubwa kwa bidhaa na huduma zenye ubora hafifu. Japokuwa yapo mbali na watawala, yakiratibiwa na mamlaka fulani, bado kwa kawaida hutawaliwa na tabaka tawala au marafiki zao

*Bonyads* wa Iran kwa mfano, japo wanachukuliwa kama asasi ya ufadhili, wanamiliki takribani moja ya tano ya uchumi wa Iran kwenye uendelezaji wa majengo, kilimo, uzalishaji bidhaa na usafirishaji kwa meli. Wakiwa wameasisiwa na Shah, wamekosolewa vikali kwa kutokuwa asasi za ufadhili hasa na badala yake kuwa vyombo vya ukandamizaji vya watawala kwa faida yao wenyewe. Hata hivyo, baada ya mapinduzi ya mwaka 1979, serikali mpya iliona yana faida mno, hivyo haikuifutilia mbali. Hivyo wakaendelea, wakifurahia msamaha wa kodi na ruzuku kutoka serikalini; na hata mali zilizotaifishwa zikawekwa chini yao.

Japo asasi hiyo iliasisiwa kuwasaidia masikini, lakini wanufaika wanaonekana kuwa wale waliopo mamlakani.

Ubinafsishaji wa biashara zinazoendeshwa na serikali unapaswa kuleta matokeo ya mabadiliko ya umiliki binafsi na ushindani katika urasimu hodhi na kuondoa nafasi ya rushwa kwa uwazi wa kibiashara.

Unaweza pia kusaidia kurejesha mtaji wa viwanda hivi kwa umma. Lakini ili kufikia haya yote, kunahitajika maono, uimara na uundaji sera makini.

Hakuna utaratibu mmoja. Kubinafsisha biashara zinazoendeshwa na serikali ni suala la kisiasa pia kama ambavyo ni la kiuchumi. Kila tasnia ni tofauti na itahitaji mbinu tofauti. Tasnia huwa za aina na ukubwa tofauti, na huwa na makundi tofauti yanayopinga mageuzi. Kwa hiyo, mbinu iliyotumika kwenye huduma za jamii kama umeme na maji ambavyo hugusa jamii nzima, inapaswa kuwa tofauti na ile itakayotumika kwa makampuni ya uzalishaji ambako watu wachache tu wataathirika.

Kwa makampuni madogo, inaweza kuwa sawa kuuza kwa waendeshaji wa kibiashara, hususani mgeni kutoka ughaibuni anayeweza kuwa na mawazo mapya na mtaji. Lakini uuzaji wa makampuni ya serikali kwa wageni unaweza kuwa wenye utata.

Kwa makampuni makubwa zaidi, inaweza kuwa jambo la busara kusambaza umiliki kwa wananchi kupitia kuuza hisa. Hili laweza kuhitaji zoezi kubwa la kuelimisha, kwani kunaweza kuwa na soko la hisa dogo tu na watu wasielewe hisa ni nini. Baada ya kuanguka kwa utawala wa kisovieti, Urusi ilianzisha 'ubinafsishaji wa vocha' ambao kwa ufanisi ambao uliwapa wananchi hisa sawa katika makampuni ya serikali. Lakiniwengi waliuza hisa hizi kwa bei ya kutupwa na umuliki wake ukaishia mikononi mwa tabaka jipya la mabwanyenye wachache.

*Kuanzisha kanuni za soko*

Ni vyema kuvunja makampuni hodhi kama mchakato wa ubinafsishaji. Serikali zaweza kudhani zitapata kodi zaidi kutokana na kampuni na ukiritimba wake, lakini nguvu ya kuhodhi huko bado kutasalia na madhara kwa wananchi. Ikiwa kampuni hodhi za serikali zitavunjwa kwenye kampuni ndogo shindani, serikali na watu wataweza kufaidika kwa muktadha wa kipindi kirefu. Makampuni mapya yatakuwa na nguvu zaidi, yenye kuendana na mabadiliko na bunifu kuliko mtangulizi wao mwenye ukiritimba.

Ubinafsishaji wa mwaka 1996 wa mfumo wa simu wa Guatemala unaonyesha umuhimu wa ushindani katika mchakato. Ushindani katika sekta ya mawasiliano ya simu ulifunguliwa kabla ya kampuni hodhi ya mawasiliano ya simu kubinafsishwa. Mawimbi pia yalibinafsishwa, hivyo kwa ufanisi kabisa kuunda haki za umiliki katika spectra ya kielektroniki, ambako makampuni mapya yanaweza kununua na kutumia kiurahisi. Matokeo yake yakawa upanuzi wa kiwango kikubwa wa ushindani, na kupelekea machaguo mengi zaidi na kufikiwa watu mahali pengi zaidi. Bei zikashuka na kuwa miongoni mwa bei za chini zaidi katika Amerika ya Kusini na idadi ya watumiaji wa simu za mkononi ikaongezeka kufikia mara mia kadhaa ndani ya muda wa takribani muongo mmoja.

*Kufanya kwa usahihi*

Kuna wingi wa uzoefu wa kimataifa – na utaalamu – ambao unaweza kuwasaidia wanamageuzi kupata siasa na mbinu za haki ya ubinafsishaji.

Jambo la msingi ni kwamba mchakato unapaswa

kuwa wa uwazi na jamii ihusika. Vinginevyo, maguezi hayatakubalika kiujumla. Kwa mfano, baadhi ya serikali za Afrika zimebinafsisha huduma za kijamii kama maji na mabenki kwa kuwakaribisha wageni pasipo kufungua fursa kwa wenyeji. Hii siyo tu si sahihi kisiasa, lakini pia ni kinyume na kanuni ya jamii huria ya kuwatendea wote kwa usawa.

Zaidi, ikiwa umiliki umewekwa kwa wachache badala ya kusambazwa kwa wengi, bado kunasalia hatari ya tasnia zilizobinafsishwa kuendelea kutamalaki na kuwamiliki wale waliopo katika serikali. Hiyo itatia sumu wazo la kubinafsisha zaidi na kuweka vikwazo hatua za kuanzisha kanuni za soko katika sekta nyingine zinazoendeshwa na serikali. Jamii inapaswa kuhakikishiwa kuwa mfumo mpya utawahudumia wateja na siyo watawala dhalimu wachache. Kuweka ushindani mkubwa kadri inavyowezekana, mapema iwezekanavyo, ni njia nzuri ya kuhakikisha hilo.

## Huduma za kibinadamu pasipo serikali

Kuna dhana kuwa baadhi ya huduma za kijamii zinaweza kutolewa tu na serikali – hasa zile za 'ki-binadamu' kama vile huduma ya afya, elimu na ustawi.

Baadhi ya watu hudai kuwa huduma hizo ni muhimu mno kwa soko kuachiwa. Kiuhalisia ni kwamba ni muhimu mno kiasi hazipaswi kuachiwa serikali. Pale watoa huduma wanapofadhiliwa na kodi, hawahitaji kuwaridhisha wateja wao ili kujipatia riziki kama ambavyo washindani katika sekta binafsi huhitajika kufanya. Namna wanavyokuza bajeti zao ni kuwashawishi wanasiasa au kutishia kuharibu ikiwa mahitaji yao hayatafikiwa. Mkazo wao upo kwa serikali na si kwa umma.

Makampuni binafsi hukumbana na ushindani zaidi ya yale yanayoendeshwa na serikali. Mara nyingi kushindana na huduma zitolewazo na serikali ni marufuku kisheria. Kwa hiyo, watoa huduma chini ya serikali huwa hawahitaji kuwa wabunifu au kuboresha huduma zao kwa kuwa wateja hawana sehemu nyingine ya kwenda.

Lakini kila serikali inapotaka kuhodhi utoaji huduma za umma, watu hutafuta mbinu ya kuizunguka. Kuna mifano mingi kote duniani ambako watoa huduma wasio rasmi na wasio wa kiserikali wanavyotoa huduma hizi muhimu – na wanazitoa kwa ubora zaidi.

*Elimu bila serikali*

Chukulia elimu kwa mfano. Watu wengi hudhania elimu ya shule binafsi ni kwa ajili ya matajiri. Lakini utafiti wa miaka miwili wa Profesa James Tooley katika nchi za India, Ghana, Nigeria na Kenya ulionyesha tofauti. Katika maeneo masikini zaidi ya nchi hizi, watoto wengi wa shule walikuwa wanahudhuria shule binafsi. Katika sehemu masikini zaidi za Hyderabad, Accra na Lagos, ni moja ya tatu au chini ya hapo ya shule zilikuwa za serikali. Mbili ya tatu au zaidi, ya watoto wa huko walikuwa wakienda shule binafsi, wengi katika zile zisizo rasmi, zisizotambuliwa na serikali. Wamiliki binafsi wanaendesha nyingi kati ya hizi shule zisizo za serikali. Ni chache sana zilipata msaada na hakuna iliyopata fedha kutoka serikalini – kipato pekee kikiwa ni ada za wazazi wao, ambazo nazo mara nyingi ni hafifu.

Pamoja na hayo, Tooley aligundua ufaulu ulikuwa juu zaidi kwenye shule za binafsi. Mjini Hyderabad, wastani wa maksi za hesabu ulikuwa karibu moja ya tano zaidi ya ilivyo kwenye shule za serikali – pamoja na ukweli

kwamba mshahara wa mwalimu katika sekta binafsi ulikuwa kati ya robo mpaka nusu ya ule wa walimu walioko serikalini. Viwango vingine vilevile vilikuwa juu zaidi. Tooley aliwakuta walimu katika shule za serikali wakiwa wamelala juu ya meza zao. Utoro wa walimu kwenye shule za serikali ulikuwa juu zaidi. Shule binafsi zilikuwa na mbao, viwanja vya michezo, madawati, maji ya kunywa na vyoo bora zaidi. (Ni nusu tu ya shule za serikali zilikuwa na vyoo, ikilinganishwa na asilimia zaidi ya 96 ya shule za binafsi.) uwiano wa wanafunzi na walimu ulikuwa karibu nusu ya ule wa shule za serikali.

Serikali inaonyesha hazioni umuhimu mkubwa wa elimu kupitia sekta binafsi katika maeneo masikini. Serikali ya China ina rekodi ya shule binafsi 44 tu katika jimbo la milimani la Gansu, japo utafiti wa Tooley ulipata shule 696, 593 kati yake zikihudumia watoto 61,000 katika vijiji vya pembezoni zaidi. Nyingi kati yake zilikuwa zikiendeshwa na wazazi na wanakijiji. Zilistawi pamoja na kwamba wastani wa kipato wa watu wa Gansu ni dola 150 tu kwa mwaka. Hata Kibera, Kenya - eneo kubwa zaidi la makazi duni kusini mwa jangwa la Sahara, likiwa na wakazi takribani 750,000 – Tooley alipata shule binafsi 76 zikiandikishwa wanafunzi 12,000.

Kwa uwazi kabisa, hata katika maeneo masikini zaidi duniani, jitihada binafsi zinaweza na zinatoa huduma ya elimu kwa viwango bora zaidi ya serikali. Na gharama yake ni chini kiasi cha kuzifanya familia masikini kuzimudu. Serikali haionekani kuhitajika kwenye elimu hata kidogo.

Haishangazi kuwa katika nchi tajiri, ambako mara nyingi kuna mtandao mkubwa wa program za shule za serikali, wako makini kuuleta ushindani huu katika elimu na

kuwapa wazazi chaguo. Mwaka 1991, Sweden ilianzisha mfumo ambapo serikali ingeendelea kutoa gharama za msingi za elimu, lakini makundi binafsi ya kibiashara na yasiyo ya kibiashara yanaweza kuanzisha shule zao na kupata fedha hizo za serikali kwa msingi wa idadi ya wanafunzi wanaoweza kuwavutia. Hata wapinzani kama vile umoja wa walimu ambao awali walipinga mfumo huu, sasa wanauunga mkono, kukiwa na matokeo katika kuimarika ufanisi, ubunifu na ubora wa shule zaidi ya elfu moja zilizoanzishwa - hasa katika maeneo magumu na masikini zaidi. Sasa nchi nyingine pia zimeanzisha mfumo kama huo.

*Huduma ya afya bila serikali*

Huduma ya afya ni moja ya huduma muhimu ambayo imetawaliwa na serikali katika nchi nyingi – huku mara nyingi ikilindwa kisheria dhidi ya ushindani, ruzuku kutokana na kodi na miongozo. Kwa mara nyingine tena, hii inaelekeza mkazo wa watoa huduma wa serikali kupata pesa zaidi na marupurupu zaidi kutoka serikalini, badala ya kutoa huduma bora zaidi kwa wagonjwa.

Marekani mara nyingi kukosolewa kwa kinachodaiwa kuwa gharama kubwa ya hudma ya afya ya 'ki-soko huria'. Ni kweli ni ya gharama; na ni ya tatu katika mifumo inayoratibiwa zaidi na serikali duniani (ikizifuata Norway na Luxembourg). Kodi na kanuni za kuongoza huduma ya afya zinajihusisha na kutaka bima kuwepo katika maeneo ya kazi, - zikiwaacha watu pasipo bima ya afya wakiwa kati ya kazi moja na nyingine. Wakati huo huo, waajiriwa (wakitiwa moyo na madaktari) wanataka vipimo na matibabu ambayo kiuhalisia hawahitaji kwa kuwa gharama huangukia kwa waajiri na si kwao. Kanuni pia zinaongoza nini kinachopaswa kuweko kwenye mikataba ya bima

ya afya na bei yake (kwa mfano, kuwazuia watoa bima kufanya kazi kwenye majimbo yao pekee, na kuwafanya kutopata fursa ya uchumi mkubwa). Vivyo hivyo, fani ya utabibu inaongozwa na mahitaji ya vibali ambayo mara nyingi yanabuniwa na madaktari wenyewe – hivyo kufanya taaluma kuzuia kuzuia upatikanaji wa madaktari na kufanya mishahara yao kubakia juu. Kanuni zote hizi na nyingine zaidi zinaongeza gharama ya huduma ya afya ya Marekani.

Kinyume chake – Singapore, nchi ndogo ambayo kiuhalisia ni tajiri zaidi ya Marekani – inatumia takribani moja ya sita ya matumizi yote kwa mwaka ya nchi ya Marekani kwa ajili ya miradi ya afya iliyofadhiliwa na serikali. Inahitaji tu kwamba familia zitunze moja ya tano ya mapato yao kwa ajili ya huduma za afya, kustaafu na makazi kwa hapo baadaye (japo kuna miradi inayofadhiliwa na serikali kwa mahitaji ya dharura ya kitabibu). Ukweli kwamba watu wanatunza pesa zao wenyewe kwenye akaunti zao za akiba za afya inawafanya kujali ubora, na madaktari binafsi wanashindani kwa ajili yao.

Nchini Uswisi, hakuna bima inayoendeshwa naserikali: watu hununua huduma za bima na za afya kutoka kwa watu binafsi. Kazi ya serikali imebakia kutoa ruzuku tu, si kwa watoa huduma, bali kwa wagonjwa wasioweza kumudu huduma za afya wao wenyewe. Hivyo, tofauti na Wamarekani, raia wa Uswisi wako katika nafasi nzuri zaidi ya thamani ya pesa yao wanayoitumia katika huduma ya afya. Watu wengi wa Ulaya wanachukulia mfumo wa soko huria wa Uswisi kama mfumo bora zaidi wa afya ulimwenguni.

*Ustawi bila serikali*

Namna bora zaidi ya ustawi kwa mtu masikini ni kuwa na kazi inayolipa. Lakini miradi ya ustawi ya serikali huharibu kazi. Barani Ulaya, 'bima ya jamii' hufadhiliwa kwa kodi maalumu kwa walioko kazini, kitu amabcho huongeza gharama kwa waajiri na kuwafanya kusita kuajiri watu zaidi. Hii humaanisha watu wengi zaidi hutegemea mafao ya kukosa kazi ambayo huhitaji kodi zaidi kuyafadhili, hivyo wachaceh hata zaidi kuajiriwa. Huo ni mzunguko wa kuelekea chini.

Sweden ilikuwa nchi huru, yenye kiwango cha chini sana acha kodi na yenye utajiri mpaka kufikia katikati ya karne ya ishirini. Halafu kwa miongo miwili kuanzia mwaka 1970 ikaanza kutoza kodi kubwa ili kufadhili miradi yake mikubwa ya ustawi. (mwaka 1976, mmoja wa waandishi wa Sweden alilalamika kuwa kiwango chake cha kodi ya jumla kilifikia asilimia 102!) kodi hizi za juu zilikuwa na athari kwa kazi na biashara. Zilipekea ukuaji duni wan chi ya Sweden mpaka pale sera hiyo ilipoanza kugeuzwa miaka ya 1990.

Nchi huru zina kawaida ya kuwa tajiri zaidi, na huwa na kawaida ya kutumia pesa zaidi kwenye shughuli za misaada kwa wahitaji. Hii kimaadili ni sawa zaidi kuliko kwa serikali kuchukua pesa kutoka kwa watu kupitia kodi na kuzitumia katika miradi ya ustawi ya kubuni wao wenyewe – na sit u kwa sababu serikali huwa na kawaida ya kupendelea rafiki zao na kutoza kodi kubwa kwa maadui wao. Hisani ya kweli ni kutoa kwa hiyari kutoka kwa mtu mmoja kwenda kwa mwingine badala ya kulazimisha.

Tatizo lingine la miradi ya maendeleo inayofadhiliwa na serikali ni kuwa hujenga utamaduni wa utegemezi. Kwa

kuwa ni kubwa, zikiendshwa na wafanyakazi wa umma, hufanya kazi kwa misingi ya kanuni badala ya tathmini binafsi na uhitaji na manufaa yanayoweza kupatikana, kama ambavyo hisani ya kweli hufanya. Hii hufanya watu kuchezea kanuni ili kuhakikisha wanafuzu. Mara nyingine familia masikini hushusha zaidi hali zao ili zionekane mabaya zaidi ili tu kupata manufaa ya juu zaidi – kinyume kabisa ya tunachotaka kukifikia. Katika nchi kongwe na kubwa zaidi kiustawi kama Uingereza, maaafisa sasa wanashuhudia kizazi cha tatu cha utegemezi – familia zinazoishi kwa kutegemea ruzuku kama walivyofanya wazazi na mababu zao kabla yao.

Kujisaidia wenyewe, kukiungwa mkono na hisani ya hiyari ni ya ki-utu zaidi, inayotia motisha zaidi na mbadala wenye ufanisi zaidi. Uingereza ilikuwa na mfumo uliokuwa ukikua wa tabaka la wafanyakazi kabla ya miaka ya 1940, lakini miradi ya maendeleo ya serikali ikpelekea kufutika. Jumuiya hizi zilikuwa za kirafiki ambapo wanachama walikuwa wakitoa mchango wa kila wiki na wao wakipata manufaa kama ruzuku ya kukosa ajira, bima ya afya na hata gharama za mazishi. Kwa kawaida zililenga aina fulani ya kazi ili waweze kuhudumia mahitaji maalumu ya wafanyakazi hao. Mamilioni ya familia, hasa familia masikini, ziliamua kuwa wanachama wa mojawapo ya jumuiya hizo. Ustawi kwa wote, bila serikali, unawezekana kabisa.

*Kufufua sekta ya ufadhili*

Watu wengi waishio kwenye nchi zenye mifumo ya kisasa ya ustawi iliyowekwa na serikali, wanadai kuwa hisani na ufadhili binafsi hauwezi kuchukua nafasi ya ukarimu unaofanywa na ruzuku za kijamii na pensheni zilizofadhiliwa kwa kodi. Ni rahisi sana serikali kuwa

‘karimu’ kwa pesa za watu, na kuna kila sababu kwa wanasiasa kutoa ahadi za manufaa ya kupindukia kwa sasa, wakijua vizazi vijavyo ambavyo havijazaliwa bado ndivyo vitakavyolipa. Hiyo tu ingetosha kuwa sababu ya kuwaweka wanasiasa nje ya ulingo wa huduma za jamii. Lakini zaidi ni kuwa ikiwa maslahi ya kutoka serikalini ni ya juu, kunakuwa na vichochea hafifu kwa familia kujitunza zenyewe na watu kutafuta kazi badala yake kutegemea ruzuku – hata zaidi ikiwa walioko kazini wakitakiwa kulipa kodi za juu zaidi ili kufadhili huduma za kijamii. Japokuwa hii ina lengo zuri, matokeo yake huwa ni kuwaondolea watu tumaini na msukumo na kuwasukumia kwenye maisha ya utegemezi.

Nchi zinazihitaji kuhamia kwenye uelekeo huria zinapaswa kuanza kwa kuzivunjavunja sekta zao kubwa za huduma za jamii katika mifumo midogo ya eneo dogo. Wanaweza hata kuzibuni kwa namna ya kufaa mahitaji binafsi katika aina fulani ya akaunti binafsi ya mtu. Wanaweza kuzisaidia familia kutambua majukumu yao na kuelewa kuwa wanasaidiwa na walipakodi halisi, na sio mfumo fulani ‘bwana kubwa’. Na kwa kuivunja-vunja mifumo kwa namna kama hii, inaruhusu ufanisi zaidi katika uendeshaji wake, kupitia watoa huduma wa sekta binafsi.

Mfano ni kwa mfumo wa pensheni wa Chile. Mwaka 1981, nchi hiyo iliugawanya mfumo wake wa pensheni uliokuwa ukifeli kwenda kwenye akaunti binafsi. Wafanyakazi walihitajika kutunza akiba kwa ajili ya kustaafu, lakini wangeweza kuchagua miongoni mwa watoa huduma wengi binafsi kutunza akiba yao. Mfumo ulichochea uwajibikaji katika akiba na ukapelekea manufaa zaidi kwa wafanyakazi na kuanzia hapo ukaigwa ban chi nyingine katika mabara kadhaa.

Mfano mwingine ni mfumo wa akaunti za akiba za afya wa Singapore (kama ilivyotangulia kuonyeshwa), ambao unaweka majukumu kwa watu binafsi na familia, hivyo kuwachochea watu kukimu mahitaji yao ya afya na mengineyo wao wenyewe. Mfumo wa zamani wa Uingereza wa jumuiya za kirafiki ni mfano mwingine ambao unaweza kufufuliwa kwa kunyumbua mifumo ya mafao ya serikali kwenda kwenye akaunti binafsi za watu.

Pale ambapo mfumo wa serikali uliofeli unaporekebishwa kwa namna kama hiyo, kuna vichocheo zaidi kwa watu kutafuta kazi na kutegemea jitihada zao wenyewe kukimu mahitaji ya familia zao badala ya kutegemea serikali. Bado kutahitajika hisani na ufadhili wa watu binafsi, lakini utakuwa katika kiwango wanachokimudu. Na kama tulivyoona, uhuru na viwango vya chini vya kodi ni njia nzuri ya kuwapa watu nia na utajiri wa kuwa wakarimu, msukumo ambao serikali kubwa inayofanya yote na kodi kubwa huuzima.

## Utandawazi na biashara

*Faida za utandawazi*

Kama ilivyo kwa Nepal, nchi nyingi zinahofia namna ambavyo kuongezeka kwa utanawazi wa masoko kutawaathiri. Lakini hofu hiyo kwa kiasi kikubwa imeelekezwa ndiko siko, na manufaa yatokanayo na utandawazi na biashara ni makubwa. Ushukuriwe mfumo wa bei za soko, sasa tunaweza kufanya biashara kwa namna ya moja kwa moja na isiyo ya moja kwa moja na watu wa duniani kote. Mavazi tunayovaa, chakula tulacho, vifaa katika nyumba zetu, ofisini na viwandani, vyote kwa namna ya kushangaza ni zao la nchi nyingi zilizo mbali.

Lakini utandawazi wa soko hufanya kazi katika njia zote. Hauzisaidii nchi tajiri tu kununua bidhaa kutoka pande zote za dunia. Unawasaidia pia watu waliokuwa katika nchi za pembezoni kuboresha matarajio ya ustawi wao kwa kupenyeza bidhaa zao katika masoko ya kimataifa. Zao gani kwa mfano mkulima alime? Awali, chanzo pekee cha taarifa juu ya bei za mazao ilikuwa ni mawakala wa serikali au wafanyabiashara wenyeji, ambao walikuwa na maslahi yao binafsi. bei zingeweza kufumuka mno kulingana na sababu kadhaa kama vile hali ya hewa. Masoko ya ndani mara nyingi hayakuwa katika mpangilio mzuri. Leo, mkulima anaweza kuchukua simu yake ya mkononi na kutazama tovuti nyingi zinazoorodhesha bei za sokoni – ikiwemo bei zinazotarajiwa baadaye – kwa karibu kila zao, katika masoko mengi duniani kote. Wakulima kutoka popote pale sasa wanaweza kuuza katika soko lililopangiliwa, soko la kimataifa katika bei inayotabirika zaidi.

*Kuifungua New Zealand*

New Zealand ni mfano wan chi iliyobadilishwa kwa kuachana na udhibiti katika biashara. Mwanzoni mwa miaka ya 1980 ilikuwa katika hali mbaya na ngumu kiuchumi hasa kwa sababu ya udhibiti mkubwa uliokuwepo. Lakini kuaznia mwaka 1984, iliachana na ukingaji na ikaiweka huria biashara yake ya kimataifa, kufungua masoko yake kwa ushindani wa kimataifa. Ruzuku kwa viwanda na kilimo ziliondolewa. Udhibiti katika masoko ya ndani uliondolewa, ikiwemo katika soko la ajira lilikuwa limedhibitiwa sana: uanachama katika vyama vya wafanyakazi uliachwa kuwa wa hiyari na mikataba iliachiwa majadiliano baina ya wafanyakazi na wasimamizi wao.

Tabiri za kutisha kutoka kwa makundi ya ushawishi, wanataaluma viongozi wa kidini na maafisa wa vyama vya wafanyakazi – kuwa kuondoa udhibiti kutatengeneza ‘uchumi wa kutaabika’ – zote zilithibitika kuwa ndiyo siyo. Wastani wa malipo uliongezeka. Mikataba ya malipo ilikamilishwa haraka zaidi. Migomo ilififia kufikia kribu kutokuwepo kabisa. Kiwango cha kutoajiwa kikashuka – na kikashuka kwa kasi zaidi miongoni mwa Wamaori, wahamiaji na makundi mengine yaliyo kwenye hali ngumu. New Zealand ikawa moja ya nchi zilizo huru na zenye ushindani zaidi duniani.

*Utambulisho wa utamaduni*

Baadhi ya watu wanahofia kuwa utandawazi wa masoko utazinyang’anya nchi utambulisho wa kipekee wa utamaduni wao. Kiupambanuo zaidi, kusambaa kwa makampuni ya Kimarekani kumeibua hofu kuwa nchi zilizokuwa tofauti zitaanza kuonekana kuwa zinafanana, kwamba bidhaa za kimagharibi na mitazamo yao itaelemea ya mahali pengine, na kwamba tamaduni kubwa zaid za duniani zitaelemewa na kiwango cha chini cha kawaida kwa wote.

Hakika ni kuwa uchumi na tamaduni zinabadilika. Bidhaa zilizokuwa zikipatikana tu nchi moja, sasa hivi ni kawaida kuzikuta katika mitaa ya nchi zote. Hii haimaanishi machaguo na bidhaa tofauti vinapotea. Kinyume chake, inamaanisha watu wa mataifa yote sasa wana chaguo kubwa zaidi ya walilokuwa nalo. Wananchi wa Uingereza kwa mfano, hawahitaji kuvumilia chakula kisichovutia na kilichopikwa mno, kitu ambacho ilikuwa maarufu kwacho. Sasa wanaweza kupata migahawa, vyakula vya kufunga na maduka makubwa yakiuza chakula cha Kihindi, ki-Vietnam, Amerika Kusini, Irani, Kimongolia,

Kipolandi na aina nyingine nyingi. Na wengine kote duniani wanafurahia machaguo kama hayo – ambayo mwanzoni waliyafaidi wachache waliokuwa na utajiti wa kutosha kusafiri. Si kwamba tamaduni zinapotea; badala yake zinasambaa ili kwamba kila mmoja aweze kuzifurahia.

Tamaduni huwa hazisalii vilevile pasipo kubadilika, kama ambavyo wanaotaka kuzilinda dhidi ya utandawazi wanajaribu kumaanisha. Utamaduni wan chi hubadilika kila wakati, na kadri utamaduni ulivyo hai, ndivyo huweza kutengeneza mawazo mapya ya kitamaduni na kubadilika zaidi. Sanaa, muziki, fasihi, mitindo ya maisha, ladha na fasheni za nchi zenye utamaduni hai zaidi zinaweza kutotambulika na watu walioishi karne iliyopita tu.

Tamaduni huvuna kwa kuchangamana na tamaduni nyingine, zikiwaruhusu watu kuchukua vijitabia vya wengine vinavyowafaa katika maisha na wakati wao. Kupitia biashara ya kimataifa tunapata nafasi ya kuona na kuelewa utamaduni kutoka ng'ambo ambao tunaweza kuuiga ukatufaa kuuchanganya na wa kwetu. Lakini mchakato huu wa mabadiliko ulikuwepo muda mrefu kabla ya yeyote kuzungumzia utandawazi.

Mabadiliko mengi tunayojutia zaidi, kama upotevu wa sehemu za kuvutia zaidi za utamaduni wetu, si kwa sababu ya ubeberu wa kitamaduni kutoka ughaibuni, bali ni kutokana na matokeo madogo ya uendelevu. Sherehe za kale, desturi na mavazi ya kitaifa yanatoweka, si kwa sababu ya utandawazi, lakini kwa kuwa maisha yenyewe yanabadilika. Sikukuu ambazo awali ziliashiria majira fulani muhimu kwa jamii ya wakulima, sasa hivi hazina mashiko sana katika ulimwengu ambao takribani nusu yetu tunaishi katika majiji.

**Swali: Je, nchi tajiri hazikombi utajiri mwingi zaidi wa dunia?**

Hapana. Utajiri ni kitu unachokitengeneza, kupitia ujuzi, biashara, nguvu, jitihada, mpangilio na uwekezaji. Hakika nchi tajiri hupata utajiri, lakini wanautengeneza pia. Na si kwa ajili yao tu; wanavumbua na kutengeneza bidhaa muhimu na michakato inayosaidia kuboresha maisha ya kila mmoja, hususani kwa ajili ya maisha ya watu masikini zaidi duniani.

Maendeleo katika madawa kwa mfano, yanasaidia kuondoa baadhi ya magonjwa yenye kulemaza zaidi ulimwenguni kama vile kifua kikuu na malaria. Teknolojia ya kibaiolojia inasaidia kukuza mavuno na kutengeneza mchele unaohimili wadudu na mazao mengine. Malighafi mpya zinasaidia kufanya majengo kuwa nafuu na imara zaidi.

Hakuna ukomo wa mtiririko wa utajiri, kiasi cha kusema nchi tajiri zinakomba zaidi bila usawa. Kinyume chake, utaalamu wa nchi tajiri unatengeneza fursa mpya kwa ajili ya watu wengine.

Pengine ni vizuri pia kuwa tamaduni zinabadilika. Tamaduni nyingi katika nchi nyingi zilishurutishwa kupitia watawala wa kikoloni, na kiasi kikubwa cha tamaduni za nchi zisizo huru zaidi ni za kiuharibifu kwa uhalisia. Tunapaswa kukaribisha ukweli kuwa kuimarika kwa usafiri na uchunguzi mpana zaidi umafanya kuwa vigumu kwa nchi kuendeleza utamaduni ambao baadhi ya makundi yalikuwa yakidhulumiwa, kunyanyaswa na kutengwa.

## Umuhimu wa amani

Adam Smith aliwahi kuandika: ‘Vichache tu zaidi huhitajika kuibeba nchi kwenda kwenye kiwango cha juu zaidi cha ukwasi kutoka viwango vya chini zaidi vya ushenzi, ila amani, kodi ndogo na usimamizi wa kuvumilika wa haki…”

Amani ndani na nje ya nchi ni mahitaji muhimu kwa ajili ya uchumi huria unaokua vyema. Watu hawataweza kuwekeza katika viwanda na mtaji wa uzalishaji ikiwa wanaamini kuwa utajiri wao unaweza kuporwa na wanamgambo na majeshi vamizi. Na nchi ambazo wananchi wake wanajihusisha na biashara na nchi zingine hawatakuwa katika nafasi ya kutaka ugomvi nao. Kwa maneno yaliyotolewa na mchumi wa Ufaransa wa karne ya kumi na tisa, Frédéric Bastiat; 'Ikiwa bidhaa hazivuki mipaka, majeshi yatavuka'

Manufaa ya amani ni kote, kiuchumi na kitamaduni. Amani huruhusu jitihada na rasilimali kuelekezwa kwenye uzalishaji badala ya uharibifu. Inatengeneza mazingira kwa utengenezaji wa mtaji na uchumi huru unaostawi. Inawaruhusu watu kupangilia kesho yao na ya familia zao. Inawapa muda, utajiri na uhakika wa kujishughulisha na mambo ya kitamaduni na kitaaluma. Na amani husaidia uhuru wa kusafiri wa watu, bidhaa na mawazo – kusambaa kwa uelewa, ustawi na uvumbuzi.

Umaizi mwingine wa Adam Smith ni kuwa, hatuna haja ya kuzifanya nchi nyingine masikini ili kuwa matajiri. Ni vyema zaidi kwetu ikiwa wateja wetu ni matajiri kuliko wakiwa masikini. Vivyo hivyo, ili kuwa wenye nguvu hatuhitajiki kuwafanya wengine kuwa wadhaifu. Pande zote hufaidika na manufaa ya amani.

Amani kwa kipindi na kipindi huhitajika kupiganiwa. Mali na watu ni lazima kulindwa. Na kukusanya pamoja rasilimali muhimu kunaweza kuhitaji kuhusika kidogo kwa serikali. Lakini serikali zinazokuwa kubwa sna mara nyingi huwa za kijeshi pia – kwa kujaribu kuficha ukosefu wa ustawi na uhru kwa kudai kuwa usalama wa nchi unahitaji kujitoa mhanga, muunganiko wa lengo

na nguvu ya kijeshi. Watu katika jamii huru si kuwa si wazalendo zaidi kwa nchi zao; lakini wamejitoa kwa ajili ya jamii iliyo waiz na huria na kwa ajili ya familia zao, marafiki, wateja wao na asasi zao za hiyari – na si kwa ajili ya dikteta, bendera au kwa ajili ya ndoto fulani ya utaifa.

Baadhi ya watu hudhania kuwa njia ya kupatikana kwa amani ni kuanzisha serikali fulani kuu ya dunia. Wakati inafaa kuwa na majukwaa ya kimataifa ambako tofauti zinaweza kusemwa na migogoro ambayo ingeweza kutokea kuzimwa, hatupaswi kudhania kuwa serikali ya dunia inaweza kuwa yenye kufaa zaidi ya hizi za kitaifa zilizopo. Kizingatiwa ukubwa wake, na hata umbali wake mkubwa kutoka kwa umma, nafasi yake ya kutanuka na kutumia madaraka yake vibaya ni kubwa zaidi. Na hakuna atakayeweza kuepuka udhalimu huo kwa kukimbilia sehemu nyingine ya dunia. Hapana, njia bora ya kuchochea amani ni kuzifanya serikali kuwa ndogo, na si kubwa zaidi, na kutegemea kawaida ya asili ya wanadamu kushirikiana kwa amani na kuboresha hali za kila mmoja.

# 9 MJADALA KWA UFUPI

## Kuhusiana na uhuru

Uhuru huleta ustawi. Jamii zilikumbatia uhuru zimeweza kujipatia utajiri. Zile zisizokumbatia uhuru zimabakia masikini.

Lakini jamii huru ni kuu zaidi kwa namna isiyo ya mali pia. Inaendeshwa kwa misingi ya kuaminiana na ushirikiano baina ya watu, si misingi ya nguvu na mabavu. Wananchi wake wana ukaribu zaidi kitamaduni na kimaadili. Wanakubali kanuni za tabia baina ya watu kwa hiyari na kwa manufaa ya wote, si kwa sababu zimelazimishwa juu yao. Serikali zao zinajali wanaoongozwa, na wao wenyewe wanaongozwa na kanuni zinazowazuia kutumia vibaya mamlaka yao.

Jamii huria hufungulia vipawa vya watu, ubunifu na uvumbuzi. Hilo husaidia kutengeneza utajiri ambao haujakuwepo awali. Watu katika jamii huria hawawi matajiri kwa kuwanyonya wengine kama ambavyo watawala wan chi zisizo huru hufanya. Hawawezi kuwa matajiri kwa kuwafanya wengine masikini. Wanakuwa matajir tu kwa kuwapatia wengine wanachokihitaji na kufanya maisha ya watu wengine kuwa bora.

## Serikali yenye mpaka

Watu wengi hukubaliana kuwa serikali huhitajika kwa ajili ya majukumu kama vile kusimamia haki na kufanya maamuzi ya mambo ambayo mtu mmoja hawezi kuamua peke yake. Lakini pia karibu kila mtu anakubaliana kuwa nguvu ya serikali inapaswa kuwa na ukomo. Serikali ya jamii huria ipo kwa ajili ya kuzuia madhara hayawatokei kwa raia wake. Itahakikisha uwepo wa haki – na kanuni za asili zinazowezesha binadamu kushirikiana pamoja kwa amani.

Serikali ya jamii huria imebanwa na utawala wa sheria. Sheria hufanya kazi kwa kila mmoja kwa usawa. Viongozi wake hawawezi kupora wananchi wake kwa manufaa yao na kuwapendelea marafiki zao au kutumia nguvu yao dhidi ya maadui zao. Nguvu yao na muda kipindi chao cha uongozi huwa na ukomo ili kupunguza ufisadi ambao huambatana na kuwa na mamlaka. Taasisi za kidemokrasia kama vile uchaguzi huru na haki, haki ya kuzungumza kwa uhuru, ukomo wa vipindi kwa wawakilishi na kanuni za kikatiba hudhibiti mamlaka ya viongozi wa kisiasa.

## Usawa mkubwa zaidi

Wanufaika wakuu wa mfumo wa uchumi huria wa jamii huru ni watu masikini. Jamii huria huwa na usawa zaidi kiuchumi kuliko jamii zisizo huru. Masikini katika nchi zilizo huru zaidi hufurahia fahari ambazo hazikufikirika miaka michache tu iliyopita, fahari ambazo watawala tu wa nchi zisizo huru pekee ndiyo hufurahia.

Jamii huria hazijaribu kulazimisha usawa wa mali. Inatambua kuwa kujaribu kusawazisha uwiano wa utajiri

au kipato huwa hakuleti matokeo mazuri. Huharibu vichocheo vya watu kujiongezea thamani, bidii ya kazi na shughuli za biashara. Hukatisha watu tamaa ya kukuza mtaji ambao unasaidia kukuza uzalishaji wa jamii nzima. Huzuia watu kutengeneza utajiri na thamani mpya. Lakini jamii huria hufurahia usawa mwingine ambao hauko katika jamii zisizo huru. Usawa wa maadili unatambulika: maisha ya kila mtu yanachukuliwa kuwa ya thamani na yanayostahili kulindwa. Kuna usawa mbele ya sheria: hukumu hutegemea ukweli wa kesi, na si wewe ni nani. Raia wana usawa wa kisiasa: wote wana haki ya kupiga kura, kupigiwa kura na kuelezea maoni yao kisiasa, bila kujali namna watawala watajisikia. Na kuna usawa wa fursa: watu hawabaguliwi katika kazi au elimu na wanaweza kujiendeleza bila kujali mbari yao, dini, ukabila au sifa zingine zozote.

## Uchumi huria

Jamii huru huwapa watu uhuru wa kufanya maamuzi yao wenyewe kuhusiana na uchumi, kama ammbavyo huwaacha huru kufanya maamuzi yao kwa mambo binafsi na ya kijamii. Watu katika jamii huria hutengeneza thamani kupitia biashara huria. Biashara huria hunufaisha pande zote husika: wasingefanya vinginevyo.

Watu hustawi kwa kushirikiana na wengine na kusambaza bidhaa wanazozihitaji – na kupata wanachokihitaji. Matarajio ya kunufaika yanawatia moyo wajasiriamali kutafuta vitu wanavyohitaji watu wengi na kuwasambazia. Bei huonyesha kuhusu uhaba waka na wingi wake, zikiambia kila mmoja nini kinahitajika kuzalishwa na nini kinahitaji kutunzwa. Kwa njia hii, muda, ujuzi, jitihada, mtaji na rasilimali nyingine hupelekwa kule zinakohitajika

na kuondolewa kule ambako hazina matumizi muhimu zaidi. Haihitaji serikali kuwaambia nini cha kufanya.

Ili kufanya kazi, uchumi huria unahitaji tu mfumo unaokubalika wa kanuni za namna gani watu wanashirikiana kwa pamoja. Hii inajumuisha sheria za umilika na uhamishaji wa mali, na sheria za mikataba ambayo makubaliano hayo yataheshimiwa. Mali binafsi ni muhimu ikiwa watu watahitajika kujenga biashara na kuuziana bidhaa. Lakini ni muhimu pia ikiwa uhuru mwingine ukiheshimiwa. Ikiwa mamlaka zinatawala mali zote, mchakato wa kisiasa na mjadala huru hushindikana.

## Haki na utawala wa sheria

Haki si kitu kinaweza kuamrishwa na watunga sheria. Kanuni za haki ni sehemu ya asili ya wanadamu – sehemu muhimu ambayo husaidia kuchochea mahusiano ya amani baina ya watu.

Watu katika jamii huria wana haki ya haki hii ya asili sifa ya kibinadamu. Haki ya asili inasema kuwa sheria zinapaswa kuwa wazi na hakika, na zinazowatendea watu kwa usawa, kwamba hazihitaji yasiyowezekana na kwamba si za kizamani, na adhabu zinatabirika na ni kulingana na kosa lililofanyika. Kunapaswa kuweko mchakato wa kisheria kwa kesi zote, kukiwa na uendeshaji mashtaka pasipo uonevu na kutokuwa na kushikiliwa watu kwa muda mrefu pasipo mashtaka. Watu wanaoshitakiwa kwa makosa wnapaswa kuchukuliwa kuwa hawana hatia mpaka watakapothibitika vinginevyo, na watu hawatapaswa kudhalilishwa kwa kushitakiwa kwa jambo hilohilo mara nyingi. Kanuni hizo zinakubalika na karibu

kila mmoja pasipo kujali nchi wanakotoka, utamaduni wao, mbari zao au dini zao.

Kuhakikisha uwepo wa haki hii ya asili na kuhakikisha uwepo wa utawala wa sheria kunahitajika mfumo huru wa mahakama ambao hauwezi kuchochewa na wanasiasa. Polisi vilevile, wanapaswa kuwa huru. Hongo na rushwa haviwezi kuvumilika kwa askari polisi na mahakama ikiwa uhuru unapaswa kuendelea kuwepo.

## Jamii huria

Jamii huru ni jamii huria. Inajengeka kutokana na matendo ya watu, ikifuata kanuni zinazokuza ushirikiano wa amani. Haijawekwa kutokea juu kwa mamlaka ya kisiasa.

Si lazima watu kukubaliana na kila kitu ili kushirikiana kwa kufaidiana. Wanaobadilishana bidhaa wanahitaji tu kukubaliana na bei. Lakini ili ushirikiano huo kuwa wa manufaa zaidi, watu hupaswa kuvumilia matendo na mtazamo wa wengine. Jamii huru huruhusu watu au serikali kuingilia kati tu ili kuzuia madhara kutokea kwa wengine. Kuzuia uhuru wa watu kwa sababu tu tuonaona tabia zao hazikubaliki au ya kuchukiza huondoa kizuizi dhidi ya uhuru wa mtu yeyote kuchezewa na yeyote anayejifikira kuwa juu zaidi kimaadili.

Kuvumilia mawazo na mtindo wa maisha wa wengine hunufaisha jamii. Ukweli siyo waziwazi siku zote, huibua katika mapambano ya mawazo. Hatuwezi kuamini udhibiti pekee kugandamiza mawazo yasiyo sahihi. Udhibiti hugandamiza mawazo na njia za kutenda ambazo zingenufaisha jamii hapo baadaye.

## Ulimwengu wa uhuru

Inazidi kuwa vigumu kwa serikali za mabavu kuficha matendo yao kwa wengine. Matokeo yake, nchi nyingi zaidi zinafunguka kibiashara na utalii, na mawazo mapya yanazidi kusambaa. Watu zaidi wanazidi kuona manufaa ya uhuru wa kiuchumi na kijamii na wanautaka.

Ni vigumu kuweka maadili na taasisi za jamii huru mahali ambapo uhuru haupo. Badala ya kufanya mabadiliko ya jumla, ni vema zaidi kuanzia chini na kutengeneza mazingira yatakayoruhusu watu kutenda kwa uhuru na kujenga jamii huru kwa matendo yao. Sehemu muhimu ya hili ni kuwapa watu haki za umiliki mali, ili kwamba watu waweze kujenga biashara kwa kujiamini kuwa mali zao hazitataifishwa.

Mageuzi yanapaswa kuleta uhuru wa kweli wa kiuchumi, na si ubepari wa kiupendeleo. Serikali nyingi zinazosema kuwa zinabinafsisha viwanda vya serikali mara nyingi hupeleka umiliki huo kwa marafiki zao na ndugu zao wa karibu. Watu wote wanapaswa kuhusishwa na mchakato wa mageuzi ili kuleta mabadiliko ya kweli.

Nchi hazipotezi kwa kufungua milango yao kwa biashara ya kimataifa. Kulinda wazalishaji wa ndani dhidi ya ushindani maana yake kuwa na bei ghali zaidi na viwango duni kwa watumiaji wa ndani. Kuwa sehemu ya jumuiya ya kibiashara ya kimataifa kunawapa wajasiriamali wa ndani masoko na fursa mpya. Kunguka kibiashara kwa takribani miongo mitatu iliyopita kumeinua zaidi ya watu bilioni moja kutoka kwenye umasikini wa kutupwa. Uhuru kwa kweli umekuwa moja ya msukumo wenye kufaa na wa faida zaidi katika historia ya wanadamu.